ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nne – Tarehe 28 Machi, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

TAARIFA YA MHE. NAIBU SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza shughuli zetu nina maelezo machache. Kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema baada ya mapumziko ya mwisho wa wiki. Leo tunategemea kazi yetu tukishamaliza maswali na majibu tuna wachangiaji watano tuwamalize ili tumwite Mhe. Waziri tuweze kuukamilisha mswada huu.

Jioni tunategemea kumwita Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ili kuwasilisha Mswada wake unahusiana na masuala ya watoto. Kwa hivyo, hiyo ndio taarifa ahsanteni.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Mtoto itakayotoa Haki na Maslahi Bora ya Mtoto, itakayoshughulikia Watoto na Matatizo na Sheria, Ulezi, Ukaaji, Kumuona na Kumtunza Mtoto, kuwasili hatua maalum za Kinga kuhusiana na Mtoto, Ridhaa ya Utabibu wa Kidaktari itakayoanzishwa Skuli za Marekebisho, Makaazi na Matunzo ya Kutwa itakayorekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na kusahihisha sheria zinazohusiana na mambo hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hatu mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Mtoto itakayotoa Haki na Maslahi Bora ya Mtoto, itakayoshughulikia Watoto na Matatizo na Sheria, Ulezi, Ukaaji, Kumuona na Kumtunza Mtoto, Kuwasili hatua maalum za Kinga kuhusiana na Mtoto, Ridhaa ya Utabibu wa Kidaktari itakayoanzishwa Skuli za Marekebisho, Makaazi na Matunzo ya Kutwa itakayorekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Kusahihisha sheria zinazohusiana na mambo haya. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 136

Kuripuka kwa Mabomu katika Baadhi ya Kambi za Jeshi Tanzania

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kumekuwa na matukio ya kuripuka mabomu katika baadhi ya kambi za jeshi huko Tanzania Bara na kusababisha vifo vya watu na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi na kuwaacha wananchi wakiwa na huzuni na unyonge mkubwa.

Je, serikali imejipanga vipi kwa upande wa Zanzibar kudhibiti matukio kama hayo hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 136 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli matukio ya kuripuka mabomu katika baadhi ya Kambi za Jeshi huko Tanzania Bara husababisha vifo vya watu na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi. Serilai imehuzunishwa sana na matukio haya na tunatoa mkono wa pole kwa wananchi wote walioathirika.

Kwa kuwa ulinzi wa taifa ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo hatua zinazochukuliwa kudhibiti matukio hayo kwa upande wa Tanzania Bara ndio hizo zinazochukuliwa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tayari serikali imewasiliana na taasisi husika ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na hivi sasa JWTZ linaendelea na kuandaa mikakati maalum ya muda mfupi na mrefu itakayohakikisha inasaidia kuondoa madhara ya miripuko. Mara jeshi letu litakapomaliza kazi hiyo, Baraza lako tukufu litajuilishwa rasmi hatua zilizofikiwa.

Aidha, nachukua fursa hii kuwashauri wananchi wanaoishi na kulima karibu na kambi za jeshi waache tabia ya uchomaji moto karibu na maeneo hayo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kuna mikakati maalum inayochukuliwa ya muda mrefu na mfupi, mimi ningeomba kujua mikakati hiyo ni ipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, mikakati ya muda mfupi ni ile ya kuhakikisha kwamba miripuko inayotokea kuondolewa katika maeneo ya kambi ambazo ziko karibu na makazi ya wananchi ili mabomu hayo sasa yawe yamekaa mbali na maeneo ya makazi ya wananchi. Lakini mikakati ya muda mrefu ni ile kujenga maghala ya silaha ambayo hata ikitokea miripuko maghala hayo hayawezi kutoa taathira kwa wananchi walio karibu na maeneo haya na hii itatokana na uwezo wa kifedha kadiri ya bajeti itakavyoruhusu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa kama tunakumbuka miripuko hii katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Bara imetokea mara mbili, mara ya kwanza ilikuweko Mbagala na mara ya pili huko Gongo la Mboto.

Katika mripuko wa mwanzo ulipotokea serikali ilitoa taarifa kuwa watajitahidi kuona kuwa suala kama hili halitotokea tena, baada ya kipindi limetokea tena. Hivi sasa pia Mhe. Waziri anasema watajitahidi kama inavyowezekana kuona wanachukua hatua ya kuwa mambo haya yasitokee katika hali aliyoeleza.

a) Je, baada ya mripuko wa mwanzo serikali haikujua ni sababu gani ikawa hizo hatua walizochukua za kutoripuka tena hazikujulikana ndio kukatokea huo mripuko wa pili.

b) Mhe. Waziri anajua ni kitu gani hasa kilichosababisha miripuko hii miwili ili na sisi tuwe na hizo kinga ili kisitokee tena.

c) Kwa sababu Wazanzibari wengi wako wanaishi upande wa pili wa Muungano na hata katika matukio haya yaliyotokea, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukua hatua gani ya kuwajua na kuwafariji katika maafa yaliyowafika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, suala hilo hasa nilikuwa nilijibu kesho, lakini sasa Mhe. Salim ameshaliuliza kwenye swali la nyongeza. Kwa kuwa amewahi kuuliza kwenye swali la nyongeza, basi sina budi nilijibu leo, kwa hivyo, mwenye swali lake la kesho litakuwa limeshajibiwa leo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hatua mbali mbali zimechukuliwa katika kuhakikisha kwamba jambo hili lisiweze kutokea tena huko mbele. Ni kweli serikali ilitoa kauli huko nyuma kwamba jambo hili lisiweze kutokea tena. Lakini kama unavyojua majanga ni majanga, juu ya jitihada za serikali bado jambo hili limetokea. Kwa sasa kinachofanyika ni nini?

Kwa sasa kwanza kumeundwa Baraza la Uchunguzi chini ya kanuni ya Jeshi la Wananchi aya ya 13-07 kwa mujibu wa sheria nambari 9 ya mwaka 1996. kufanya uchunguzi ili kuweza kujua kiini cha tatizo lenyewe na kutafuta mbinu hasa za kukabiliana ili kuepukana na matatizo hayo siku za mbele.

Hata hivyo, wanausalama wa jeshi pia nao wanafanya uchunguzi wa namna hiyo hiyo kujua suala hilo, pamoja na nchi rafiki ambazo zimejitolea kushirikiana na jeshi letu katika kuhakikisha kwamba wanafanya uchunguzi na kusaidiana na jeshi letu ili kuhakikisha mambo kama haya hayawezi kutokea tena huko mbele. Lakini majanga ni majanga, juu ya jitihada hizo tumuombe Mwenyezi Mungu mambo kama haya Mhe. Naibu Spika, yasiweze kutokea.

Kwa upande wetu Zanzibar tunawasiliana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania Zanzibar na limetuhakikishia kwamba hali ya Zanzibar ni shuwari na salama.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mhe. Mtando alieleza kwamba, moja ya hatua za dharura zinazochukuliwa ni kuhamisha miripuko kutoka katika kambi zilizoko karibu na makazi ya watu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kambi zetu zote za hapa Zanzibar zipo karibu na makazi ya watu. Je, Mhe. Waziri miripuko hiyo ambayo ipo hapa Zanzibar imehifadhiwa katika kambi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali suala la ulinzi ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na linashughulikiwa na taasisi husika za JWTZ, mambo mengine ni siri za kiulinzi kwa hivyo, sitaweza kueleza zaidi ya hayo niliyoyaeleza.

Nam. 2

Eneo la Hoteli ya Bwawani Kujazwa Kifusi

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na wazo la kulijaza kifusi eneo liliopo mbele ya Hoteli ya Bwawani, ingawaje wazo hilo mara nyengine linapingana na ushauri wa umuhimu wa kutunza mazingira katika eneo hilo.

(a) Mhe. Waziri, kwa kuwa eneo hilo ni sehemu ya uso wa mji wa Zanzibar, serikali imefikia wapi katika mpango wa kulijaza kifusi.

(b) Kwa kuwa hivi sasa limeanza kujazwa kifusi je, serikali imefanya utafiti gani kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na umuhimu wa usalama wa kudumu wa eneo hilo.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa haraka wa kuandaa mazingira mazuri ya eneo hilo ili liendane na hadhi ya mji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2, naomba nifanye yafuatayo:-

Kwanza naomba nikubaliane naye kwamba kwa muda mrefu kweli kumekuwepo na wazo la kulijaza kifusi eneo liliopo mbele ya Hoteli ya Bwawani na kweli kwamba huwa linapingana na ushauri wa umuhimu wa kutunza mazingira katika eneo hilo.

Lakini pili naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Bwawani ni sehemu ambayo ina historia ndefu, kuanzia Makumbusho ndogo iliyopo Mnazi Mmoja hadi unapofika Bwawani, sehemu yote hiyo ilikuwa ni bahari. Eneo hilo likaimarishwa kwa kufukiwa (*reclaimation*), kazi ambayo iliendelea hadi baada ya vita vikuu vya mwanzo vya dunia mwaka 1918. Baada ya hapo kazi hiyo ilisita na eneo ambalo lilikuwa halijafukiwa ni eneo hili la Bwawani. Ujenzi wa gati ya Malindi uliofanywa miaka ya tisini ulihusisha uchimbaji mkubwa wa gati hiyo uliolenga kuongeza kina cha maji kwenye eneo la gati.

Uchimbaji huo ulipelekea kutolewa kwa mchanga mwingi sana. Mchanga uliotolewa kwenye hatua za awali za uchimbaji ulikuwa unatupwa karibu na visiwa vya Bawe. Kwa kuwa utupaji wa mchanga huo karibu na visiwa hivyo ulikuwa na athari mbaya kwa matumbawe yaliyoko karibu na maeneo hayo, Idara ya Mazingira ilishauri ni bora mchanga huo utupwe eneo la Bwawani. Hiyo ndio ikawa hatua ya mwanzo ya kulifukia Bwawa hilo. Hatua ya pili ya kulifukia Bwawa hilo ilikuja tena wakati wa matengenezo ya pili ya Bandari ya Malindi.

Mhe. Naibu Spika, ufukiaji wa Bwawa hilo kwa mara zote mbili ulifanywa kwa muongozo maalum kwa kuzingatia hali halisi ya Bwawa hilo. Tokea wakati huo Bwawa la Bwawani limekuwa na kazi kubwa za kimazingira zifuatazo:-

1. Kupokea maji machafu kupitia mitaro mitatu (3) ya maji machafu kutoka baadhi ya maeneo ya Mji Mkongwe, Mbuyuni na Mchangani. Maji hayo hupitia sehemu hiyo kabla ya kumwagwa baharini.

2. Kupokea kiwango kikubwa cha maji ya mvua kutoka maeneo ya Mlandege, Michenzani na Mchangani. Hivi sasa maeneo hayo yananusurika na kupata mafuriko kwa kuwa maji hayo yanapokelewa kwenye Bwawa la Bwawani.

Kutokana na sababu hizo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira mara zote imekuwa inaunga mkono hoja ya kufukia Bwawa la Bwawani, lakini ufukiaji huo ni lazima uzingatie mambo hayo mawili makubwa na pia uzingatie maumbile ya ardhi yenyewe (*hydrological-geology).* Kufanya hivyo kutaondoa athari mbaya za kijamii na kimazingira zinazoweza kujitokeza na ndio maana hata ufukiaji wa mwanzo uliofanywa umezingatia mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo hivi sasa kwa ruhusa yako tena naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa Bwawa la Bwawani limeshafukiwa kwa kiwango cha chini ya theluthi moja ya bwawa lote. Hata hivyo, kila inapotokea fursa serikali imekuwa ikichukua hatua za kuruhusu kufukiwa bwawa hilo. Naomba nieleza kuwa ufukiaji wa bwawa hilo ni gharama kubwa zinazohitaji nguvu ya uwekezaji. Nia ya serikali ipo pale pale ya kuliendeleza bwawa la Bwawani kwa faida za kimazingira, kiuchumi na kijamii.

(b) Mhe. Naibu Spika, mwaka 1994, serikali iliunda Kamati Maalum ya Wataalamu kushauri njia muwafaka za kuliendeleza eneo la Bwawa la Bwawani ikiwa ni pamoja na eneo hilo kufukiwa. Kamati hiyo ilitakiwa kuangalia kwa kina hali halisi ya eneo la bwawa hilo juu ya faida na athari za kimazingira, kijamii na kiuchumi ziliopo na kushauri ipasavyo juu ya namna bora ya kuliendeleza eneo hilo. Miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na kamati hiyo ni kufukiwa eneo lote hilo kwa utaratibu maalum.

Hata hivyo, kamati hiyo ilishauri kuwa ni vyema kuzingatia tathmini za athari za kimazingira kabla eneo hilo halijafukiwa moja kwa moja. Tathmini hiyo ni muhimu kuzingatiwa kabla ya hatua yoyote ile ya kulifukia eneo lote la bwawa la Bwawani haijachukuliwa. Hatua hiyo itasaidia kuweza kuepusha matokeo mabaya yanayoweza kutokea.

Hivi sasa serikali imo katika juhudi za kutafuta wawekezaji wa kuendeleza Hoteli ya Bwawani pamoja na bwawa lake. Naamini uwekezaji wowote ule wa kuliendeleza bwawa la Bwawani utazingatia matakwa ya hifadhi ya mazingira ya eneo hilo.

(c) Mhe. Naibu Spika, ili kulifanya eneo la Bwawa la Bwawani kuwa na mazingira mazuri baada ya kufukiwa, Kamati ya Wataalamu iliyoundwa mwaka 1994 ilitoa mapendekezo matatu ya kuzingatiwa ambayo ni:-

- Kuanzisha na kuendeleza bustani
- Kuanzisha na kuendeleza kituo cha maduka ya kisasa (*shopping centre*)
- Kujengwa maofisi ya kiserikali.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa mambo hayo unahitaji umakini na mtaji mkubwa. Hivyo, serikali inaendelea na hatua zake za kuhamasisha wawekezaji ili kusaidia kuendeleza eneo la Bwawa la Bwawani kuwa na hadhi stahiki kwa faida ya kiuchumi, mazingira na kijamii. Serikali itatoa kila msukumo unaostahiki kuhakikisha kuwa tathmini ya athari ya kimazingira (*EIA*) inafanywa mara mwekezaji wa eneo hilo atakapopatikana.

Mhe. Hijja Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

a) Mara zote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanapoishauri serikali kurekebisha mazingira ya Mji Mkongwe, serikali hujibu kwamba wanashindwa kurekebisha kwa sababu ya kuhofia vikwazo vya *UNESCO* na kwamba Mamlaka ya Mji Mkongwe itaathirika. Je, kwa ufukiaji huo wa bwawa hakuna masharti ya *UNESCO* juu ya Mamlaka ya Mji Mkongwe.

b) Kwa kuwa kamati ya wataalamu ilipendekeza kwamba bwawa la Bwawani lifukiwe na hatimaye lipandwe bustani. Sasa mtakubaliana na ushauri wa kitaalamu na kushauri Baraza la Manispaa kuweka bustani ya maegesho ya magari kule Bwawani badala ya pale Darajani Makontena.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, katika suala la kufukia na kuliendeleza eneo la Bwawani hakuna vikwazo vya masuala ya urithi wa Mji Mkongwe katika eneo hilo.

Lakini jibu lake la pili linalohusiana na ushauri wa kuliendeleza eneo hilo kwa kutengeneza bustani badala ya eneo la Darajani kwenye makontena, Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukau ushauri wake na tutawasiliana na wahusika wakiwa ni Baraza la Manispaa na pili wenyewe wenye Bwawa hilo ambao ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa ajili ya mashauriano hayo.

Mhe. Mabrouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza. kwa kuwa katika Hoteli ya Bwawani upande wa Kusini ya mlango wa kuingilia kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ya uchimbaji wa mchanga kiasi cha kwamba baada ya muda ile njia ya kuingia pale Bwawani itakuwa haipitiki. Kwa sababu imeshakuwa inamong'onyoka kwa uharibifu huo wa mazingira. Je, serikali itachukua hatua gani juu ya tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika eneo hilo kuna uharibifu mkubwa kwa uchimbaji wa mchanga ambao usio halalikama ilivyo katika maeneo mengine ya visiwa vyetu. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imejipanga na kujidhatiti katika kuhakikisha kwamba inasimamia sheria ili k uhakikisha utunzaji wa mazingira unakuwa katika kiwango cha juu ndani ya visiwa vyetu.

Nam. 19

Kukodishwa kwa Eneo la Shangani

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 46

Kamati za Baraza Kufanya Ukaguzi wa Thamani

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:-

Serikali katika kukabiliana na wimbi la ufisadi wa fedha na mali za umma, imeanzisha utaratibu wa ukaguzi wa thamani halisi ya matumizi (*Value for money Auditing*) kwa kipindi kirefu.

(a) Kwa kuwa Zanzibar bado haijaanza kuutekeleza mpango huo. Je, serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili iweze kutekeleza jukumu hilo kwa maslahi ya taifa.

(b) Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ndio chombo chenye mamlaka ya kusimamia utendaji wa serikali, ikiwa ni pamoja na kusimamia matumizi ya hesabu za serikali. Je. serikali imeandaa mpango gani wa kuliwezesha Baraza kupitia kamati zake, kuweza kutekeleza jukumu hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lakini kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, dhana ya Ukaguzi wa Thamani *(Value for Money Auditing)* ni ukaguzi unaozingatia ufanisi katika upatikanaji wa huduma, ununuzi wa bidhaa na matumizi yake ili kila bidhaa au huduma nyengine yoyote inayotolewa isigharimu zaidi ya kuliko inavyopaswa kuwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinatumika vyema na wananchi hawabebeshwi mzigo usiohusika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia bajeti yake hupatiwa fedha zote wanazoziomba kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo kwa lengo la kuimarisha Afisi hiyo kiutendaji, Serikali inaipa kipaumbele Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa lengo la kuimarisha Utawala Bora katika shughuli za kifedha na hatimae kuweza kupunguza na kuondoa kabisa kasoro katika matumizi mabaya ya fedha na mali za umma.

(b) Kwa vile Kamati ya Kuchunguza Mahesabu ya Serikali *(PAC)* kazi yake kubwa ni kufatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa ushauri kwa Serikali kwa kupitia Ripoti yake ambayo huwasilishwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, kwa maana hiyo ipo haja kubwa ya kuipatia taaluma kamati hiyo. Wizara yangu kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu itaendelea kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hiyo kama tulivyofanya hivi karibuni.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa suala la kukagua thamani *(Value for Money Auditing)* linahitaji wataalam na wataalam wanahitaji kuwa na malipo makubwa. Taarifa tulizonazo ni kwamba Serikali ilitoa ruhusa kwa Afisi ya

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iajiri wataalam lakini bahati mbaya siku ya usaili wataalam hawa hawakuonekana. Hii ilitokana na viwango vidogo vya malipo ya mishahara iliyoko katika afisi ile.

(a) Je, serikali iko tayari kuliongezea fungu afisi hii ili iweze kuajiri wataalam.

(b) Ili kuipa uwezo afisi ya *CAG* pamoja na kamati zetu ni muhimu pia kuweza kujiunga na Jumuiya za Kimataifa. Je, serikali itazisaidia vipi taasisi hizi kujiunga na Jumuiya za Kimataifa kwa lengo la kuzilipia ada.

(c) Kwa vile inasemekana kwamba taasisi kama hizi zilizoko katika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vikwazo kuziwezesha taasisi zetu kujiunga na Jumuiya za Kitaifa. Je, serikali itasaidia vipi kuondosha vigingi hivi ili na taasisi zetu hizi za Kamati za Baraza la Wawakilishi na afisi ya *CAG* ziweze kujiunga na Jumuiya za Kimataifa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ni kweli serikali kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea na itaendeleza utaratibu huu wa kufanya ukaguzi wa thamani kupitia wataalam wake. Katika hilo Mhe. Mwakilishi amesema kwamba tuliwahi kuwaita watu wenye ujuzi na kuweza kufanya usaili ili tuweze kuwaajiri na waweze kufanya kazi hizi.

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia wizara yangu katika kipindi kinachokuja cha bajeti cha mwaka 2011/2012 tutahakikisha kwamba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaongezewa fungu kwa ajili ya kuhakikisha wataalam wanapatiwa mishahara inayolingana na ujuzi wao. Mpango huo haupo kwa wataalam wa *CAG* tu peke yake lakini upo kwa serikali nzima.

Mhe. Naibu Spika, jibu (b) kwanza serikali inathamini sana mchango wa Jumuiya hizi za Kimataifa kwa mfano *AFROSAE* na *INTOSAE* na hivi sasa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ipo katika jumuiya hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikijibu swali langu la msingi nilisema serikali huipatia bajeti yake yote afisi hii. Kwa sababu kila siku kinachotumika katika matumizi ya serikali hupangwa kwenye bajeti, basi bado nilihakikishie Baraza la Wawakilishi kwamba serikali itaendelea na hilo ili afisi ya *CAG* kuweza kumudu kulipa ada kwenye jumuiya ambazo wamejiunga.

Mhe. Naibu Spika, jibu © mimi nadhani serikali haina vikwazo, ukishakubaliana na utaratibu wa kujiunga na taasisi husika na ukawa tayari umeshaanza kushiriki maana yake hujaweka vikwazo. Sisi tutahakikisha kwamba havitokei vikwazo kwa sababu afisi ya *CAG* kujiunga na jumuiya hizi na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya hizi kuna faida mbali mbali ambazo zinapatikana katika kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna wizara Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amezichunguza na amekuta kuna makosa na akashindwa kutoa ripoti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mtu ambaye anafanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mtu au taasisi yoyote. Kwa hiyo, mimi siamini kwamba Mdhibiti amegundua makosa katika utendaji wa kazi zake na akaweza kuyaficha. Kwani kufanya hivyo yeye angekuwa hajafikia kiwango cha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndio mwenye kuchunga mahesabu yote ya serikali. Je, mikataba inayotiwa katika mashirika na taasisi mbali mbali za serikali inapitiwa na nani. Ikiwa kuna taasisi zinafanya mikataba zaidi ya miwili kwa jambo hilo hilo moja ni hatua gani zinachukuliwa kurekebisha hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kikawaida ya mikataba yoyote ile ya serikali kwanza huandaliwa na taasisi husika lakini kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baada ya hapo taasisi husika hulazimika kusaini kwa mujibu wa masharti ya ule mkataba ulivyo. Lakini hakuna kizuizi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kufanyika kwa zoezi hilo kwenda kuhakikisha kwamba kilichofanywa ni sahihi au sio sahihi, ndio maana Mdhibiti hutakiwa kupitia matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, jibu (b) mazingira ya mkataba wowote ule unapofungwa inategemea una mahitaji gani. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile kama kwa mfano wizara yangu ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora haina jambo ambalo inahitaji kufunga mkataba, lakini Wizara ya Kilimo na Maliasili ina masuala hayo yanayofika saba itaendelea tu kujirejea rejea kwa sababu huo ndio utaratibu.

Mkataba unaohusu na kazi za Wizara ya Utumishi utafungwa na Wizara ya Utumishi, unaohusu Wizara ya Fedha utafungwa na Wizara ya Fedha. Lakini kuna ile mikataba ambayo inakuwa inabeba mzigo wa nchi hiyo itaendelea bado kuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha.

Nam. 130

Mfuko wa Vijana

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Wizara yako inashughulikia vijana na hivi karibuni umekabidhi Shs. Milioni Mia Moja na Arubaini na Tisa kwa ajili ya Mfuko wa Vijana.

Je, Mhe. Waziri unaonaje fedha hizo zikagaiwa Kiwilaya ili vijana wetu wengi zaidi kufaidika na mfuko huo katika wilaya zao.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 130 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Wizara yangu kupitia msaada wa Serikali ya Norway imetengewa Tsh. 149,000,000/= kwa ajili ya Mfuko wa Vijana wa Zanzibar ambao unaendeshwa na *UN Habitat.* Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ingekuwa vyema kila Wilaya kutoa vikundi vya vijana kufaidika na mfuko huo. Ili kikundi kiweze kupata fedha hizo kinahitajika kukamilisha yafuatayo:-

a) Kiwe kimesajiliwa,
b) Kiwe na akaunti ya akiba,
c) Kiwe na ripoti ya mwaka
d) Kiwe kimefanya shughuli zake si chini ya mwaka mmoja, na
e) Kiombe msaada huo kupitia mtandao maalum.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kwa kuelewa kwamba suala la kuwaendeleza vijana kiuchumi ni moja ya jukumu letu, tumeorodhesha vikundi vyote vya Unguja na Pemba kutoka kila Wilaya ambavyo vimekamilisha masharti haya na kwa vile kazi ya kujaza fomu hizo inahitaji utaalam mkubwa, Wizara imeweka utaratibu wa kuwasaidia vijana kujaza maombi hayo kupitia mtandao. Kazi hii imepangwa kukamilika baina ya mwisho wa mwezi wa Machi na wiki

ya kwanza ya Aprili; kabla ya siku ya mwisho ya maombi ambayo ni tarehe 15/4/2011.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu wasimamie vikundi vya vijana katika maeneo yao kwani fedha hizi zitakuwepo kwa kila mwaka na msaada huu ni endelevu.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vijana ndio mhimili mkubwa wa serikali na kila kijana anahitaji kuweza kufaidika na mfuko huo.

(a) Je, Mhe. Waziri ni msimamizi gani mkubwa kutoka katika wizara yako.

(b) Je, ni utaratibu gani utakaotumika na kujua kila kijana anaweza kufaidika na mfuko huo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwanza mhusika mkubwa wa usimamizi ni wizara yetu ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Sisi ndio wasimamizi wakuu na tutajitahidi kuona kwamba kila kijana anayeshughulika apate msaada huu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi sana fedha za wahisani zinapoletwa katika wizara yake Mhe. Waziri huwa zinaliwa. Je, Mhe. Waziri, wizara yako imejiandaa vipi kuweza kuzilinda fedha hizi kwa uhakika na zisiweze kuliwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi sielewi kwamba Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ina tabia ya kula fedha zinazofikia pale kwa ajili ya msaada. *(Makofi)*

Lakini la pili kwa sababu hizi fedha zitakuwa hazitolewi mikononi baina ya mtu na mtu zinapitia benki nadhani zitakuwa salama kwa anayepokea na huyo anayezileta hizi fedha.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar sasa hivi kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa kuwa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa inazingatia maslahi na maadili ya watu wetu wa Zanzibar

wote. Kwa kuwa baadhi ya sehemu kuna vikundi hujikusanya watu wakasema ni vikundi vya vijana wa umma ikawa ni kikundi cha watu binafsi wa kula fedha peke yao.

Je, katika hivyo vikundi vilivyokwishaletwa wamefanya utafiti gani wa kuhakikisha kama vikundi hivyo vina uwiano wa vyama vyote vya siasa vilivyomo katika nchi yetu kwa ajili ya vijana hao.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, katika mfuko huu kutakuwa hakuna mizengwe yoyote wala hakuna mababaisho yoyote, jambo kubwa ni kuwa umetimiza masharti yanayotakiwa yaani unayo akaunti benki, umesajiliwa unayo haki, kikundi chako ni endelevu na kama hukuwahi kuomba kwa mara hii mara nyengine unayo nafasi ya kuomba huu msaada na utasaidiwa na wizara ili uweze kupata huu mkopo.

Kwa hivyo, usiwe na wasi wasi wowote hakuna kwamba huyu nani, ni vikundi vya vijana vyote vitakavyoomba kupitia utaratibu unaotakiwa vitapata msaada huu.

Nam. 32

Viwanda vya Mafuta Kujengwa katika Makaazi ya Wananchi

Mhe. Salma Mohammed Ali – Aliuliza: **-**

Kwa kuwa Kiwanda cha Kusindika Mafuta ya Makonyo kilichopo Wawi Pemba kinatoa moshi mwingi katika kipindi cha uzalishaji na moshi huo huwaathiri wananchi waliozunguka eneo la kiwanda hicho kilichojengwa karibu na makaazi ya wananchi.

(a) Je, ni vigezo gani vya kitaalamu vilivyotumika na kupelekea Serikali kuamua kujenga kiwanda hicho katika makaazi ya wananchi.

(b) Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi kwamba moshi unaotoka katika kiwanda hicho hauna madhara kwa afya zao.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapima wananchi wanaoishi karibu na kiwanda hicho ili kugundua idadi ya wananchi walioathirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vifungu (a), (b) na (c) lakini kabla ya kujibu naomba kutoa utangulizi ufuatao:-

Mhe. Naibu Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa Kiwanda cha Kusindika Mafuta ya Makonyo kilichopo Wawi Pemba huwa kinatoa moshi mwingi wakati wa uzalishaji. Lakini nataka nitofautiane nae kwamba moshi huo huwa unawaathiri wananchi wanaolizunguka eneo la kiwanda kwani kuna wafanyakazi wanaofanya kazi kiwandani hapo na hatujapata hata kesi moja ya kuthibitishwa hospitali kuwa wameathiriwa na moshi huo.

Mhe. Naibu Spika, wakati kiwanda kinajengwa mwaka 1982 palikuwa na wananchi kidogo sana wanaoishi katika eneo hilo, lakini kadri muda ulivyokwenda wananchi walianza kujenga karibu na maeneo ya kiwanda hicho.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, vigezo vilivyotumika kujenga kiwanda katika eneo hilo la Wawi ni kama ifuatavyo:-

1. Eneo hilo kuwa kati kati ya Kisiwa cha Pemba hivyo ilikuwa ni kuwarahisishia wananchi wa Kaskazini na Kusini kufikisha makonyo yao kiwandani hapo.

2. Kwa wakati ule eneo lile lilikuwa ni sehemu pekee ambayo ina vianzio vya umeme na maji ya kutosha kwa mahitaji ya kiwanda.

(b) Kwa kuhakikisha usalama wa afya ya wananchi Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

1. Imefunga *(boiler)* lenye kifaa kinachoitwa *(cyclone)* chenye uwezo wa kuondosha mavumbi na taka zote katika moshi huo unaotoka wakati wa uzalishaji.

2. Kiwanda sasa kinatumia makapi ya makonyo yaliyokamuliwa mafuta na sio kuni, *diesel* au aina nyengine ya nishati ambayo inaharibu mazingira. Aidha, moshi unaotoka pamoja na kuwa ni mzito lakini hauna madhara yoyote kwa wananchi. Uzito wa moshi huo unatokana na uchomaji wa makapi ya makonyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa vile moshi huo hauna madhara hivyo Serikali haijachukua hatua ya kuwapima afya wananchi wanaoishi maeneo hayo kuhusiana na moshi huo. Hata hivyo Mhe. Niabu Spika, uwezo wa kiwanda hicho kwa sasa kwa kufanya kazi ni siku 20 tu kwa mwaka ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kiwanda hicho kilikuwa kinafanya kazi kwa siku 200 kwa mwaka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amejibu kwamba hakuna madhara yoyote yanayopatikana kutokana na moshi unaotolewa na kiwanda kile.

(a) Je, anaweza akatuletea uthibitisho wa daktari uliioonesha kwamba moshi ule hauna madhara.

(b) Kwa kuwa Jimbo la Wawi lina sehemu kubwa ambazo ziko wazi. Kwa kuwa kile kiwanda kipo kati kati ya barabara na Jimbo la Wawi. Je, serikali itafikiria vipi kukiondosha kiwanda kile kukipeleka katika maeneo kama ya Makaani ambako yako wazi na hakuna shughuli kubwa za binadamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, hakuna uthibitisho wa daktari hasa tukizingatia kwamba hakuna mwananchi aliyekwenda hospitali kwa kulalamikia kudhuriwa na moshi.

Mhe. Naibu Spika, hii inathibitika kwa mbunge katika jimbo lako ambaye alikuwa miongoni mwa wafanyakazi wa mwanzo kabisa tokea kiwanda hicho kuanzishwa. Amekuwa katika kiwanda kile siku nyingi na afya yake ni nzuri hatimaye ameweza kugombea ubunge na ameshinda katika Jimbo la Mfenesini.

Mhe. Naibu Spika, jibu (b) ni kwamba serikali haina mpango wa kukihamisha kiwanda hicho kukipeleka sehemu nyengine.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, haoni Mhe. Naibu Waziri kwamba ipo haja sasa akaweza kufanya kwa makusudi kuwapima afya wale watu waliokizunguka kile kiwanda na akaweza kujiridhisha na hayo matamshi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, katika jibu la msingi nimesema kwamba hakuna uthibitisho wa daktari na hii naendelea kusema kwa sababu wafanyakazi wa kiwanda hichi wamekuwa wakienda hospitali na wanakaa katika kiwanda hicho masaa mengi na moshi

huo unaonekana haujawadhuru. Hasa ikizingatiwa kwamba tayari hatua za kudhibiti taka zinazotokana na moshi huo zimeshachukuliwa na serikali.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba kiwanda hichi kilipojengwa palikuwa na wakaazi wachache sana katika eneo hilo. Kwa kuwa sasa hivi kumekuwa na tabia ya wananchi kusogelea maeneo ambayo yamejengwa viwanda au makambi ya kijeshi na hatimaye huwa inatokea athari pale panapokuwa na mambo kama haya. Je, serikali inatoa wito gani kwa wananchi juu ya jambo kama hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, tatizo hili la wananchi kuhamia katika maeneo ya viwanda na pia maeneo ya jeshi limekuwa ni tatizo sugu. Kwa hiyo, tunakuombeni Waheshimiwa Wawakilishi kwa kuwa nyinyi pamoja na mimi tuko karibu zaidi na hawa wananchi basi tuwaelimishe kwamba kuhamia karibu na maeneo kama hayo ni hatari kwa afya zao, lakini pia ni hatari kwa jamii yote kwa jumla. Kwa hivyo, tunawaomba tushirikiane katika hili ili kuondoa tatizo hilo Mhe. Naibu Spika.

Nam. 36

Kuimarisha Upatikanaji wa Chakula

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Hali ya uzalishaji wa chakula Zanzibar bado sio nzuri sana, ingawa juhudi za kukabiliana na tatizo hilo zimeanza kuchukuliwa miaka mingi iliyopita. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kuimarisha mashamba ya umwagiliaji ili yaweze kuongeza mavuno ya chakula hususan mpunga.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazokwamisha kurejesha ukulima wa kitaalamu wa umwagiliaji katika baadhi ya mabonde hapa Zanzibar, kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula.

(b) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuona suala hilo linatekelezeka.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru yeye na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kutambua kwamba kilimo cha umwagiliaji maji ndio ufumbuzi wa kuzidisha mavuno ya mazao ya chakula hapa Zanzibar, hasa zao letu la mpunga.

Mhe. Naibu Spika, mabonde ya umwagiliaji maji yote ya Unguja, hivi sasa yanaendelea kuzalishwa kwa kutumia utaalamu, ndio kusema kwamba yale yote yaliyokuwa hayalimwi sasa yamesharejeshwa katika utaratibu wa ukulima huo, (kama vile bonde la kibokwa, cheju na Bumbwisudi). Mabonde haya yamerejshwa kwa mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na uhisani wa KOICA kwa bumbwisudi na Kibokwa, TASAF **na** PADEP kwa bonde la Cheju.

Mhe. Naibu Spika, kwa mabonde yaliyoko Pemba nayo baadhi yamerejeshewa katika uzalishaji wa umwagiliaji maji. Mabonde hayo ni kama Kinyakuzi na Saninga kwa mchango wa Serikali pamoja na JP- 5 na PADEP.

Mhe. Spika, wizara katika mikakati yake ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kwa kipindi cha muda mrefu, ni utekelezaji wa mpango wake mkuu wa umwagiliaji maji, na kulijengea miundo mbinu eneo lote lililo ainishwa kwenye mpango huo, ambalo lina hekta sawa na (8,521) kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mkakati wa muda mfupi, napenda kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba katika kipindi cha miaka mitano (2011-2015) katika kutekeleza mpango mkuu wa umwagiliaji maji, wizara imejipanga kufanya yafuatayo:-

Kwa kushirikiana na Benki ya Exim ya Korea Kusini tunategemea kuanzisha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Chaani, Kibokwa, Kakwararani na Mlemele kwa upande wa Pemba, ambapo mradi huu ukimalizika utaweza kutayarisha eneo la kuzalisha mpunga lenye ukubwa wa hekta 2,100 sawa na ekari 5,250 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya umuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa kilimo cha kumwagilia maji sio kwa mpunga tu, bali kuna vilimo vingine ambavyo vinahitaji navyo kumwagiliwa maji.

Kwa mfano, nyanya, vitunguu, mbatata na vilimo vingine. Kwa kuwa katika ardhi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kuna maeneo vilimo hivyo vinastawi kwa nguvu kubwa. Je, ni lini wizara yake itasimamia kwa dhati na

kuliona suala hili lina mkazo na kuweza kulitilia mkazo zaidi ili wananchi wa visiwa vyetu wafaidike na vilimo hivyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana kwa swali lake, kwa sababu ni la msingi na linaendana na sera ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, iliyoainishwe kwenye sera ya uhakika wa chakula ya mwaka 2008 na hata kwenye mswada huu ambao tunaendelea kuupitia hapa. Lengo kuu la serikali ni kuwawezesha wakulima wake, kuwajengea uwezo ili kilimo kiwe kivutio kwao na kiwe chenye tija kwa wakulima wa nchi yetu.

Kwanza tuweze kujihakikishia usalama na uhakika wa chakula cha ndani. Pili, wakulima wetu waweze kuuza mazao hayo na matimaye kuweza kujipatia tija. Ni sahihi kabisa Mhe. Naibu Spika, kwamba kilimo cha mboga mboga kwa zaidi ya asilimia 80, tunategemea mboga mboga kutoka Tanzania Bara. Hata sekta yetu ya utalii tumeshindwa kukidhi mahitaji yake.

Mhe. Naibu Spika, ipo mikakati ambayo imeshaanza kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia miradi ya PADEP, na mradi wa huduma ya kilimo ambayo imeanzisha mashamba darasa 360. Hivi sasa tumo kwenye mpango wa kuongeza mashamba darasa 360 mengine na wakulima wameanza kupewa taaluma ya ukulima wa mboga mboga. Kwa bahati mbaya wanaendelea kutumia vianzio vya maji vilivyokuwa karibu na wao. Kwa hivyo, miongo inapokuwa haiongoki, jua linapokuwa kali, kwa kweli wanashindwa kuzalisha na kwa misngi hiyo tunashindwa kuwa na uendelevu katika uzalishaji wa mboga mboga. Lakini serikali itaendelea kuchukua jitihada na ninaamini katika bajeti ya mwaka ujao serikali itaonesha hasa kwa dhati katika kutenga fedha nyingi kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, ili tuanze kuwapa taaluma wakulima wetu wa umwagiliaji wa kudumu. Kwa mfano *drip irrigation* hatua baada ya hatua.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Pamoja na maelezo yake mazuri. Mhe. Waziri umeyataja mabonde ya Kibopwa na mabonde mengine. Lakini je, utakubaliana na mimi kuwa mabonde hayo hivi sasa hayana maji ya kuweza kumwagilia mpunga.

Je, Mhe. Waziri una mikakati gani katika wizara yako ili kuweza kuhakikisha maji katika mabonde hayo uliyoyataja.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa swali lake, kwa maana yeye anatokana na jimbo la wakulima na nimpongeze kwa kuwa karibu sana na wakulima na kuwatetea maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwishakueleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba katika mpango wetu wa umwagiliaji tumefanya utafiti wa kina, na hata huu ambao tunategemea uwekezaji kupata msaada kutoka Serikali ya Korea ya Kusini ambao umelenga kuwekeza dolla za Kimarekani 53,000,000 utafiti wa kina umefanywa juu ya hali halisi ya upatikanaji wa maji ardhini na ndio maana hatimaye mpango huo mkuu umepitishwa na ili uweze kutekelezwa. Kwa hivyo, tafiti zimefanywa na tunaamini kwamba maji yapo ya kuweza kuyatumia kwa ajili ya umwagiliaji na pia kwa uendelevu.

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ikiwa tutaendelea kukata miti ovyo, tutaendelea kuvamia maeneo ya vianzio vya maji, basi nchi yetu itakuwa katika hatari kubwa sana ya kukosa maji, sio kwa ajili ya kilimo tu, bali hata kwa matumizi yetu ya kila siku. *(Makofi).*

Nam. 91

Idadi Kubwa ya Wanafunzi Waliofeli Kuendelea na Masomo

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2010 yameonesha asilimia 90% wamepata daraja la nne na wengine kufeli kabisa (*Zero*), kwa maana hawana uwezo wa kuendelea na masomo ya kidato cha tano (*Advanced Level*).

Je, kuna sababu zipi zilizopelekea kupatikana kwa idadi kubwa ya waliofeli.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 lakini kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2010 yameonesha kuwa asilimia ya kufaulu kwa wanafunzi kwa daraja la kwanza hadi la nne Kitaifa Tanzania yameshuka, kwani ni asilimia 50.4 ya watahiniwa wote ndio waliofaulu. Hata hivyo kwa Zanzibar asilimia ya kufaulu kwa wanafunzi ni asilimia 72.1 ambacho ni kiwango cha juu kuliko Mikoa yote ya Tanzania.

Mkoa wa pili kwa asilimia ya kufaulu kwa wanafunzi ni Mkoa wa Mwanza ambapo ni asilimia 59.90 tu ya watahiniwa walifaulu mitihani yao na kufuatiwa na Mkoa wa Iringa ambapo asilimia 58.64 ya watahiniwa walifaulu. Kwa

matokeo hayo ni wazi kuwa matokeo ya wanafunzi wa Zanzibar ni mazuri kiasi ukilinganisha na matokeo ya Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, kwa kulinganisha matokeo kwa wanafunzi wa Zanzibar kwa madaraja mbali mbali ni kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wanafunzi 85 wamefaulu katika daraja la kwanza (ukilinganisha na 40 mwaka 2009) sawa na asilimia 0.5 ya watahiniwa wote;

(b) Wanafunzi 173 wamefaulu katika daraja la pili (ukilinganisha na wanafunzi 166 mwaka 2009) sawa na asilimia 1.04 ya watahiniwa wote;

(c) Wanafunzi 1,330 wamefaulu katika daraja la tatu (ukilinganisha na wanafunzi 1,202 mwaka 2009) sawa na asilimia 7.99 ya watahiniwa wote;

(d) Wanafunzi 10,395 wamefaulu katika daraja la nne (ukilinganisha na wanafunzi 5,658 mwaka 2009) sawa na asilimia 62.5 ya watahiniwa wote;

(e) Wanafunzi 4,646 wameshindwa kabisa na kukosa vyeti (ukilinganisha na wanafunzi 1,659 mwaka 2009) sawa na asilimia 27.9 ya watahiniwa wote;

Mhe. Naibu Spika, kwa matokeo haya idadi ya wanafunzi wa Zanzibar waliofaulu katika daraja la nne ni asilimia 62.5 na sio asilimia 90 kama mheshimiwa alivyosema. Kwa matokeo hayo, jumla ya wanafunzi 1,868 kutoka skuli za serikali, wamefaulu na wana sifa za kuendelea na masomo ya kidato cha tano na kujiunga na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume. Idadi hiyo ni kubwa ukilinganisha na wanafunzi 1,202 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume mwaka 2009. Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa matokeo ya wanafunzi wetu sio mabaya sana kama wengine wanavyodhania.

Mhe. Naibu Spika, kushindwa kwa baadhi ya wanafunzi wetu kufanya vizuri kunatokana na sababu mbali mbali, zikiwemo uhaba wa vifaa vya maabara katika skuli zetu, uhaba wa walimu wenye uwezo wa kutosha, msongamano wa wanafunzi katika madarasa na ushirikiano mdogo kati ya walimu na wazazi katika baadhi ya skuli. Wizara inachukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha matatizo hayo yanatatuliwa ili wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza, baada ya majibu ambayo yalipotoshwa kidogo katika jibu la Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema katika swali langu kwamba kuanzia daraja la nne na daraja *zero* ni asilimia 90. Daraja la nne Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa ya Baraza jusi alikuwa akitoa mtaalumu kwamba hata polisi hutakiwi tena kwenda kupeleka cheti cha daraja la nne sasa hivi na hawezi mtu aliyepata daraja la nne kisha akajiunga na *form five.* Kwa hivyo swali langu lilikuwa hivi, kuanzia daraja la nne na daraja la ziro ni asilimia 90.

Lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa asilimia 90 kama nilivyosema wako daraja la nne na ziro na kwa kuwa hao waliokwenda wakapata daraja ya kwanza na ya pili wanatoka skuli nne tu za Unguja na Pemba. Zaidi ni Fidel Castro, Kiuyu, Lumumba na Bembela. Je, hatuoni kama kuna tatizo la mfumo wa elimu katika kuwapata vijana wetu waweze kufaulu na ni lini serikali itayaachia matokeo ya *form two* yapelekwe maskulini badala ya kutangaza kwamba amefaulu na hali ya kuwa hakufaulu katika redio, ahsanate.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, bado tunasema waliopata daraja la nne ni kweli hawana uwezo wa kuingia pale, lakini wana fursa wa kujiendeleza sehemu nyengine na wakaweza kufanya vizuri. Ninasisitiza kusema kwamba matokeo ambayo yametoka sio mabaya sana na niseme iwapo tutashindwa kushukuru kidogo sidhani kama tutaweza kushukuru kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, hapa la kufanya ni kushirikiana kwa pamoja kati ya wizara na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nimeshuhudia wawakilishi wengi wakiwasaidia wanafunzi wao ambao wamefeli *form two,* kwa kushirikiana na wizara kuwaundia madarasa wakaweza kuendelea. Pia nimeshuhudia Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu Mhe. Naibu Spika, wakiwasaidia wanafunzi wao ambao wamepata daraja la nne na kuweza kuendelea na masomo yao katika njia nyengine ambayo inawaruhusu kuendelea, nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

(a) Matokeo ya mitihani ya kidato cha nne mwaka jana yameonesha kwamba Unguja ni mshindi wa mwanzo kitaifa na Pemba ni

mshindi wa sita kwa Tanzania. Naomba kujua ni nini siri ya mafanikio haya.

(b) Mara zote mitihani inapofanywa wanafunzi wa Zanzibar baadhi yao hulalamika kwamba matokeo yao sio sahihi na wanapokata rufaa huonekana kwamba kweli wamepasi vizuri na kuweza kuendelea kidato cha tano. Je, ni sababu gani baadhi ya wanafunzi hutokezea matokeo yao wakaambiwa ni ziro, lakini wakifuatilia kwenye rufaa huwa ni daraja la kwanza au la pili. Je, wizara imegundua vipi.

(c) Serikali hii ya Zanzibar chini ya Umoja wa Kitaifa inahimiza wanafunzi wa Zanzibar wa kike na wakiume kusoma masomo ya Sayansi, hatua hiyo imechukuliwa sana na wanafunzi wa Skuli ya Jimbo langu la Mtangani na walimu wao kwa kutoa mwanafunzi bora Tanzania kwa somo la Chemistry na skuli ya pili Tanzania kwa somo hili. Je, wizara yako itatoa motisha gani kwa skuli hiyo na mwanafunzi huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, swali nambari (c) sijalifahamu vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, swali (c) ni kwamba Serikali inahimiza wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, ili kupunguza tatizo la wana sayansi hapa Zanzibar, Skuli yangu ya Mtangani imetoa mwanafunzo bora kwa somo la *Chemistry* na skuli ya pili kwa somo hiyo Tanzania. Je, wizara yako itatoa motisha gani kwa skuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, siri ya mafanikio ya skuli za Unguja kupata nafasi ya nne Tanzania na skuli za Pemba kupata nafasi ya sita kwa Tanzania ni mashirikiano, mashirikiano kati ya wazazi na walimu. Hii ndio maana Mhe. Naibu Spika, nasisitiza wazazi kutoa mashirikiano kwa walimu, tunapotoa mashirikiano wazazi kwa walimu basi bila shaka matokeo yatakuwa ni mazuri.

Mhe. Naibu Spika, hawezi mwanafunzi kwa kusoma *tuition* peke yake akaweza kufaulu bila ya mzazi yeye mwenyewe kufanya jitihada ya makusudi kuhakikisha kuwa mtoto huyu anaporudi nyumbani kweli anasoma masomo yake.

Mhe. Naibu Spika, matokeo kutokuwa sahihi. Suala hili ni kweli, kwa sababu yanajitokeza masuala haya lakini yanapojitokeza kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali basi tunapopata habari kwamba kuna wananfunzi ambao

wanaonekana daraja lao ni la pili halafu wamepelekwa daraja la tatu au la nne, basi tunashirikiana ili kuhakikisha kwamba yanakaa sawa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili linaweza kutokea pahala popote, sio kwamba Baraza la Mitihani linafanya makusudi ili wanafunzi wetu wa Zanzibar wafeli.

Mhe. Naibu Spika, suala la huyo mwanafunzi wetu kufanya vizuri katika somo la sayansi huko Skuli ya Mtangani, wizara ina maandalizi kabambe sio kwa mwanafunzi huyo tu, lakini kwa wanafunzi wote ambao wamefanya vizuri na kwa skuli zote ambazo zimefanya vizuri, basi tutawazawadia zawani maalum. Ahsanate sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba kwa kuwa katika maelezo yake alisema kutokana na msongamano wa wanafunzi na upungufu wa walimu ndio unaosababisha vijana wetu wengi kutokupasi vizuri.

Je, Mhe. Naibu Spika, ni lini tatizo hili litapatiwa ufumbuzi na hasa kuwaajiri walimu wengi ili kuondosha usumbufu na kuweza kupasisha wanafunzi wengi, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni kweli nilisema katika jibu langu mama kwamba sababu kuu ambazo zinafanya baadhi ya watoto wetu kutokufanya vizuri ni uhaba wa vifaa vya maabara, msongamano wa wanafunzi na pia kukosa walimu wenye sifa.

Mhe. Naibu Spika, niseme kuwa matatizo haya hivi sasa wizara tumeyakalia na tunajaribu kuyatatua. Kwa upande wa vifaa vya maabara, tayari tumepata vifaa kwa awamu ya kwanza na vifaa hivyo tumeshavigawa kwa Unguja na Pemba. Pia tumetoa tenda nyengine kwa vifaa vya maabara. Kwa upande wa tatizo la walimu, kwa tatizo hili tayari tuna mradi wa kuhakikisha kwamba walimu wetu tunawaongezea uwezo wao.

Mhe. Naibu Spika, suala la msongamano wa watoto. Wizara yetu kwa kuliona hilo, hivi sasa tuna mradi maalum ambao unafadhiliwa na benki ya dunia. Tunajenga skuli za kisasa kabisa. Naomba niwatajie Waheshimiwa Wajumbe kwa faida ya Baraza kuwa ni skuli gani ambazo tunajenga.

Mhe. Naibu Spika, Skuli ya Utaani tunaiongezea, Skuli ya Konde, Pandani, Tumbe, Kiwani Mauwani, Chambani na Wawi na kwa Skuli za Unguja ni Uzini, Dimani, Chaani, Matemwe, Paje Mtule, Tunguu, Uzini na Muwanda.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, tuna mradi mkubwa wa matengenezo wa Skuli zetu za Unguja na Pemba kama vile skuli ya Utaani ile kongwe, Fidel Castro na Forodhani. Zote hizo ni katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanapata nafasi nzuri ya kusoma na kuondokana na msongamano ambao tunao hivi sasa nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nitowe taarifa kidogo, kwa kuwa maswali yetu yamebakia matatu na tunazo dakika tano, namuomba Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais alete utaratibu ili tuweze kuyamaliza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza maswali yaliyokuwemo kwenye orodha wa shughuli za leo, naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu, wakubali tutenguwe muda wa kanuni ili tuweze kuendelea na kipindi cha maswali ili tuweze kumaliza maswali yaliyokuwa mbele yetu, ahsante.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nam. 71

Kuchelewa Kesi za Ardhi

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Jengo la Mahakama ya Ardhi liliyopo Wete tayari limeshakamilisha ujenzi wake, lakini kesi za ardhi zimerundikana.

(a) Je, Jengo hilo litafunguliwa na kuanza kazi lini.

(b) Kwa sababu Mahkama ya Ardhi ina upungufu wa Mahakimu Wizara ina mpango gani wa kuongeza Mahakimu ili kuondoa usumbufu wa kesi kurundikana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa jengo liko tayari na pesa za fanicha ziko tayari ila kwa sasa hatukuweza kuingiza fanicha hizo kwa vile

Mahakimu bado hawajateuliwa, kinachosubiriwa kwa sasa ni uteuzi wa Mahakimu wapya ambapo mara tu utakapofanyika uteuzi huo jengo liliopo huko Pemba litafunguliwa rasmi na kuanza kazi .

a) Mhe. Naibu Spika, kutokana na mazungumzo yaliyofanyika baina ya wanasheria wa ardhi na Mheshimiwa Mrajis wa Mahakama Kuu, imeelezwa kuwa kwa sasa ni vigumu kwa Tume ya Mahakama kuteuwa Mahakimu wapya wa Mahakama ya Ardhi kutokana na sababu hizi zifuatazo:-

- Tume ya uajiri ya Mahakama ndiyo ya kuteua Mahakimu ambayo hadi sasa ina upungufu wa wajumbe wawili ambao wamemaliza muda wao wa kazi.

- Mbali na hilo wajumbe hao wanapaswa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa sasa bado hawajateuliwa.

Nam. 78

Wanafunzi wa Chuo cha Habari Kutosoma Somo la Kompyuta

Mhe. Hija Hassan Hija – Alijibu:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuanzisha Chuo cha Uandishi wa Habari, nchini katika zama hizi za utandawazi, sayansi na teknolojia. Hatua hii sio tu kwamba itaongeza nafasi za ajira kwa vijana wetu, lakini pia itapandisha hadhi ya Zanzibar ndani ya Tanzania, Afrika ya Mashariki na duniani kwa ujumla.

(a) Je, Chuo chetu cha Uandishi wa Habari Zanzibar, kina walimu na wanafunzi wangapi.

(b) Je, kuna ukweli gani kwamba, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanaochukua somo la Kompyuta ya Habari (*Computer Journalism*) bado hawajasoma somo hilo mpaka muda huu, ikiwa imebaki muda mfupi kumaliza muhula wa kwanza (1st *Semester*).

(c) Kuna sababu zipi zilizopelekea kutosoma somo hilo, wakati liliorodheshwa katika masomo ya muhula huo wa masomo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar kina jumla ya walimu kumi na nne (14) , kati yao wanane (8) ni wa muda na sita (6) ni wa kudumu.

Kwa upande wa wanafunzi, Chuo hivi sasa kina jumla ya wanafunzi mia moja ishirini na mbili (122) kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (*Diploma*). Kati ya hayo wanafunzi wa Cheti ni 43 na waliobakia ni *Diploma*.

b) Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu swali lake kifungu cha (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Chuo chetu hakina wanafunzi wanaochukua somo linaloitwa Kompyuta ya Habari. Ila kinafundisha somo linaloitwa "*Computer Assisted Journalism*". Haya ni mafunzo ya *program* maalum yaliyoingizwa katika Mtaala wa Chuo, ili kuwasaidia waandishi katika kazi zao za kila siku.

Miongoni mwa yanayofundishwa katika program hiyo ni namna ya kutumia mtandao wa Habari "*Internet*", utayarishaji wa magazeti (*Adobe Quicker, Adobe Publisher and Page Making* pamoja na
E Design).

Aidha wanafundisha *program* za kufanyia uhariri kwa vipindi vya Radio kama vile "*Adobe Edition New eddo and TV Pen cal*."

Program hizo zote zintakiwa zifundishwe katika "*Semester*" moja (1) tu miongoni mwa *Semester* nne (4) kwa wanafunzi wa *Diploma* ama "*Semester*" moja (1) miongoni mwa mbili (2) kwa wanafunzi wa Cheti.

c) Ni kweli katika Ratiba ya Vipindi vya masomo kwenye "*Semester*" ya kwanza liliwekwa somo la "*Computer Assisted Journalism*". Lakini kutokana na upatikanaji wa fedha, chuo hakikuweza kufundisha *Programs* hizo kwenye "*Semester*" ya kwanza na badala yake mafunzo hayo yataanza katika "*Semester* " ya pili.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi, kwamba matayarisho yamekamilika ikiwa ni pamoja na kuingiza *programs* hizo katika kompyuta za Chuo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kutonisahau kunipa nafasi hii. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba walimu waliopo ni kumi na nne (14) na wanane (8) kati yao wamekwenda pale kwa *part time*. Kuna athari gani ambazo walimu hawa wanasababisha juu ya matokeo na masomo ya wanafunzi hawa.

(b) Amesema kwamba sababu za kutosomeshwa wanafunzi hao somo la *Computer Assisted Journalism* ni pamoja na fedha. Lakini zipo taarifa kwamba wanafunzi hao wameshindwa kusomeshwa kwa sababu *computer* zao zimeingia virusi. Kwa hivyo, wizara nzima haina uwezo wa kutatua tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mjumbe arejee tena swali lake la kwanza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba walimu wanane (8) wanaingia kwa *part time*. Kuna athari gani ambazo wanafunzi hao wanazipata kutokana na utaratibu huo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, umeshalifahamu swali.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, bado.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, rejea tena.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba Mhe. Waziri amekiri kuwa walimu ni kumi na nne (14) wa Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma Zanzibar, walimu nane (8) kati yao wanaingia kwa mikataba, yaani *part time teachers*. Kwa hivyo, kuna athari gani wanafunzi wetu wanazipata kimasomo kwa utaratibu huo wa kuajiri walimu nane *part time* kati ya kumi na nne (14).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri umeshafahamu, yaani athari gani inayopatikana kwa walimu wanane (8) wanaosomesha kwa part time kati ya walimu kumi na nne (14) ambapo ni nusu ya walimu hao wameajiriwa. Sasa

kutokana na mwenendo huo kuna athari gani ambayo inapatikana kwa wanafunzi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hakuna athari yoyote ambayo inayopatikana na huo ni utaratibu wa vyuo vingi walimu wote sio *fulltime*. Kwa mfano, siku hizi kuna kuwa na *Visiting Lectures* huwa wanatoka sehemu mbali mbali, wanakuja na kusomesha baadaye kuondoka. Kwa hivyo, hakuna athari yoyote Mhe. Mjumbe.

Kuhusu suala la *computers* kuingia virusi. Si kweli kwamba *computers* ziliingia virusi, isipokuwa hii *program* ya Kichina ambapo inakwenda sambamba na Somo la Kichina na wataalamu walitakiwa waje mapema, ili waje na vifaa. Lakini hivi sasa tayari wameshafika pamoja na vifaa na *program* hii tayari itaanza rasmi.

Nam. 38

Kuimarisha Huduma za Afya

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Kampeni zake aliahidi kuimarisha huduma za afya hapa Zanzibar.

(a) Je, wizara yako ina mkakati gani katika kutekeleza ahadi hiyo.

(b) Kwa kuwa Mhe. Rais aliahidi kuimarishwa Hospitali za Wilaya na Mikoa, na kwa kuwa Wilaya ya Kati wagonjwa wengi wanapata taabu kufuata huduma za afya, wakati mwengine akinamama (wazazi) huzalia njiani wanapofuata huduma hiyo. Je, ni lini Wilaya ya Kati itapata Hospitali yake ya Wilaya, ambayo itakuwa na uwezo wa kutoa huduma za uzazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye vifungu (a) na(b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, wakati wa Kampeni za Uchaguzi aliahidi kuimarishwa kwa huduma za afya, hasa kinga na tiba na zaidi alisisitiza kuimarisha huduma hizo kwenye Rufaa Hospitali ya Mnazimmoja.

(a) kwa kutekeleza ahadi hiyo kwa kuanzia wizara imetayarisha mpango wa muda mrefu wa miaka mitano uliozingatia maeneo muhimu kama ifuatavyo.

(i) Rasilimali watu,

(ii) Mafunzo ya Madaktari Bingwa na Wakawaida,

(iii) Mafunzo ya Kujiendeleza kwa kada mbali mbali na

(iv) Mpango mzima wa Ajira za Dharura kwa Madaktari Bingwa kwa Hospitali ya Chakechake na Mnazimmoja.

Katika eneo la pili upandishaji Daraja kwa Vituo vya Afya kwa ajili ya kutoa huduma za ziada zikiwemo kuzalisha, maabara, ugawaji wa dawa kwa wagonjwa pamoja na huduma za meno. Pia vituo 34 tayari vimeshachaguliwa pamoja na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi karibu na vituo hivyo unaendelea.

Hospitali ya Micheweni, Vitongoji, Makunduchi na Kivunge zimo katika mpango huo ulioandaliwa, ili ziwe Hospitali za Wilaya.

Aidha Hospitali ya Chakechake imo katika kuandaliwa kupandishwa Daraja na kuwa Hospitali ya Mkoa.

Sambamba na hayo, mpango unajumuisha kujenga Hospitali katika Wilaya ya Magharibi yenye hadhi ya Wilaya.

Eneo la tatu ununuzi wa madawa muhimu, vifaa na zana za uchunguzi wa maradhi. Pamoja na mpango hatua za kuimarisha Hospitali ya Mnazimmoja tayari wafadhili wa kusaidia kutoa huduma za matibabu kutoka *Falkland University* nchini Norway wameshajitokeza. Vile vile tunategemea kuwasili kwa *Neurosurgeon* Dr. Young kutoka Marekani.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia wizara yangu imevipandisha Daraja Vituo vitatu vya Wilaya ya Kati, Chwaka, Unguja Ukuu na Uzini, ambavyo vitatoa huduma za ziada ikiwa ni pamoja na kuzalisha. Ujenzi wa Nyumba za Madaktari kwa vituo viwili vya Chwaka na Uzini. Kituo cha Chwaka kimeshindwa kutoa huduma za kuzalisha kutokana na ukosefu mkubwa wa maji. Hata hivyo, wizara yangu imo mbioni kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwa ujumla washirikiane na Kamati zetu za Afya za Wilaya (*DHMT*) katika kutatua tatizo hili, ili huduma zianze kutolewa mara moja.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ambayo ameyatoa, swali langu ni kwamba kutimiza ahadi ambazo Mhe. Rais amezungumza katika Kampeni ni suala moja. Lakini suala la kusomesha au kuwapatia taaluma zaidi madaktari ni jambo la pili.

Kwa hivyo, swali langu hilo hapa pamoja na juhudi zote ambazo zinafanywa wizara yako Mhe. Naibu Waziri imejipanga vipi katika utaratibu wa madaktari, ambao wanapangwa baada ya masaa ya kawaida ya kufanyakazi na wanapokwenda kufuatwa katika maeneo husika hawapo na wakati mwengine inatokezea ajali na madaktari wanatafutwa kwenye nyumba zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli zipo taratibu katika hospitali zetu za madaktari kuingia kwa zamu na wale ambao wanaoingia kwa dharura pale ambapo kuna haja ya kufanya hivyo. Kwa mfano, madaktari wanaingia kwa zamu asubuhi, mchana na usiku, lakini wa dharura wanahitaji mazingira maalum, ili waweze kuwepo hospitali. Kwanza kuwepo na nafasi ya kuwalaza, pili *allowance* za kuwalipa.

Kwa kweli nafasi ya kuwalaza katika Hospitali ya Mnazimmoja hatuna, kwa hiyo utaratibu uliopo ni kwamba gari inawafuata pale wanapohitajika na huwa wanaacha namba zao za simu na ipo ratiba ambayo inayofuatwa. Kwa hivyo, daktari anakaa nyumbani dharura inapotokea anajuilishwa anayehusika na kumfuata na kuja hospitali kwa ajili ya kutoa huduma. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kweli nakubaliana naye kwamba kuna baadhi ya Vituo vya Wilaya Kati vimepandishwa Daraja kama vile Uzini, Chwaka na Unguja Ukuu.

(a) Lakini kupandishwa Daraja kwa vituo hivyo, bado kukitokea tatizo la dharura inabidi wananchi wa Wilaya ya Kati wafuate huduma hiyo mjini na pengine kutokezea matatizo katikati.

(b) Vile vile niliuliza kwamba ni lini wizara yako itaipatia Wilaya ya Kati Hospitali ya Wilaya, ili kuwapunguzia masafa marefu kufuiatia huduma za dharura wananchi wa Wilaya ya Kati.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ili huduma za afya ziweze kutolewa, basi tunahitaji wafanyakazi wa kutosha katika vituo vyetu na hilo la kwanza. Pili tunaangalia mtandao wetu jinsi gani ulivyo katika wilaya tofauti. Kwa mfano, Wilaya ya Kati ni wilaya ambayo inayo vituo vingi na katika suala hilo tumeangalia tukiweza kutoa huduma zipi zitawasaidia watu wa kiasi gani.

Kwa hivyo, kwa vyovyote vile itakavyokuwa itakavyokuwa hata kama kuna Hospitali ya Wilaya itafika wakati mtu yule anahitaji kuja Hospitali ya Mnazimmoja. Vile vile watu kutoka Kaskazini, Kusini Unguja wanakuja, pia kutoka Vitongoji wanakuja Hospitali ya Mnazimmoja.

Kutokana na hali hiyo, zile huduma za msingi zikitolewa katika sehemu hizo tatu, yaani Chwaka, Unguja Ukuu na Uzini kwa mpangilio ambao tumeuona kwamba huu utafaa, basi kwa zile huduma ambazo mzazi au mjongwa mwengine yoyote akizipata zinaweza kutosheleza kutokana na ufinyu wetu wa wafanyakazi.

Kwa hivyo, tunataka tuhakikishe kwamba hivyo vituo vitatu vinakuwa na wafanyakazi wa kutosha. Baadaye tutakapopata wafanyakazi wa kutosha zaidi na tukiona ipo haja ya lazima ya kuongeza vituo au kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Kati basi itajengwa. Lakini kwa hivi sasa tunachokiona Wilaya ya Magharibi ndio inayohitaji mwanzo, kwa hiyo tutaanza na Magharibi na baadaye tutatizama mahitaji ya Wilaya ya Kati. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Wakati alipokuwa akijibu swali la Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kuhusu madaktari. Hivi kweli ndio utaratibu wa hospitali daktari kufuatwa kwake au kuna taratibu zipi za kuhakikisha hospitali madaktari wanakuwepo wakati wote, ili linapotokezea tatizo lolote isiwe tena huku mtu yuko katika hali ya kutaka kufa na daktari anatafutwa nyumbani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, hospitali tunazo taratibu zifuatazo. Tunao madaktari ambao wanakuwepo masaa yote, pia na madaktari ambao wanakuwepo zamu. Kwa mfano, madaktari wanaokuwepo masaa yote hospitali kuanzia asubuhi, mchana pamoja na usiku. Vile vile kuna madaktari ambao wanaokaa nyumba, kuna daktari wa kwanza, pili na wa tatu.

Kwa kweli mara nyingi suala la mgonjwa anayekuja usiku likiwa limeshindikana na daktari wa kwanza ndipo anapofuatwa daktari wa ngazi ya pili na tatu na hao ndio wanaokuwepo majumbani, kwa sababu daktari wa kwanza anakuwepo pale na yeye akiona hili limemshinda basi daktari wa pili

anaingia kati na yeye akiona daktari wa pili ameingia ndipo daktari anapoitwa. Kwa hivyo, daktari wa pili na wa tatu hao ndio wanaolala majumbani, lakini madaktari wa kwanza siku zote wapo mahospitalini. (*Makofi)*

Nam. 23

Serikali Kutafuta Meli Nyengine kwa Wasafiri wa Zanzibar

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Alijuliza:-

Maingiliano yaliyopo kati ya Visiwa hivi viwili, vya Unguja na Pemba yanalazimisha mzunguko mkubwa wa watu kati ya visiwa hivi na usafiri unaotegemewa na wengi ni wa baharini. Hata hivyo, hivi sasa hali ya usafiri wa vyombo hivyo vya bahari vinavyotegemewa na wananchi walio wengi, imekuwa ni tete hususan baada ya kuonekana meli zinazosafiri katika visiwa hivi haziko katika hali ya ubora.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuondoa tatizo hilo.

(b) Ni lini serikali italeta meli nyengine ambazo zitachukua nafasi ya M.V Maendeleo na M.V Mapinduzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba tokea mwaka 1984 serikali iliporuhusu wawekezaji binafsi kuekeza katika Sekta ya Usafiri wa Baharini kumekuwa na maendeleo makubwa katika sekta hiyo.

Katika kufanikisha azma hiyo serikali imewashajihisha wafanyabiashara kuongeza meli nyingi hasa zile zinazokwenda Pemba na Unguja. Kwa mfano, hivi sasa kumekuwa na safari za kila siku baina ya Unguja na Pemba na hivyo kupunguza kabisa tatizo la usafiri baina ya visiwa hivi.

Aidha serikali itaendelea kuwashajihisha zaidi wawekezaji, ili waweze kuongeza meli zitakazofanya safari baina ya Unguja na Pemba kwa wingi zaidi. Kwa upande wa serikali Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iataendelea na juhudi zake za kuimarisha meli zilizopo na kununua nyengine mpya, ili kuondosha kabisa tatizo la usafiri wa visiwa hivi kama ilivyo kwa usafiri wa Dar-es-Salaam na Zanzibar.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeanza kufanikisha mpango wa kupatikana meli mpya, ambapo hivi sasa hatua za mazungumzo yenye mwelekeo wa kufanya ubia na kampuni nyengine za nje ya nchi yanaendelea. Katika kutimiza azma hiyo, serikali imeandaa mradi, yaani *project writeup*, ambayo imefanyiwa *feasibility study* na kuanza kuuzwa kwa washirika wa maendeleo.

Hadi hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tayari kampuni mbili kutoka Dubai zimeshaonesha nia ya kutaka kuja kuwekeza kwa mfumo wa *PPP*. Imani yetu ni kwamba pindi wawekezaji hao watakapofika nchini na kuanza kufanya utaratibu wa uwekezaji, basi suala la upatikanaji wa meli mpya litakuwa limepatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nimelazimika kuhaka hapa na kuhamia kule, kwa sababu hapa hunioni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwa kuwa Shirika la Meli ni wazoefu sana wa kuendesha usafiri hasa kati ya Unguja na Pemba limefanya kazi hiyo kwa muda mrefu na mafanikio makubwa.

Pamoja na serikali kuzishajihisha taasisi binafsi kuwekeza katika masuala ya usafiri lakini inaonekana kwamba bado matatizo yapo, kwa sababu ukipanda boti ya *Sea Express* huwezi kuchukua hata kifurushi cha kilo hamsini.

Vile vile Shirika la Meli kutokana na uzoefu wake, hivi karibuni lilikuwa limeandaa mpango wa kuleta meli ya kisasa inayokwenda kwa kasi na yenye uwezo wa kuchukua abiria na mizigo kwa wingi na wakuu wa serikali mpango huo wameusitisha. Je, Mhe. Waziri anaweza kutwambia kwa sababu gani serikali ilisitisha mpango huo wa Shirika la Meli.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba kweli serikali imesitisha mpango wa Shirika la Meli kutaka kuleta meli mpya kwa mkopo kwa sababu zifuatazo:

Kwanza Mhe. Naibu Spika, Shirika la Meli halimiliki meli yoyote meli zote ni mali ya serikali na hii inatokana na sheria iliyoanzisha shirika hili na hadi sasa hivi sheria hiyo haijabadilishwa. Kwa hivyo, mnunuzi ama kwa fedha taslim au kwa mkopo ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ni kweli kabisa katika juhudi za kutafuta ufumbuzi Shirika la Meli, lilifanya juhudi kubwa hadi kufikia maafikiano ya kupata mkopo wa dola milioni 25 kununua meli kwa ajili ya abiria na mizigo.

Lakini kama nilivyoeleza kwamba wanunuzi wa meli au wakopaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kuangalia masharti ya mkopo na maslahi yenyewe wakaona mpango huu wausitishe na mpango huu wa dola milioni 25 ilikuwa ni meli itakayoweza kubeba tani hamsini na abiria 1,200.

Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanataka kuondoa tatizo hili la kudumu kwa mpango maalum wa uwekezaji wa watu binafsi na serikali. Kwa hivyo, serikali imeagiza baada ya kusitisha mkopo huu ikaiagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kufanya mambo yafuatayo na tayari yamefika katika hatua kubwa.

Kwanza kutayarisha mradi ambao serikali na wawekezaji binafsi kama ambavyo amesema Naibu Waziri *Public Private Partnership (PPP)* wawekeze pamoja na hili litaweza kuondoa kabisa tatizo hili. Mradi huo tayari umeshatayarishwa na tayari umeanza kuuzwa na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wangu *response* ya tuliowauzia ni nzuri sana. Kwa hivyo, hivi sasa tunasubiri baada ya kuwaalika ili tuweke mazungumzo nao mmoja baada ya mmoja, yule ambae serikali itaona ina maslahi nae zaidi basi twende na huyo na mpango huu ni vizuri wajumbe wako waelewe ni mpango ambao una awamu tatu.

Awamu ya kwanza Mhe. Naibu Spika, ni kuleta meli mbili za abiria zenye mwendo wa kasi, meli moja wanaita *roll on roll off* abiria na mizigo wanafika pahali wanateremka na magari hiyo moja.

Lakini vile vile Meli ya *roll on roll off* kwa ajili ya bandari za Afrika ya Mashariki zote ikiwemo na Msumbiji.

Lakini vile vile kuna na meli ya makontena mia moja na hamsini hii ni kuanzia *phase* ya kwanza ambayo gharama yake ni dola za Kimarekani 32. Awamu ya pili ni kuongeza tena kontena *vessel* meli inayochukua makontena 250 lakini vile vile na kuongeza meli ya mafuta ambayo *phase* ya kwanza ni milioni 32 na *phase* ya pili ni milioni 42.

Mhe. Naibu Spika, lakini *phase* ya tatu sasa hii itaongeza meli moja ya mafuta gharama dola 250. Kwa hivyo, *phase* ya kwanza, *phase* ya pili na ya tatu itakuwa imegharimu mradi huu wa serikali pamoja na wawekezaji binafsi

jumla ya milioni arubaini na nne na nusu hii serikali wameikubali na ndio tunayoifanyia kazi nayo.

Mhe. Naibu Spika, nina hakika baada ya mradi huu kumalizika Shirika la Meli litakuwa limehuika kwa sababu hakutokuwa na mfanyakazi ambae atafukuzwa ni baina ya serikali na wawekezaji na sio kuhuika tu, lakini tutakuwa na mapato makubwa kwa mujibu wa *study* ambayo tumefanya.

Kwa hivyo suala la shirika la meli kwamba limekufa hawaleti mapato halitahadisiwa tena humu katika Baraza lako, lakini zaidi ni manufaa ambayo serikali itapata katika kuongeza uchumi wake na ukiongezeka uchumi maana yake ni kwamba serikali inakuwa na nguvu zaidi ya kuleta na kufanya au kutekeleza ahadi zote ambazo wamezifanya.

Mhe. Spika, kwa hivyo mradi wa dola milioni 25 ni kweli uliletwa lakini serikali baada ya kuangalia kwa kina wakasema hapana tusitishe. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Shirika la Meli lilikuwa limeshafanya huo mpango tayari lakini Waziri hapa katupa mipango mingi sana ingawa mipango sio matumizi.

Mimi nataka kujua ni lini mipango hiyo itakuwa imeshakamilika?.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, mipango si matumizi nakubaliana nae, lakini kwa serikali makini na yoyote na hata mtu wa kawaida tu bila ya kupanga huwezi kufanya lolote utaingia kichwa kichwa na mamilioni yako utapata hasara, kwa hivyo suala la serikali kupanga ni la lazima.

Lini mpango huu utakamilika, nimesema juhudi zimeanza zinaendelea tunawasubiri ni baraza hili hili tutatoa taarifa rasmi maendeleo ya mradi huu ambao serikali wameukubali, hapo watakapoarifiwa kwamba umekamilika au tunakwenda vipi ndipo tutakapojua mpango huu utakamilika lini. Lakini nasema serikali mipango yake ni ya kawaida inaendelea na itaendelea kupanga na sio Wizara hii tu lakini serikali nzima na tuna waziri kabisa maalum anayeshughulikia mipango ya maendeleo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza suala moja dogo sana la nyongeza. Kwanza niishukuru serikali na niipongeze serikali kwa kuwa na mipango mizuri ya baadae, ishaalla tumuombe Mwenyezi Mungu aitie roho.

Sasa naomba niulize kwamba Shirika la Bandari karibuni lilifanya matengenezo ya meli ya MV. Jitihada kwa shilingi 2.6 bilioni pesa ambazo zinatosha kununua meli mpya. Je, Mhe. Naibu Spika, kwa nini Serikali imeliruhusu shirika suala kama hilo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, hili swali ni zuri lakini kwa muono wangu sio pahali pake, lile ni Shirika la Meli liliofanya matengenezo ni Shirika la Bandari. Lakini hata hivyo naomba nimjibu kuwa sio Shirika la Meli lililotengeneza Meli ya Jitihada ni Shirika la Bandari, meli ya jitihada ni meli ya serikali na hapo awali ilikuwa chini ya Wizara ya Kilimo, lakini baada ya meli ile kuwa hali ambayo serikali wameona kwamba haiuziki na ina umuhimu wake ina historia ndefu wakaona kwa nini tusitafute shirika meli hii ikatengenezwa.

Kwa hivyo ukafanywa utafiti na ikagundulikana kwamba meli hii inatengenezeka, kwa hivyo Wizara ya Kilimo kwa sababu hawana uwezo wa kutosha wa kutengeneza serikali ikakubali kwamba basi wapewe Shirika la Bandari, kwa hivyo Shirika la Bandari wakachukua meli ile na ndipo walipoanza kuitengeneza. Ni kweli kwamba metengenezo ya meli ile ni gharama kubwa ni zaidi ya bilioni mbili kama alivyosema, ni kweli meli ile sasa hivi hata ukiiuza haiwezi kufika bilioni mbili, lakini kwa sababu ni ya zamani lakini ungeweza kuiita mpya, ni meli ambayo Shirika la Bandari wanaangalia uwezekano ama kuikodisha kwa mtu binafsi au kuiendesha wenyewe, au kutafuta njia kiasi ambacho meli ile italeta maslahi kwa uchumi wa Zanzibar na hapo ndipo tulipofikia.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba wajumbe wako wafahamu kwamba meli ya MV. Jitihada sasa hivi imetengenezwa karibu ya upya na karibuni sana tutamualika Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenda kuifungua rasmi na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari inatafakari ni vipi meli hii waitumie ili iwe na maslahi na kama kuna mtu yoyote anataka kuinunua kwa bei zaidi ya tuliyotengenezea anakaribishwa, lakini tumeamua tusiikodishe kwa sasa kutokana na sababu zetu za msingi ambazo baadhi ya wajumbe wako wanafahamu, tutachukua muda mrefu kulipa gharama ya matengenezo kama tutaikodisha.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe tuna masaa mawili yamebakia hivi sasa ni saa tano na tunawachangiaji sita, kwa hivyo naomba nishauri kwamba hii saa moja tutumie kwa uchangiaji wa wajumbe sita kila mtu dakika kumi, aliyekuwa haziwezi atamkopesha mwenziwe ikifika saa sita namuita Waziri ili aweze kujibu na kuweza kufanya majumuisho.

Mhe. Hassam Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nami kupata fursa hii ya kuweza kuchangia katika Mswada wa Uhakika wa Chakula na Lishe Bora, mswada huu umekuja pahali ndipo kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ya kisiwa na nchi yenye amani na utulivu wa kutosha hasa katika maridhiano ya vyama vyetu viwili tumekuwa watulivu wa kutosha.

Lakini kwa kuzingatia hapa tulipo ni mahali pazuri wananchi wetu kufarajika kwa uhakika wa chakula na lishe bora, Wazanzibari wote wa Unguja na Pemba wana matumaini na serikali yao iliyochaguliwa tarehe 31/10/2011 sasa hivi wana matumaini makubwa na serikali ya Zanzibar ambayo ina matumaini mazuri ya mshikamano wa kutosha katika mambo ya chakula. Lakini ukiangalia mfumko wa bei za kula umezidi siku hadi siku unapanda na wananchi wanakata tamaa lakini wana imani na umoja wa serikali ya umoja wa kitaifa kama makali ya maisha yatapungua kwa ukali wa vyakula hivi.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa sukari kilo moja shilingi elfu mbili na sisi tunataka tupate uhakika wa chakula na lishe bora, lakini ukiangalia ukurasa wa 103 kifungu cha 4 ufafanuzi kama kilivyovyoeleza. Kuna Ofisa hapa maana yake ni Afisa mwenye sifa za kitaalam na ujuzi na maarifa yatakayomuwezesha kutoa maamuzi na mapendekezo ya kitaalam na masuala yanayohusiana na uhakika wa chakula na lishe kulingana na majukumu ya Wizara yake. Kifungu hiki mimi nakipongeza sana sina wasi wasi nacho.

Lakini tu pamoja na elimu yake au sifa za *Certificate* msomi huyo pia awe na sifa ya kuwa na mlahaka mzuri kwa watu wote awe mtumishi wa watu badala ya watu kumhudumikia yeye, ajenge mazingira mazuri na uhuwishaji wa chakula mijini na vijijini hususan wazalishaji kwa vijijini ambao wanahitaji semina, mafunzo, uwezo na uwezeshaji na kupewa pembejeo za kilimo uvuvi na ufugaji na sio kujifungia ofisini akisubiri watu wamnyenyekee.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni zuri sana kama kilifungu kilivyoelsa lakini utakuta uzalishaji huu wa ndani unataka ufanisi mkubwa sana, kwa sababu kumekuwa na wimbi la wachungaji kuharibu vipando vya wakulima ambavyo ni tegemeo letu, jambo ambalo linamkatisha tamaa mvuja jasho anayejituma kwa nguvu zao na hatimae vipando vile havithaminiwi na wachungaji au wafugaji.

Mhe. Naibu Spika, kwasababu jaduweli ya kwanza imeonyesha Wizara tofauti kule kuweza kukidhi ili jambo hili la uhakika wa lishe na chakula liweze lifanikiwe, tunawaomba Idara zote zilizotajwa humu zisimamie kikamilifu ili tuweze kufikia malengo hayo tuliyoyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango wangu mfupi na kujali muda wako naomba niishie hapo, kwa mujibu wa Jimbo la Kojani naunga mkono mswada huu mia juu ya mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kutoa shukurani zangu za zati kwako nami kunipatia nafasi ya kuchangia mswada huu, namshukuru Mhe. waziri husika kwa uleta barazani kwa wale wa chakuka kwani mswada huu umekuja katika wakati muafaka. Mimi ningependa kuchangia kwa jumla katika mambo yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, uagizaji wa bidhaa ni utulivu katika nchi nyingi duniani kote inategemewa na upatikanaji wa chakula cha kutosha kinyume chake huwa ni vurugu kwa upande wan chi, kwa mfano nchi yetu ile asilimia tisini ya chakula chetu inaagizwa nchi za nje, hii inaonyesha kwamba uzalishaji wa chakula nchini umepungua sana.

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu haina budi kufanya jitihada za makusudi kupitia mswada huu kuweza kuzalisha chakula cha kutosha ili kupunguza uagizaji wa chakula, hususan kwa bidhaa kama mchele, unga, sukari na kwa vile ndizo zinazotumika kwa wingi hapa nchini. Bado tuna mabonde mengi ambayo tukiyatumia vizuri yanaweza kutupa tija katika kuzalisha mpunga na miwa, wakulima wetu wengi wamekata tama na kilimo na kuona hawapati faida nah ii imesababishwa na kutokupata pembejeo za kutosha ikiwemo mbolea, mbegu bora na madawa.

Mhe. Naibu Spika, katika wizara zote za serikali Wizara ya Kilimo na Maliasili ina wataalam wengi na wazuri lakini cha kushangaza sijui wataalam hao hawawezeshwi, au kwa makusudi wamekuwa hawaithamini taaluma yao kwa wakulima na huku wizara ikiwatizama bila ya kuwachukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa mashirikiano ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Bashara, Viwanda na Masoko ndiko kunakopelekea chakula kukosekana, nasema hivi kwa sababu nchi hii haina viwanda jambo ambalo linawapa tabu wakulima mahali pa kuuzia bidhaa zao. Nchi nzina ina kiwanda kimoja cha sukari kiwanda ambacho muwekezaji aliyepewa kashindwa hata kuzalisha robo rika ya watu wa Unguja kwa mwezi, hivyo ipo haja ya serikali kujipangia juu ya viwanda ili mpunga unapozalishwa wakulima wajue wanaupeleka wapi katika kupata soko sambamba na matunda.

Mhe. Naibu Spika, katika sulala la umwagiliaji maji serikali lazima itambue kuwa kilimo chenye tija duniani kote ni kilimo cha umwagiliaji, hivyo wizara haina budi kujipanga katika sekta hii kwa kuchimba visima vya kisasa kwa kuwapa kazi watu wenye uwezo isiwe kwa visima vilivyochimbwa kwa gharama ya milioni 42 kwa kila kimoja na hatimae havitoi maji, huku ni kupoteza pesa za serikali bure.

Mhe. Naibu Spika, wizara iwe na wakati wa kuyalinda mabonde na isiwachukue watu kujenga, pamoja na wizara kujitahdi kuwawekea mpango malengo ya kulima ekari thalathuini kwa mwaka , hata hivyo malengo hayo ni madogo ikilinganishwa na eneo lililopo Zanzibar kwa kilimo.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa niseme suala la muhali hatuna budi tuliondoe ili werikali ionekane iko mamkini kwa yale mambo ya maendeleo katika kutafuta, hatua zichukuliwe kwa mfano kampuni inayotengeneza barabara ya Amani/Dunga wanabeba maji ya mto Mwera kwa wastani wa lita elfu sita kwa siku katika kazi zake, maji hayo hayalipwi kampuni ilipaswa ichukue maji katika eneo maalum ambalo Mamlaka inalitambua ili mapato yaingie serikalini. Tatizo hilo limepelekea maji kupungua na kupelekea usumbufu kwa wakulima wa Mtwango na Mwera ambao kilimo chao kinategemea mto huo.

Mhe. Naibu Spika, niseme ni imani yangu mswada huu utakaopitishwa na kuanza kutumika utajijengea matumaini yaliyo hai ya zana ya uhakika wa chakula ya kuongeza uzalishaji sambamba na kuongeza uwezo wa wananchi wa chini kumudu kujinunulia chakula hicho.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kwahani naunga mkono hoja.

Mhe. Hija HAassan Hija: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kutoa mchango wangu kwa ufupi juu ya mswada huu wa Mhe. Waziri wa Kilimo kwa ajili ya kusaidia Maendeleo ya mswada wenyewe. Mhe. Spika,

kwa sababu umenipa dakika kumi naomba nitoe mchango wangu kwa jumla juu ya baraza katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu unakusudia kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa chakula na lishe kwa wananchi wa Zanzibar, katika mswada huu umezingatia mpango wa chakula ambao tunaambiwa ndio hasa uliozingatiwa katika mswada huu. Mimi naweza kusema kwamba Wizara ya Kilimo imekuwa na wataalam wengi lakini kadiri wanavyozungumza suala la kilimo na hasa katika umwagiliaji wa maji wanazungumzia suala la kilimo cha mabondeni, lakini ni mara chache mno wataalam wa wizara hii kuzungumzia kilimo cha maweni. Ukiangalia Mhe. Spika, ni kwamba Mashariki ya Visiwa vya Zanzibar ni maeneo yawe na ndiko kwenye wakulima wanyonge, lakini wataalam wa wizara hii sijawaona kuangalia umuhimu wa kuwapatia utaalam wamwagiliaji maji katika maeneo haya ya juu ambayo yanazalisha matunda na viungo vingi sana.

Mhe. Naibu Spika, nadhani mswada huu ungeliangalia zaidi huku kuliko kwenye mabonde ya kumwagilia maji katika mabonde ya mpunga ambayo nahisi ni machache mno kwa Unguja na Pemba, sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri labda angeangalia kipengele ambacho kingewapa nguvu wataalam wetu kuelekeza nguvu katika kilimo cha maeneo ya juu mwa maeneo ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu pia umetoa majukumu katika wizara tofauti na umeunda kamati tendaji kubwa sana kwa maana ya makatibu wakuu, zaidi ya watendaji kumi na nane watakuwa kamati tendaji. Mhe. Naibu Spika, sio tatizo lakini nadhani isijekuwa Mswada huu unakusudia kutengeneza maslahi ya watendaji tu watendaji wamekuwa wengi, wasi wasi wangu ni kwamba mswada umeandaa watendaji wengi kwa hivyo unaandaa mazingira ya maslahi kwa watendaji na ile dhana ya kilimo bora na lishe itakua haipo.

Nasema hivyo kwa sababu hivi sasa mswada huu umesema kwamba utasimamia mazingira, lakini serikali yenyewe wakati mwengine ndio inayoharibu mazingira yetu ya Unguja na Pemba niseme kwamba Mhe. Hamza Hassan juzi alizungumza hapa kwamba maeneo ya Mwambe yameathirika kimazingira, ni kweli asilimia kubwa sana ya Mwambe imeathirika kimazingira lakini serikali inapokaa inazungumzia uharibifu ule ni kwamba kwamba wananchi ndio wanaoharibu peke yao, mimi kama ni Muwakilishi wa Jimbo la Kiwani nakiri kwamba wananchi wa Mwambe wanachangia kuharibu mazingira lakini kwa asilimia ndogo sana sio zaidi ya thalathini. Serikali yenyewe kupitia Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu imechangia kwa asilimia kubwa kuharibu maziringa ya watu wa Mwambe ambayo ni maeneo ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, karibuni hivi tulikuwa na ziara ya Makamo wa Kwanza wa Rais baadae tukafuatiliwa na Rais mwenyewe wa Zanzibar na hata Mhe. Waziri wa Kilimo mwenyewe amefika katika maeneo ya Mwambe, tumeharibiwa sana. Lakini hakuna kauli ya serikali inayosema kwamba mazingira yale yalindwe kwa ajili ya kilimo cha juu, Mwambe sisi hatuna mabonde ya mpunga ni maeneo yam awe ambayo tunajipatia vitu vyetu katika kilimo chetu cha juu, lakini serikali imechimba pale katika eneo la Mbogoja imeona pale hapatoshi sasa imeelekea sehemu nyengine kuharibu mazingira juu ya ujenzi wa barabara zake za Pemba.

Ninapozungumza hoja hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wanasema Mhe. Hija hana shukurani, shukurani haiendi penye uharibifu Mhe. Naibu Spika, lazima serikali izingatie jinsi mazingira ya watu wa Kiwani yanavyoharibiwa kwa maslahi ambayo watu wa Mwambe wanayaona ni madogo sana, kama kweli wanataka kupatikana mazingira mazuri ya kupatikana chakula na lishe naomba serikali izingatie sana juu ya umuhimu wa kulinda mazingira, hasa katika jimbo langu upande wa sheria ya Mwambe. Vyenginevyo mswada huu watu wa Kiwani hautowasaidia kiasi hicho.

Jengine ambalo ningesema haraka haraka ni sula zima la upatikanaji wa nyama kwa ajili ya *protean,* wataalam wanasema kwamba nyama ya samaki inaongeza sana lishe za wanaadam, lakini hadi leo tumeshindwa kujenga machinjio katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba kwa ajili ya wananchi wetu kuwapatia nyama halali na nzuri. Sasa tukiangalia kwa mswada huu ni hatua gani ambayo itawapatia wananchi wetu huduma ya kupatikana kwa nyama hadi hivi leo soko la machinjio ya Kisakasaka halijamalizika matengenezo yake, seuze yale machinjio ya Wilaya zetu na Mikoa yetu Unguja na Pemba. Kuona kiasi gani Wazanzibari wanapata huduma hii ya nyama kwa ajili ya kuongeza *protean* ambazo zinakusudiwa katika mswada huu.

Lakini sambamba na hilo nadhani sasa serikali ingeelekeza nguvu kule Makurunge kwenye shamba kubwa ambalo tumeliweka kwa muda mrefu bila ya kulimwa na kuweka mifugo, shamba tumeliwacha hivi hivi watu wanajenga majumba ya makaazi. Kama kweli serikali inakusudia kuimarisha huduma ya kilimo na lishe basi nadhani ni muda muwafaka sasa kuelekea Makurunge kwa ajili ya kilimo na mifugo hivi sasa kwa ajili ya kupata Wazanzibari huduma hii ya chakula na lishe kwa ajili ya ustawi wan chi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitalisema haraka haraka ni suala zima la ugawaji wambegu mimi nimekuwa nikishangaa kwamba pale ambapo panatokezea ukame kwa Unguja na Pemba, serikali hujitolea na kutoa misaada ya mbegu lakini inashangaza sana kuona mbegu ambazo wanapewa wakulima wetu

pengine ni vikombe viwili vya mbegu za mhindi, au vikombe viwili vya mtama sijui ni kwa kiasi gani mbegu hizi zitawafikia na kuongeza uwezo wa wakulima wetu. Mimi namuomba Mhe. Waziri namuamini sasa utaratibu huo wa kuwapatia mbegu wakulima wetu vikombe viwili vya mbegu ya muhindi nadhani uondoshwe haufai na kama tutaendelea na utaratibu huu basi tutakuwa hatujaondoa tatizo la kufanya kuwa na lishe kwa wananchi wetu walio wanyonge, ni utaratibu mbovu ambao hauwasaidii wakulima wetu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kusema kwamba suala la kuwa na ghala la akiba ni muhimu na namuomba Mhe. Waziri katika hili lazima kuwe na umakini mkubwa, tusije tukaandaa maficho ya panya wala mali, mana kuna maficho ya panya wala nguo na wala mali, tusije tukaandaa mahala kwa ajili ya kuwanufaisha watu wachache, kwa hivyo maghala haya yawanufaishe Wazanzibari pale inapotokezea dharura. Mimi nimuombe Mhe. Waziri aongeze umakini wake na asimamie sheria hii katika masuala ya maghala ili wachache wajanja wasije wakanufaika kwa ajili ya kula mali za wanyonge.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi naunga mkono mswada huu namuomba Mhe. Waziri kwamba awe makini ili ufanisi na haki ipatikane kwa Wazanzibari wote. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Radhu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, kwa sababu ya ufinyu wa muda na kwa kuwa nilikuwa na vifungu vingi nilikuwa nataka nipatiwe ufafanuzi na kuvitolea maoni, naomba niseme kwa ufupi ufupi tu lakini naamini utanimegea muda kidogo.

Mhe. Naibu Spika: Nakupa dakika ishirini.

Mhe. Ismail Jussa Radhu: Ahsante. Hasa kwa kuwa mswada huu umeletwa na rafiki yangu mpenzi Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kwanza nianze kwa kumpongeza kwa hatua hii ya kuleta mswada huu ambao umekuja kwa wakati wake kabisa, kama walivyosema wenzangu dunia nzima hivi sasa inakabiliwa na matatizo makubwa, unapofungua redio, TV na vyombo vyengine vya habari vinazugumzia janga lililoikumba dunia na upungufu wa chakula. Wataalam wetu juzi walitupa maelezo ya kutosha katika semina lakini pia nilibahatika jumamosi tulikuwa na mkutano wa chama chetu na mwenyekiti wangu *Professar* Lipumba akiwa mchumi alilieleza vizuri sana hili juu ya hali ilivyo katika dunia, kiasi gani imepelekea kupanda kwa bei ya mchele, sukari, unga na mafuta ambayo ndio yanapelekea kupanda kwa kasi kwa bei za vyakula duniani. Na sisi kama tulivyoelezwa tunategemea zaidi chakula cha kuagiza kutoka nje kwa hivyo bila ya shaka tutaathika pakubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, hili ni muhimu kulizingatia kulisema kwa wakati huu kwa sababu tumeona katika nchi za wenzetu upungufu wa ukosefu wa chakula na kupanda kwa bei mara nyengine kunapelekea kukosekana kwa utulivu wa kisiasa, tumeona nchi nyingi zinaingia katika machafuko kwa sababu wananchi wake weanafika pahala wanakata tamaa na hawapati maelezo ya kutosha au kutafakari hizi hoja panda za kidunia, wanatizama katika mazingira yao tu. Kwa hivyo hili linapelekea umuhimu sana wa kutoa taarifa kuhusu masuala kama haya kwa sababu kama wanavyosema wenzetu mtu ambae kaingia katika hamkani anaweza kufanya hamkani kubwa katika vitendo vyake tunahitaji kuwaepusha wananchi wetu kwa kuwapa taarifa za kutosha.

Sasa kuhusiana na mswada huu Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mambo machache ya jumla halafu nitakwenda kwenye vifungu, katika mambo ya jumla yanayohusiana na mswada nilikuwa naomba kuelezwa suala moja ingawa pengine halimhusu moja kwa moja Waziri, lakini kwa sababu ndio mwenye dhamana ya mswada huu nitalisema hapa hapa. Tukisoma katika tafsiri hii inajumuisha upatikanaji wa maji. Moja katika tatizo kubwa sana katika nchi yetu hivi sasa ni suala zima la ukosefu wa maji. Wananchi wetu wengi wanapiga kelele jua ya hili. Sasa tunazungumzia lakini hata kile chanzo cha uhai ambacho ni maji bado serikali yetu imeshindwa kulipatia ufumbuzi suala hili.

Nilikuwa nina ombi moja niliseme hapa. Najua sio wizara husika lakini ndio wizara inayo *coordinate* mambo yote yatakayohusika na mswada huu. Hili litizamwe kwa umakini sana. Kama nilivyosema kwa sababu ya muda nitayasema kwa ufupi.

Jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala zima la umuhimu wa kuwatumia wataalamu wetu. Wajumbe wengi waliochangia wameeleza kwamba Wizara ya Kilimo inautajiri wa wataalamu. Ni kiasi gani tunawatumia wataalamu hao kwa kutunufaisha. Hili ndio swali. Hii linaonekana ni tatizo lakini sio katika Wizara ya Kilimo tu, inaonekana limekuwa tatizo katika nchi yetu kwa ujumla. Tunagharamika sana mara nyengine. Kwanza kuwa nao ndani ya nchi yetu na hii kubakia katika nchi yetu peke yake ni uzalendo mkubwa. Mara nyengine tunagharamika kuwawezesha kufanya tafiti. Lakini baada ya kufanya tafiti, unazikuta tafiti nyingi zimejaa katika marafu katika afisi zetu, hazifanyiwi kazi. Hili ni tatizo katika kila Wizara takriban.

Nitoe mfano mmoja. Hapa Mhe. Hija alipomaliza kuchangia alizungumzia suala la kuendeleza maeneo haya ya Ukanda wa Mashariki kwenye maeneo ya mawe.

Mhe. Naibu Spika, nilibahatika kuona ripoti moja ya utafiti iliyoandaliwa mwaka 1963 juu ya kuendeleza haya maeneo ya mawe katika ukanda wa Mashariki katika visiwa vyetu. Ripoti ile ukiisoma mpaka hii leo unaona kwamba ni *relevant* inafaa kabisa. Ninahakika itakuwa zipo nyengine ambazo zimefanyika baada ya mwaka ule. Ni kiasi gani tunazitumia ili kubadilisha hali katika nchi yetu ndio swali.

Moja katika *research find* zinazopatikana tuzifanyie kazi sio tunagharamika pakubwa kuzitengeneza halafu baadaye hazifanyiwi kazi. Tunaendelea kufanya kazi kwa mazoea kila siku.

Mhe. Naibu Spika, la tatu nataka tuzungumzie suala zima la umuhimu katika kunyanyua kilimo. Suala la kufidia gharama nchi nyingi zilizopiga hatua katika kuendeleza kilimo katika nchi za Kiafrika zilizokataa masharti ya nchi wahisani juu ya hoja nzima ya serikali kufidia kiasi fulani cha gharama ili wakulima waweze kupata pembejeo na mahitaji mengine kwa gharama nafuu wameweza kupiga hatua ya maendeleo. Katika hali ya sasa huwezi kuongeza uzalishaji, ikiwa mkulima, mbolea na pembejeo nyengine anazipata kwa bei kubwa, inafanya uzalishaji uwe mgumu.

Nchi za wenzetu yaani wahisani wetu juu ya kuwa wanatusaidia sana lakini kunakuwa na mkakati wa kuhakikisha wanawalinda wazalishaji wao. Sera kama hizi wanazozifanya kwao tukitaka kufanya nchi zetu za kiafrika wanakuwa wa kwanza kuingilia kati, wanasema hizi hazina manufaa kiuchumi, zinatupelekea kila siku kuwa wategemezi.

Mhe. Naibu Spika, Malawi ni nchi moja iliyokataa masharti hayo na ilikumbana na vikwazo vingi. Ilipoamua kuendelea na *process* yake leo Malawi ni katika nchi iliyoongeza sehemu kubwa sana katika Bara la Afrika na linauza nje badala ya kuwa nchi ambayo inakabiliwa na upungufu wa chakula kila wakati.

Serikali ilitizame hili na wizara ilitizame kwa umakini na ilisukume kwa nguvu. Katika Kikao cha Bajeti tuletewe hapa ili tuliwekee mkakati maalum, vipi kuweza kuwasaidia wakulima wetu na pia kuweza kupata pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu ili kuweza kuwapa motisha katika uzalishaji.

Mhe. Spika, jengine la nne kuhusu suala la mabwana shamba. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kwamba tunao wataalamu mabwana shamba lakini wengi wanaishia mijini hawaonekani kule ambapo wanahitajika. Pengine ni kwa sababu ya kutokuwepo huduma kule, pengine hakuna nyumba, hawana usafiri wanapohitaji kurudi mjini siku za mapumziko. Wizara itwambie

imejipanga kiasi gani kuona kwamba mabwana shamba walionao ambao tunaambiwa wataalamu ni wengi.

Mhe. Spika, la tano ni suala la Wizara ya Fedha moja katika jukumu lilopewa ni suala zima la kusaidia kupata mikopo na kuwa na sera ambazo zitakazowezesha uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Hili nalizungumza inaonekana kuna tatizo kwa upande wetu, kwa sababu bahati mbaya wanaotoa mikopo ya kuendeleza miradi kama hii ni mabenki. Mabenki hatuyadhibiti sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, leseni zake, udhibiti wake, *regulation*, inafanywa na Benki Kuu ambayo haipo chini yetu. Haidhuru sisi ni sehemu ya wenye haki katika Benki Kuu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana Benki Kuu ilichapisha ndani ya gazeti la The Gurdian, taarifa kwamba imezitambua benki kadhaa zikiwemo za ndani mpaka za nje, ambazo zimekuja kufungua matawi yake hapa Tanzania. Kutoa mikopo maalum kwa ajili ya wajasiri amali wa chini na wakati ili kuweza ku-*invest* katika masuala ya *agriculture*.

Mimi ninayokesi ya mtu katika jimbo langu ambaye ameandaa mradi mzuri tu wa kuendeleza kilimo na ufugaji katika eneo la Fuoni, kakamilisha taratibu zote. Baada ya hapo akenda katika moja ya benki zilizotajwa hapo, mpaka leo anasumbuliwa. Kwa hiyo kumekuwa kama kuna urasimu. Faida zikija zinakuja kwa jina la Tanzania na Zanzibar ikiwemo zinaingia katika mabenki haya. Baadaye maelekezo kwa upande wa Zanzibar yanashindikana kutekelezwa . Naomba hilo nalo pia serikali ilitupie macho.

Mhe. Naibu Spika, leo nimesema katika gazeti la *East Africa* hili nataka kumsaidia tu rafiki yangu Mhe. Waziri. Shirika la Maendeleo la Swiden (SIDA) limetenga dola milioni 12 kwa ajili ya kuzisadia nchi za Afrika Mashariki kufanya tafiti zinazohusiana na haya mambo tunayoyajadili hapa ya uhakika wa chakula. Wameweka mpango wanaita *The BIO resources the innovation net work for East Africa development program* wanaita *BIO innovate* ningemuomba Mhe. Waziri hebu na hili walifuatilie tuone na sisi Zanzibar kama tunaweza kuwa wa mwanzo kufikisha mapendekezo yetu pale pengine tukawezesha kufanya tafiti ili kuweza kusaidia hizi kazi zinazokusudiwa kufanywa.

Mhe. Naibu Spika, niende kifungu cha 4 kinachohusu tafsiri. Nilikuwa naomba kumu-*alert* Mhe. Waziri katika ukurasa wa 103 pale Mamlaka ya Umma, ile tafsiri haikutimia. Ukiisoma ile tafsiri ya kiingereza kuna maneno mengi yameachwa. Naomba aikamilishe tu. Mstari wa tatu baada ya inayotumika Zanzibar ile inayohusika iondoke yaingie maneno haya ili isomeke vizuri. Mamlaka ya umma maana yake ni Wizara, Idara, Shirika la Umma, Wakala,

Serikali ya Mtaa au Afsa, Umma, ambaye au ambayo, sheria yoyote inayotumika Zanzibar. Sasa kuna maneno yameachwa ambayo katika kiingereza yapo ambayo napendekeza yaingizwe kisomeke. Imeipa au imempa majukumu ya udhibiti au uendeshaji wa mambo yanayohusika na uhakika wa chakula na lishe."

Jengine Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 5(1) ukurasa wa 104 kunaanzishwa Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe ambalo litakuwa ndio chombo cha juu cha maamuzi. Mimi nilikuwa naomba tui-*qualify* chombo cha juu cha maamuzi si kwa kila kitu, isomeke kuhusiana na uhakika wa chakula na lishe kama ambavyo ipo. Unaona hata kiingereza pia haipo hivyo, lakini nayo pia tuiongeze katika kiingereza ili isomeke kuwa "hili Baraza litakuwa ni chombo cha juu cha maamuzi sio kwa kila kitu" siku moja wasije wakatwambia Baraza la Wawakilishi walifunga hapa, lakini iwe ni kuhusiana na uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Naibu Spika, nilichokiona kingine ni *serious* hichi. Kidogo napata mashaka nitavisoma hapa kifungu cha 8, kifungu cha 10 (e) na kifungu cha 13(2) (a), nitaisoma *concern* yao.

Kifungu cha 8 "Idara ya Uhakika wa Chakula. na Lishe itakuwa kama sekretariet ya Baraza na itaongozwa na Katibu Mkuu"

Pana matatizo ya lugha. Hayo nitakuja kuyarekebisha wakati wa kupitisha vifungu. Nitaomba ruhusa yako wakati huo. Lakini ile *concept* yenyewe, tunaambiwa idara ya uhakika wa chakula na lishe itakuwa kama ndio *Secretariat* ya Baraza na itaongozwa na Katibu Mkuu. Lakini ukisoma

kifungu cha 13 (2) "Idara itakuwa na:-

(a) Mkurugenzi ambaye atakuwa na jukumu la kuratibu shughuli za kila siku za Idara"

Nimefahamu kwamba inachokusudiwa kwamba ikifanya kazi kama secretariat Katibu Mkuu ndiye atakuwa Mkuu wake na akifanya kazi zake za kawaida Mkurugenzi ndiye atakuwa ndiye mkuu wake. Lakini sasa hapa tuna-*creat* mazingira yanaweza kuja kuwa na mvutano usiokuwa na sababu juu ya nani hasa mwenye dhamana. Haidhuru Katibu Mkuu kwa jumla ndiye msimamizi wa wizara nzima.

Kuna lile suala la kuamua nani anahusika na lipi katika sehemu gani. Sasa kidogo ilikuwa inanipa mashaka katika inapo-*act* kama secretariat Katibu Mkuu anatajwa hapa kwamba ndiye Mkuu wake. Lakini huku tunaambiwa

idara itakuwa inaongozwa na mkurugenzi. Lakini pia ukikisoma kifungu cha 10 (e) *confusion* inaongezeka tena, kinasomeka kwamba, hapa inazungumza ile Kamati Tendaji.

Kifungu cha 10(e) "Mkurugenzi anayehusika na uhakika wa Chakula na Lishe kama Katibu."

Katika wale wajumbe wake inayonipa mashaka kamati tendaji Mkurugenzi ndiye Katibu. Huku idara hii hii iki *act* kama *secretariat* ya Baraza Katibu Mkuu unaambiwa ndiye anayeiongoza. Lakini huku ukisoma kifungu cha 13(2) (a) kinasema Mkurugenzi ndiye Mkuu wa Idara. Sasa nadhani hapa ili kuja kuepuka mkanganyiko wa madaraka na dhamana hebu tuiweke vizuri zaidi.

Kifungu cha 11(1) "Kamati Tendaji itakuwa ni chombo cha Ushauri kwa Baraza na Idara.

Mimi najiuliza hii hali ya *structure* ya serikali na wizara kwa jumla na vyombo vyake ni sahihi. Kamati tendaji ukiisoma wajumbe wake ni Katibu Mkuu ambaye atakuwa ni Mwenyekiti, Makatibu Wakuu wa Wizara husika. Hiki kuwa chombo cha ushauri kwa Baraza sina tatizo kwa sababu hawa ni wakubwa wao. Lakini chombo hichi ambacho kinakuwa cha Makatibu Wakuu halafu kinakuwa chombo cha ushauri wa idara ambayo ipo chini yake, inanipa mashaka kidogo. Makatibu Wakuu wanakuwa washauri wa Mkurugenzi, maana idara inaongozwa na Mkurugenzi katika shughuli zake za kila siku.

Nilikuwa naomba na hili nalo vile vile atakapokuja Mhe. Waziri kidogo atupe ufafanuzi. Je, haingetosheleza kwamba chombo hiki Kamati Tendaji ikawa ni mshauri kwa Baraza tu na idara, *secretariat* ikaachwa kwa sababu itakuwa ni mtekelezaji bila ya kwamba nayo pia inapewa jukumu la kushauriwa na Kamati tendaji.

Kifungu cha 11(2)(b) "Katika kazi za Kamati Tendaji ni kuongoza, kuelekeza, kuidhinisha na kusimamia shughuli za Baraza kama ilivyoelezwa na masharti ya sheria hii."

Ukisoma kiingereza nayo ina maneno hayo hayo, mengi, mazito. Najiuliza hapa ikiwa Kamati Tendaji ndiyo yenye mamlaka ya kuongoza, kuelekeza, kuidhinisha na kusimamia shughuli za Baraza. Nani mkubwa hapa? Baraza linalosimamiwa na Kamati Tendaji au Baraza linaloisimamia Kamati Tendaji. Naona kidogo hapa pana tatizo. Mhe. Naibu Spika, ningeomba na hili tulitizame vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa hapa naomba nipatiwe ufafanuzi. Waziri akiniwekea sawa sina tatizo.

Kifungu cha 13(2)(b) "Idara itakuwa na:-.

(b) Wafanyakazi wengine kama itakavyoamuliwa na Mkurugenzi. '

Nilikuwa nasema baada ya kupita sheria ya Utumishi wa Umma haya mamlaka ya kuamua *staff* katika idara ni ya mkurugenzi wa kila idara anaamua *staff* wake au yanaratibiwa na serikali kuu kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma. Na hiko kidogo ningeomba nipatiwe ufafanuzi.

Kifungu cha 16(1)(a) hapa naomba nikiache katika ku-save muda kwa sababu kuna tatizo ambalo nitalizungumza wakati wa kupitisha vifungu.

Kifungu cha 18(2)(c) hii vile vile naomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kurekebisha ile tafsiri iliyokuwa imewekwa pale. Imeandikwa kama hivi ifuatavyo:

> "Kuhakikisha uainishaji sahihi wa mipango itakayowanufaisha walengwa na vigezo sahihi vinavyofaa."

Sasa ukikisoma kifungu hiki katika kiingereza Mhe. Naibu Spika, kinasomeka:

> *"to ensure the proper identification of eligible program beneficiaries and the correct application of eligibility criteria*."

Mimi nadhani tafsiri iliyowekwa hapa hailengi sawa. Nilikuwa naomba isomeke "kuhakikisha uainishaji sahihi wa watu wenye sifa za kunufaika na miradi na kuhakikisha vigezo sahihi vya kuwatambua wanaofaa vinazingatiwa."

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 19 nikisome kwa ujumla wake ili kufupisha muda. Hapa imezungumzwa wizara husika kila moja kuandaa bajeti yake. Lakini hapaoneshwi *coordination* ukisoma shughuli za Kamati Tendaji.

Kifungu cha 11(1)(e) "Kamati Tendaji Miongoni mwa kazi zake ni kuidhinisha mipango kazi na mapendekezo ya Bajeti ya mwaka ya uhakika wa Chakula na Lishe iliyopendekezwa na wizara husika"

Lakini shughuli za Baraza ya ku-*coordinate* ambayo tunaambiwa ndiyo majukumu yake haionekani, kama hii ndio Kamati Tendaji, ikisha inatakiwa mapendekezo yake baada ya kuyapokea katika Wizara husika niyawasilishe katika Baraza, huioni katika shughuli za Baraza. Nilikuwa naomba na hilo nalo vile vile Mhe. Waziri Kidogo atusaidie.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 23 hiki kinaweka adhabu kinasema mtu au afisa atakaekiuka, sharti lolote la vifungu vya 20,21,22 vya sheria hii amefanya kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu au adhabu zote mbili faini na kifungu.

Tatizo langu Mhe. Naibu ni kujumuisha kifungu cha 22, kwamba atakayekuwa pia amekiuka sharti hili atakuwa ametenda kosa. Kifungu cha 22 kinaeleza wajibu wa mkuu wa kaya. Tunasema wajibu wa mkuu wa familia au kaya ni kuhakikisha kuwa anatoa chakula kwa watu wote wa kaya. Maana yake tunasema kwa kifungu hiki cha 23 kwamba ikiwa mkuu wa familia atashindwa kula chakula kwa familia yake huyo ametenda kosa na anaweza kupigwa faini na hata kufungwa.

Mhe. Naibu Spika, tuangalie hali halisi ya nchi yetu ilivyo. Sisi kama serikali tumetengeneza mazingira ya kumuwezesha huyo mkuu wa familia kuweza kuwapatia chakula watu wake hata kama akishindwa tuhakikishe kwamba tunamtia hatiani. Hili kidogo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba Waziri akubaliane na sisi kwamba kifungu. hiki cha 23 kwenye *reference* ya kifungu cha 22 iondoke ili ibakie kuwa ni wajibu wake lakini mtu asiadhibiwe kwa sababu hali hiyo katika nchi yetu bado haijakuwa nzuri ya kiuchumi kuweza kumwambia mtu kuwa atakuwa ametenda kosa.

Mwisho kabisa nakuja kwenye suala la jaduweli. Mhe. Naibu Spika, jaduweli imetaja wizara nyingi, kila moja na jukumu lake. Lakini wizara moja imo lakini kwa dhamana yake nyengine nayo ni Wizara inayohusika na nishati. Hapa imetajwa kwa maana ya kuhusika na mambo ya maji. Lakini wizara zinaweza zikapanguka. Mimi nilikuwa naomba katika jaduweli tuongeze suala zima la wizara inayohusika na nishati na hasa tukitambua umuhimu wa umeme au nishati kwa jumla katika kukuza kilimo hasa katika maeneo ya umwagiliaji. Hatuwezi kukuza uzalishaji tukitegemea kilimo hicho hicho cha mvua kila siku. Kama tunazungumzia kilimo cha umwagiliaji umeme ni uhakika.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu imo katika *crisis* juu ya suala hilo. Hatujitegemei, tunategemea umeme kutoka Bara ambao wao wenyewe unashindwa kuwatosheleza. Jana tulikuwa tunasoma katika gazeti la Citizen wanasema kiwango cha uwezo wa kuzalisha wa mitambo iliyokuwepo ya gesi

hydroelectricity ni megawatt 106. Lakini inayozalishwa hivi sasa baada ya *crisis* hii ni megawatt 470 ambayo ni asilimia 67 tu ya uwezo wa uzalishaji.

Mhe. Naibu Spika, sisi kuendelea kutegemea umeme huu kila siku na hauna uhakika na tunaona hivi sasa. Nilikuwa naomba katika jaduweli iingizwe Wizara ya Nishati ili nayo ipewe jukumu la kuhakikisha unapatikana umeme wa uhakika kupata chanzo cha mbadala cha umeme Zanzibar kuwezesha kufanya shughuli za umwagiliaji maji vizuri na hivyo kutuhakikishia uhakika wa chakula na lishe.

Baada ya kusema hayo naomba niseme baada yakupata maelezo na ufafanuzi wa Mhe. Waziri nataka nimuhakikishie kabisa nitaiunga mkono hoja yake kwa ukamilifu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, angalau na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa mawazo yangu katika Mswada uliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo kuwa hai na kuhudhuria kikao hichi siku ya leo, hatuna budi kumshukuru Allah.

Vile vile natumia fursa hii kukushukuru wewe na mimi kunipatia fursa hii. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa niipongeze serikali kwa kuweza kuleta Mswada huu. Mswada huu ni muhimu sana kwa nchi yetu na umekuja katika wakati wake. Vile vile nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikumpongeza Mhe. Waziri ambaye alitupa mafunzo ili kupata chochote juu ya Mswada huu, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kutupatia ile semina ambayo ilitufunua vichwa kidogo angalau tukajua (a)(b)(c) kuhusu Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa niende katika jina la Mswada. Jina la Mswada huu limeelezwa katika sehemu ya kwanza ukurasa wa 101 inasema “sheria hiyo inajulikana kama Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Mwaka 2011.” Mimi nadhani lingeongezwa neno katika jina hili. Lingeongezwa sio “Uhakika wa Chakula na Lishe” tu pamoja na matumizi mazuri ya chakula hicho.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa wataalamu juzi walitueleza kwamba watu wanaweza wakawa wamekosa chakula na ikatokea taathira kadhaa kwa wale waliokosa chakula. Na inawezekana ikawa mtu chakula anacho lakini ikawa hakitumii chakule kile au anakitumia kwa ziada. Kwa hivyo nadhani Mswada huu kutokana na mawazo ya wataalamu ungeingiza neno hili pamoja na matumizi.

Nadhani juzi kama tutavuta kumbukumbu zetu wataalamu walitwambia kwamba mtu anaweza akawa na uzito mkubwa sana kwa sababu ya kukitumia chakula vibaya. Vile vile mtu anaweza akawa na uzito mdogo sana kwa sababu pengine chakula anacho lakini hakitumii vizuri chakula kile. Sasa katika hili ndio nikaona kwamba kwa vyovyote vile neno hili litumiwe ili watu waone umuhimu wa upatikanaji wa chakula na lishe pamoja na matumizi bora ya chakula hicho.

Mhe. Naibu Spika, tuje kwenye muundo. Anasema kutakuwa na muundo wa Baraza la Uhakika wa Chakula na Lishe. Mimi sitaki niseme kwamba wataalamu hawakuangalia vyema katika muundo wa Baraza hili. Lakini kwa mawazo yangu nadhani hili Baraza linaweza likawa mkutano wa hadhara. Kwa sababu wizara 15 ni wajumbe zinazohusika na mambo haya. Sasa mimi nadhani wizara tano tu zingetosha zinazohusika moja kwa moja na mambo haya ya chakula la lishe.

Mwenyekiti wa Baraza hili ni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambaye ndiye mtendaji mkuu wa Serikali. Maamuzi yakipita katika Baraza lile basi itakuwa rahisi kufanya mawasiliano tu ya kiserikali kama kuna maagizo kuna marejesho, yanatakiwa basi yangepitia kupitia afisi ya makamo wa pili wa Rais. Lakini kuwaingiza mawaziri 15 katika Baraza hili nadhani itakuwa wao tu peke yao ndio wamehodhi maamuzi yale.

Mimi nashauri zile asasi zisizokuwa za serikali wapatikane wawakilishi wawili waingie huku na watolewe katika Kamati tendaji waje katika hili Baraza lenye maamuzi. Pia kuwepo na wawakilishi wa wananchi angalau wawili katika Baraza lile. Ili ile hoja niliyoijenga mwanzo kwamba kuna watu hawapendi kula na huku chakula wanacho. Wengine wanatumia chakula vibaya wanazidi uzito. Uzalishaji unapungua katika nchi kutokana na uzito wao. Inakuwa si rahisi kufanya kazi kwa ufanisi. Ikiwa hatukuwaweka wawakilishi wa kwenda kuwanasihi. Kama mchangiaji aliyepita naibu Katibu Mkuu wangu hapa ana tatizo la uzito mdogo kwa sababu hapendi kula. Si rahisi mtu kwenda kumshauri Mhe. Naibu Waziri wa Afya ale zaidi ilivyokuwa chakula anacho. Lakini atakuwa mwakilishi mimi naamini kwa heshima na taadhima atawaendea kina Mhe. Mshimba awashauri kwamba wapunguze chakula.

Mhe. Naibu Spika, kuna nadharia ya sayansi ya chemia inasema: *"the rate of chemical reaction is direct proportional to active masses of the reactance".* Yaani na tija ya mchanganyiko wa kisanyansi wowote, inapatikana pale ambapo vile vilivyochanganywa ni madhubuti. Sasa ikiwa nadharia hii tutaihamishia kwenye *political sciences* na *national development,* utakutia

maendeleo ya taifa lolote hayawezi kupatikana ikiwa raia wake hawapo madhubuti na wanakuwa hawana lishe.

Mhe. Naibu Spika, katika hili Mswada huu umekuja kwa wakati ambao utawakomboa wananchi wetu, kwa ajili ya kupata chakula chenye lishe. Najenga hoja hii ukija katika ukurasa wa 109 kifungu cha 20(1) kinasema:

Kifungu cha 20(1) "Serikali inajukumu la kurahisisha upatikanaji wa haki ya chakula kwa kila mtu kwa kuendeleza haki ya kuendelea kupata nyenzo ambayo itamuezesha mtu huyo kuzalisha"

Kila mtu anasema pajengwe maghala kuhifadhi mazao. Kama kuna chakula ambacho ni *delicious* na *nutrition* na *marine food* yaani vyakula vya baharini. Vyakula vya baharini inakuwa si rahisi kuvi-*store*, wakati mswada huu unakuja ni mkakati gani wa serikali ambao wameutayarisha kwa ajili ya wavuvi ambao hulazimika kuuza samaki wao inapokuwa wakati wa bamvua. Kuna kipindi bamvua linapokufa inakuwa hakuna samaki. Wanalazimika kuwauza wakati ule kwa sababu wanakuwa hawawezi kuwa *store.* Je, serikali itawasaidia nini wavuvi pamoja na wananchi wa Zanzibar ili wavuvi waweze kuwa *stock* samaki wao waweze kuwauza katika kipindi kingine ambacho hakina samaki.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua mazao ya kilimo ni muhimu watu wanapeleka chakula pale sokoni kipindi cha mavuno utakuta kama embe zinaoza na zinauzwa bei ndogo. Mhe. Naibu Spika, ni kwa kiasi gani wizara ita-*stabilize agricultural price* ili katika kipindi cha mwaka nzima bei iwe haishuki. Hivyo watafanya vipi serikali ku-*stabilize agricultural price*.

Mhe. Naibu Spika, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Wawi hakuna matatizo na mswada huu na tunauunga mkono mia kwa mia. Lakini nina tanbihi ndogo tu kwamba mara nyingi serikali yetu inakuwa na document nyingi, lakini tatizo letu ni *transition* ya *document* katika matendo, yaani kuiondosha hizi nadharia kuzipeleka katika matendo. Kwa kweli tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno, haja yoyote ikiwa haikushughulikiwa kwa matendo basi huwa haiwi nzuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya majeruhi ya kuchangia mswada huu kwani ni mswada muhimu sana Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula yaani MTAKULA Sheria Nam. ya Mwaka 1988 na kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia kwa ufupi kidogo kuna baadhi ya mambo naomba nisaidiwe katika mswada huu muhimu. Kwanza tuanze na ukurasa wa 107.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 107 kifungu Nam. 14 sehemu ya pili kwa ruhusa yako naomba kunukuu.

“Kuwa idara inaweza kuajiri au kushirikiana na mtu au watu wowote watakaosaidia kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake”.

Mhe. Naibu Spika, hapa nikitaka kujua kuwa kweli kama watu hawa wako idara kama idara moja kwa moja ina mamlaka ya kuajiri au itaomba uajiri kwa kufuata taratibu zilizopo. Hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, la pili watu wowote maana yake ni watu wowote, hivyo ningeliomba hawa watu wowote wawe ni watu wenye sifa ambao watasaidia katika kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake. Katika kifungu Nam. 15 ukurasa huo huo wa 107 sehemu ya 2 imeeleza kuwa Mkurugenzi atakuwa ni mtu mwenye kuheshimika na mwenye sifa na uzoefu katika masuala ya kilimo, uhakika wa chakula na lishe.

Mimi najua watu wako waliokuwa na sifa ya elimu yao katika fani ya kilimo, lakini ule uhakika wa chakula na lishe sio kuwa wako watu wenye sifa hizo. Kwa hivyo, naomba pia nisaidiwe hili.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 109 kuhusu Kamati ya Uongozi ya Wilaya hii iko katika kifungu Nam. 18 sehemu ya 3 ndio iliyokusudiwa. Mhe. Spika, naomba kunukuu kwa ruhusa yako.

“Kamati ya Uongozi wa Wilaya inaweza kuanzisha kikosi kazi ili kusaidia katika utekelezaji wa kazi zake na kwamba inaweza kujumuisha watu wasiokuwa wajumbe”.

Mhe. Naibu Spika, sasa sijui kwa nini isijumuishe watu kwa idadi hiyo wanaotaka iliyokuwa ni wajumbe kwa nini hata waliokuwa sio wajumbe wajumuishwe wakati kila kitu kina muundo wake. Hilo pia ningeliomba nisaidiwe.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika ukurasa huo huo wa 19 sehemu ya 2 chini kabisa mstari wa mwisho imeandikwa fedha kupitia mfumo wa fedha wa serika, kama mfumo ni neno sawa, lakini nilifikiria ni mfuko. Pia na hapo naomba nisaidiwe juu ya hilo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni mswada muhimu sana na Mwenyezi Mungu akitujaalia ukifanya kazi inshaallah taifa letu litaweza kutoka katika hali ngumu ya ugumu wa maisha ulivyo na kupata watu wenye lishe bora na maisha bora. Kama tunavyoona kuwa uhakika wa chakula na lishe maana yake ni kuwa hali ya watu wote katika jamii husika kwa wakati wote kuwa na uwezo wa kiuchumi na uwezo wa kupata chakula cha kutosha kilicho salama, chenye virutubisho sahihi na kukidhi mahitaji ya lishe.

Mhe. Naibu Spika, upatikanaji wa chakula hiki unatokana na ardhi yetu ilivyo, ardhi ndio inayozalisha. Mhe. Naibu Spika, ardhi yetu tunaijua namna ilivyo kwa sababu ya umasikini tulionao ilivyokuwa katika hali duni sana kuna uharibifu wa mazingira mkubwa sana, ukataji wa miti ovyo. Tunajua miti inapokatwa kwa wingi kiasi chote hicho, basi ardhi inakauka, mbolea inakimbia na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna uhaba wa maji ya kutosha kwa hivyo ili tuweze kufikia katika hali hii ni lazima zile wizara zote husika zilizotajwa katika mswada huu kusaidia Wizara ya Kilimo ifanye kazi kila mmoja kwa upande wake kuona kuwa lile lengo lililokusudiwa linafikiwa. Mhe. Naibu Spika, vyenginevyo mswada utakuwa umekaa na kila wizara inafanya kazi zake na tija haitopatikana.

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu tumeshuhudia kabla ya mswada huu ilikuwa ikifanya kila inavyowezekana kuona kuwa ile hali ya kupata chakula bora kwa wananchi wote na ubora wa maisha unapatikana, lakini imeshindikana kutokana na mambo kadhaa. Kwanza kwa serikali kwa wizara kutoshirikiana kwa pamoja kuona kuwa ardhi yetu inaweza kufanya hivyo shughuli.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili tuangalie katika mambo tuliyoyafanya na tujifunze kwa sababu ni yakurejea yale kwa yale. Kwa mfano, serikali yetu ilijitahidi sana kuhamasisha wafugaji wawe na ng'ombe bora wenye maziwa mengi na nyama nyingi, kuku, mbuzi na wengineo na tulianza kwa mpango wa kopa ng'ombe ulipe ng'ombe mpaka sasa tunatafuta kizazi kwa kutumia sindano. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba matokeo yake ng'ombe wanazaa lakini wanaozaliwa hawafiki kuzaa wenzao wanakufa. Huwa tunapata mbegu nzuri tu lakini haziwezi zikaendelea huwa zinakufa.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo ukija kwa upande wa kuku ndio hivyo hivyo tokea tunaanza kwa kuku wale wa kigeni mpaka sasa tunafanya *cross breeding* na kuku tulionao, lakini bado tija haijapatikana kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi natoa ushauri tunapofanya jambo lolote tujue kuwa ni lazima wataalamu wetu tunawatumia vilivyo na ikiwa hawapo watafutwe. Kwa

mfano, unapochukua mbegu ya nchi nyengine ukataka kuizalisha katika nchi yako ni lazima tuhakikishe kuwa tumesoma mazingira vizuri ya kule mbegu inakotoka pamoja na umbile la maisha ya vile viumbe vinavyowekwa kabla hatujaja sisi huku tukafanya *cross breeding* kwa kutarajia kuwa tutapata kizazi chenye sifa kama kinachohitajika. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu mimi ili kuingia huko katika kilimo na katika mifugo ni lazima tuanze kujipanga kupata wataalamu ambao wataweza kutushauri kuwa hii mbegu kwa hapa Zanzibar inaweza ikaendelea na mbegu hii haiwezi kuendelea kwa hapa petu. Mhe. Naibu Spika, vyenginevyo itakuwa tunapoteza pesa nyingi muda unakwenda na wala tija haipatikani.

Mhe. Naibu Spika, najua unataka kunikatisha naomba japo kidogo nimalizie. Mhe. Naibu Spika, tukija kwenye kilimo pia tumejitahidi sana, katika kilimo cha irrigation tulichokuwa tukikifanya tukichukua mbegu fupi sana. Mhe. Naibu Spika, tumekuja katika muhogo kuna mbegu mpaka tena wakulima wanaziita Sepideh kwa vile ni za muda mfupi na kuzaa. Lakini baya mbegu ile baada ya kuvuna haiendelei utaona imepotea moja kwa moja. Kwa hivyo, kufanya jambo ni moja lakini kulifanya likafanikiwa ni jambo jengine, hivyo mimi naomba utaalamu wa hali ya juu utumike ili tusiwape tamaa wafugaji wetu na halafu badala yake tukaona kuwa wamepata hasara kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine ili kupata lishe bora ni lazima tuwe cha chakula cha protein cha kutosha, sehemu kubwa tunaipata kwenye wanyama, mboga mboga na samaki. Kwa hivyo, tukielekea katika upande wa bahari Mwenyezi Mungu katujaalia kuwa Zanzibar imezungukwa na bahari na ina mali asili kubwa sana bahari yetu, lakini Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya umasikini wetu imefika mahala sasa Zanzibar haitoshelezi hata kwa samaki kutokana na hali ngumu ya uvuvi tunayoifanya ambayo ni ya kuuwa mazingira ya baharini.

Mhe. Naibu Spika, uvuvi tunaoufanya wa kutumia nyavu ndogo, wakutumia mabomu na kadhalika unasababisha mandhari ya bandari yetu pamoja na mazalio ya baharini kuondoka na matokeo yake bahari imebakia kavu kama ilivyo kwenye ardhi. Kwa hivyo, ili kulifikia lengo hili Mhe. Naibu Spika, kwa sababu watu hawafanyi hivi kwa kutaka, wanafanya kutokana na hali ngumu ya maisha ilivyo. Kwa hivyo, kwa makusudi kabisa serikali ingalijipanga kuwasaidia hawa wananchi waliokuwa hawana njia nyengine ya kuendeleza maisha yao isipokuwa kufanya hivyo wanavyofanya, waingie katika ile hali ambayo si ya kuharibu mazingira kwenye ardhi, si ya kuharibu mazingira kwenye bahari wasaidiwe kwa namna ambayo na kushughulikiwa kuona hili lengo lilokusudiwa katika mswada huu linafikiwa vilivyo.

Mhe. Naibu Spika, ilikuwa nizungumze mengi lakini kwa vile muda hakuna, nashukuru kwa hapo nilipofika.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kujumuisha michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar kwa mswada huu muhimu sana kwa mustakbal wa nchi yetu. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza na Chakula MTAKULA ya Mwaka 1988 na Kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, mswada niliowasilisha mbele ya Baraza lako tukufu umechangiwa na wajumbe 20 kwa ruhusa yako naomba niwataje.

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Mohammed Mahmoud Mussa
4. Mhe. Assaa Othman Hamad
5. Mhe. Hamza Hassan Juma
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
7. Mhe. Panya Ali Abdalla
8. Mhe. Ashura Sharif Ali
9. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
10. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
11. Mhe. Hassan Hamad Omar
12. Mhe. Ali Salim Haji
13. Mhe. Hija Hassan Hija
14. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
15. Mhe. Saleh Nassor Juma
16. Mhe. Salim Abdalla Hamad

Mhe. Naibu Spika, na hawa wengine wamechangia kwa maandishi nao ni:

1. Mhe. Asha Abdu Haji
2. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
3. Mhe. Farida Amour Mohammed na
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali ya muda na kwa vile Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wameufahamu kwa kina hasa maana na sababu na madhumuni ya kuleta mswada huu wakiwa wawakilishi wa wananchi wa nchi yetu, hivyo naomba nende moja kwa moja katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe.

Salmin Awadh Salmini Mwenyekiti wetu juu ya ushauri wake kwa nyanja mbali mbali juu ya mswada huu pamoja na maelezo yake juu ya umuhimu wa kuwa na maghala ya chakula ya kujitosheleza na pia kuzingatia ubora wa chakula ambacho tutakihifadhi katika maghala hayo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kwa kuanzia maghala tuliokuwa nayo yanayomilikiwa na wizara yangu pekee ni kwamba tunayo ya kutosha na tuna uwezo wa kuhifadhi chakula cha hadi miezi mitatu kwa mahitaji ya nchi yetu. Tunaamini na utaratibu wa kuendelea kuratibu maghala tuliokuwa nayo nchini yanayomilikiwa na serikali na taasisi za serikali unaendelea na tunaamini kwamba kwa kuanzia tutakuwa nayo maghala ya kutosha hivyo tutazingatia ubora wa chakula ambacho tunahifadhi, lakini lengo la mwanzo ni kuzalisha chakula cha kutosha ili tuweze kununua kwa wakulima wetu. Kwa hivyo, ile hoja pia ya masoko kwa ajili ya wakulima ambayo yamezungumzwa na wawakilishi wengi ni moja njia ya kutatua ni kuweza kununua chakula kilicho bora na kuhifadhi kutoka kwa haya yote tunayoyazingatia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti wetu pia alizungumza juu ya aina ya chakula cha kuhifadhi, kwa maana tusihifadhi chakula aina moja. Hilo nalo litazingatiwa kwa upeo wake.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwa Mhe. Rashid Seif Suleiman namshukuru kwa mchango wake amezungumzia umuhimu wa kuwa na sera ya matumizi bora ya ardhi. Sera ya ardhi ipo naamini kwamba wizara husika ya ardhi na makaazi inafanya mapitio ya sera hiyo ili iendane na wakati na kukidhi matumaini ya wananchi na haja zao kwa wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, pia amesisitiza umuhimu wa kilimo cha kutumia *machine*. Mhe. Naibu Spika, niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kwamba serikali kuwa wizara yangu inaendelea kujipanga vizuri ili kuwa na mikakati iliyokuwa bora na endelevu hasa katika suala zima hili la kutumia *machine*, matumizi ya mbolea, matumizi ya mbegu bora na taaluma kwa wakulima wetu.

Mhe. Naibu Spika, tunategemea na hili naanza kulishawishi hapa pengine Waziri wa Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo atayasikia, ni kwamba lengo ni kuishawishi serikali kwamba kwa bajeti hii kilimo kifikie asilimia 7 ya bajeti ya serikali. Waheshimiwa Wajumbe nyinyi mkiwa wawakilishi wa wananchi na wananchi wengi takriban wote wa nchi hii ni wakulima au wafugaji basi naamini mtaliunga mkono ili tuweze kuwa na nguvu zaidi kuweza kukidhi matumaini ya wakulima wetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid amezungumzia muundo wa Baraza kifungu cha 5 (1c) kwamba orodha ni kubwa mno, hilo limezungumzwa na wengi. Mhe. Naibu Spika, hili la uhakika wa chakula na lishe haliwezi kufanywa na wizara moja, Wizara ya Kilimo na Maliasili itakuwa msimamizi na mratibu wa suala hili la uhakika wa chakula na lishe. Lakini bila ya kuwa na maingiliano na sekta hizi nyengine na zilizotajwa kazi hii haiwezi kufanyika na kila aliyetajwa humu ana umuhimu wake wa pekee hasa pale kwenye masuala ya kupitia mipango wenyewe, pia wakati tunapopatwa na dharura. Kwa mfano, majanga haya ya ukame na wengine lazima tupate ushiriki wa taasisi takriban zote hizi kuweza kukabiliana na majanga hayo na mapungufu hayo yatakapokuja kujitokeza.

Kwa hivyo, niwaombe sana na hizi kamati hazikai kila siku na wote waliokuwemo humu wana kazi zao ndani ya serikali. Kwa hivyo, hawalipwi mishahara ya ziada, ni watu ambao wanaendelea kufanya wajibu wao, hivyo ukitengenezewa chai na kahawa hayo ni mambo ya kawaida katika utaratibu wetu. Lakini hakuna muelekezo wa posho humu wala gharama za ziada kukimu mahitaji ya watu hawa watakuwa wanafanya wajibu wao wa kawaida. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wanikubalie hilo muundo huu umepewa fikra ya kina na tumeona kwamba baada ya kuyajadili na kupitia moja baada ya moja kuna umuhimu wa wote hawa kuwepo.

Mhe. Naibu Spika, pia amezungumza jambo moja la msingi kabisa kwamba mswada haukuzungumzia kuweka uwiano wa bei kwa kutoa chakula cha akiba wakati kuna mfumko wa bei katika soko. Sio kila jambo tunaweza kuliweka kwenye mswada wa sheria, lakini katika utaratibu wa kanuni hilo limezungumzwa kwa kina katika ngazi zote za serikali na akiba hii pia itatumika pale ambapo kuna upungufu wa chakula pia bei zilizopanda ghafla ili kuweza kushusha bei kama ilivyo hali hii na mazingira ya sasa tuliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, alizungumzia kwamba sekretari ni chombo kidogo lakini kwa mtizamo wangu sina tatizo nalo hilo kwa hivyo chombo kikubwa kitajwe mwanzo na kidogo kitajwa na pia Mwanasheria Mkuu yupo wa Serikali ataliona hilo na tutafanya marekebisho katika mswada wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Mhe. Mohammed Mahmoud Mussa kwa mchango wake na ushauri wake wa kina aliotupa yeye pia akiwa Mjumbe wa Kamati yetu, tunamshukuru sana. Vile vile alizungumzia viwango vya fedha katika kuhakikisha vinaenda kwa hali halisi wakati zinapofika haja hizo. Kimsingi ushauri wake na maelekezo yake yote mimi nakubaliana nayo ya msingi kabisa na ya kina na tutayafanyia kazi kwa umuhimu huo huo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwa Mhe. Assaa Othman Hamad namshukuru sana, hili azimo la maputo nimelizungumzia kwamba tunategemea mwaka huu wa fedha serikali itatukubalia kwamba sasa tuende kwenye asilimia 7 na miaka ijayo tufike kwenye lile lengo la azimio la maputo la asilimia 10. Dhamira ya serikali pia ni kuendelea kuwawezesha wananchi hasa vijana, kwani rika la vijana limekimbia sekta ya kilimo, vijana hawalimi, wakulima wetu wako kwenye umri wa kati wanaelekea kwenye utuuzima. Hili nalo pia linaleta kupungua sana uzalishaji kwenye nchi yetu. Kwa hivyo, tuna mipango na mikakati thabiti ya kushirikiana na wizara inayohusiana na uwezeshaji, Wizara ya Fedha ili kuweka vivutio kwa ajili ya vijana wetu kushiriki kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Mhe. Naibu Spika, hiyo pia iwe sehemu moja ya kupata ajira kwa ajili ya vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, vianzio vya maji ni hakika kabisa bila ya kuwa na usimamizi mzuri katika vianzio vya maji tunaweza tukapata taathira kwenye kilimo na shughuli nyengine za kuimarisha uchumi wetu. Jengine ambalo limezungumziwa na yeye na Mhe. Jussa alizungumzia kwa umakini zaidi ni fidia kwa ajili ya pembejeo.

Mhe. Naibu Spika, hili ni la uhakika zaidi na kama alivyozungumza Mhe. Jussa miaka mitatu nyuma tu nchi ya Malawi ilikuwa kila mwaka inapata ukame na pia ukosefu wa chakula. Lakini baada ya kuingia katika kufidia pembejeo sasa hivi Malawi sio tu kunajitosheleza kwa chakula bali inasafirisha nje. Wakulima wa Malawi ni wadogo wadogo kama tuliokuwa nao sisi hapa, wengine wanalima kwenye robo eka, wengine nusu eka, kwenye robo tatu ya eka. Kwa hivyo, tayari serikali yetu inafidia pembejeo hizi kwa asilimia 50 kwa maana ya mbegu bora, mbegu pamoja na mbolea na hata *mechanization*.

Lakini serikali imeona bado hivi sasa tumo katika mazungumzo na majadiliano ndani ya serikali kuona kwenye msimu ujao na katika utaratibu wetu wa bajeti kwamba bado serikali inakuwa na mpango madhubuti hasa uliokuwa rasmi katika kufidia wananchi kwenye mbolea, mbegu na *mechanization* kwa maana ya matrekta na mengineyo, pia tutakuja na programu ambayo itakuwa pana zaidi. Kwa hivyo, tunategemea kuanzia mwaka ujao hali halisi kwa wakulima wetu itakuwa nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikenda kwa Mhe. Hamza Hassan Juma namshukuru sana kwa michango yake namuomba aniruhusu niende moja kwa moja kwenye maeneo matatu ambayo ameyazungumza. Nianze la mwanzo ambalo alisema atazuia kifungu mimi najua hafanyi hivyo. Mimi niseme tu kwamba ninakubaliana nae na kwa sababu hili limezungumzwa na wajumbe wengine kwamba sina tatizo na Mkurugenzi wa Uhakika wa Chakula na Lishe

kuwekewa sifa. Kwa hivyo, sifa za uzoefu angalau shahada ya mwanzo hilo tunalikubali na tutalifanyia utaratibu uliokuwa rasmi.

Vile vile amezungumzia misumeno ya meno na namna inavyoteketeza miti hasa ile ya asili ya matunda. Hilo ni sahihi tupo katika hali mbaya lakini tumeshaanza harakati tunashirikiana na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na tayari Idara ya Mazingira na Idara ninayoisimamia mimi ya maliasili zisizorejesheka wamo kwenye kupitia sheria na kuandaa kanuni ili tuweze kuendelea kudhibiti matumizi mabaya ya misumeno ya moto na uchimbaji mbaya wa mchanga. Mhe. Naibu Spika, siku mbili tatu zilizopita idara yangu tayari imeshaanza mikakati hiyo wakati haya tunaendelea lakini mkakati sasa hivi thabiti ili mkono wa serikali uonekane tayari katika siku ya Jumamosi na Jumapili tumekamata misumeno 14 na tutawafikisha mbele ya sheria na kuna magari kadhaa tumeyakamata ambayo yanajishughulisha na uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Naibu Spika, wote hao tutawapeleka mbele ya sheria tuliamua kwa makusudi tusiwe tunapiga kelele sana lakini tuoneshe mifano kwa sababu tuna hofu kwamba hao tunaowakamata ni wapiga kura wetu. Kwa hivyo, hatimae wenzangu mtanipata ili kuwe na shufaa lakini naomba kwa hili kwa wale ambao wanachangia katika kuangamiza mazingira yetu aidha kwa kuchimba mchanga ovyo au kukata miti ya maana ndani ya nchi yetu, jamani tusiwaonee huruma.

Ninawahakikishia Wajumbe wa Baraza lako hili kwamba sisi mikakati hiyo tutaendelea nayo na mkono wa serikali utaonekana katika kusimamia masuala yote hayo mawili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na Mhe. Suleiman Hemed Khamis namshukuru sana kwa mchango wake na yote aliyoyaeleza tutayapokea.

Mhe. Bi Panya Ali Abdalla naye tunamshukuru sana kwa michango yake na maelekezo yake aliyotupa na mengi ambayo nimeyazungumza nimemgusa na yeye pia.

Mhe. Ashura Sharif Ali na yeye namshukuru sana, nakubaliana naye kwamba chakula ni msingi wa uhai wa binadamu na nakubaliana na ushauri wake. Nilizungumza hili la mabibi na mabwana shamba, ni kweli kabisa Mhe. Naibu Spika, limekuwa ni gumzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi takriban wote kwa sababu kama nilivyokwishasema, Wazanzibari takriban sote ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Tunawahitaji mabibi na mabwana shamba kuwa karibu nasi katika kutupa taaluma.

Bahati mbaya hivi sasa bibi na bwanashamba mmoja anahudumia wakulima karibu 2000, anapaswa kuhudumia wakulima 400. Tunategemea kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kuanza utaratibu wa kuajiri vijana waliotoka Kizimbani karibu 107. Lakini hapo pia tuna tatizo, kwa maana imekuwa vijana hawa sasa na wengi wanatumia wizara yangu ya Kilimo na Maliasili kama mlango wa kutafutia ajira na baadae wanatukimbia. Tunawaajiri mabibi na mabwanashamba hawendi mashamba wanabaki mjini baadae wanaombewa kubaki katika idara ambazo hazihusiani na ile sababu ya msingi tuliyomuajiri.

Kwa hivyo, nikiwa waziri nimekuwa kidogo nalitizama hili jambo kwa upeo wake, kwanza nataka tujiandae na mikataba ambayo itawafunga hawa tuliowaajiri. Kwanza wakubali kufanya kazi ndani ya wizara kwa muda maalum bila ya kutoweka au kutafuta sababu za msingi za kutukimbia, pili wafanye kazi pale ambapo tutawataka wafanye kazi, kama hawajafanya hivyo, nataka niwahakikishie kwamba hatutorudi nyuma sasa katika kuwafukuza kazi.

Sasa vijana hao wanatumia Wizara ya Kilimo na Maliasili kama mlango wa kupitia kwenye ajira halafu wanatukimbia hasa wale ambao tunawahitaji wakae vijijini. Kwa hivyo, tutaendelea na zoezi hili la kuajiri vijana wetu wanaotoka Kizimbani na wale tu ambao wametoka Kizimbani, hatutochukua mwengine nje ya utaratibu huo labda awe na sifa ambazo tunazihitaji na tutakwenda nae. Lakini tutawaajiri kwa mkataba maalum na wakishindwa kukidhi sharti hizo tutawaondosha kwenye utumishi wa serikali na tutaendelea kuwasomesha na kuajiri vijana ambao wanataka kufanya kazi ambayo tunawaajiria.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na yeye namshukuru sana na mchango wake na yote aliyotelekeza pamoja na Mhe. Shawana Bukheti Hassan tutayazingatia kwa kina.

Mhe. Hassan Hamad Omar naye namshukuru sana kwa mchango wake, ni sahihi kabisa kwamba bei za vyakula zinapanda na njia moja ya kukabiliana na kupanda kwa bei ya chakula ni uzalishaji wa ndani. Tuna nafasi kubwa katika kilimo cha mbogo mboga, maua na kilimo cha kudumu kwa maana ya matunda. Tunaendelea kupiga vita nzi wa matunda na hivi karibuni utaratibu wa kununua dawa na mitego umeshafikia pahala pazuri tutaendeleza zoezi la kusambaza mitego katika wilaya zote 9 tulizokuwanazo kwa maana ya hii ya mjini haitokuwa na kipaumbele hicho.

Zoezi hilo linaendelea na tunategemea mwakani matunda tutayapata kwa wingi zaidi na kuwapa matumaini wale ambao walikuwa wanasafirisha matunda kutoka Zanzibar ambayo kwa ladha na kwa maumbile ni ya aina ya pekee, kinachopatikana Zanzibar kwa maumbile na utamu hakipatikani kwengine

popote. Kama tunavyoelewa cha Zanzibar maisha kitamu. Kwa hivyo, tunategemea kwamba wakulima wataanza kujenga matumaini sasa na kujipanga upya katika kusafirisha matunda na hiyo kuchangia katika ajira na kuwawezesha wakulima wetu kulima zaidi.

Mhe. Ali Salum Haji naye tunakubali mchango wake, Mhe. Hija Hassan Hija na yeye namshukuru sana kwa mchango wake na yote aliyoyazungumza tutayazingatia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu namshukuru sana, kuna badhi nimeshayazungumza nakubaliana naye kwamba, upungufu wa chakula unaweza ukaondosha hali ya utulivu wa kisiasa, wananchi wanakuwa hawatulii na hali hii tuliyokuwanayo hivi sasa ya hata ule mchele wa chini ambao tunauita Mapembe umepanda sana, sukari imepanda, unga wa ngano na mafuta, pamoja na jitihada ya serikali kuondosha kodi bado hali hii imekuwa ngumu kwa wananchi wetu. Tunategemea mwezi wa Aprili Vietnam, Indonesia na kwengineko watakaoanza kutoa sasa zao jipya na kuweka sokoni dalili za kuanza kupungua bei za mchele inaonekana, lakini hapo hapo bei ya mafuta inazidi kupanda.

Kwa hivyo, pengine nafuu ya moja kwa moja itakuwa ngumu kupatikana, lakini serikali itaendelea kuwekeza kwenye kilimo ili tujitegemee na tusidharau kwamba kwa sababu ya upande wa mihogo, ndizi na vyakula nyengine nya msingi kama matunda tunajitegemea wenyewe tayari. Tatizo letu kubwa ni zao letu kuu (mchele). Kwa hivyo, tutaendelea kuwekeza tujitosheleze zaidi katika uzalishaji wa mihogo, ndizi na vyakula vyengine na tutaendelea kuwekeza ili tuweze kutimiza lengo la serikali, kwamba ifikapo mwaka 2015 angalau basi zaidi ya asilimia 40 hadi 50 ya mahitaji yetu ya ndani ya mchele tuwe tunazalisha sisi wenyewe.

Mhe. Jussa pia amezungumzia suala la fidia hilo nimeshalizungumza, amezungumzia masuala ya benki kwamba mabenkio hayatoi mikopo kwa wakulima yenye masharti nafuu. Mikopo wanatoa, lakini wakulima hawapati mikopo kwa maana ya kwanza kile cha kuweka dhamana (mali) kigumu kwao kupatikana. Lakini kwa bahati nzuri serikali tangu mwaka jana imeshabadilisha sheria yake ya ardhi kwa hivyo, sasa mkulima anaweza kutumia ardhi kuweka zamana. Tayari tumeshapitisha utaratibu sasa mali zinazoweza kuhamishika nazo kuwekwa dhamana kwa hivyo, mazingira ya kumuandalia mkulima nayo ili aweze kutumia ardhi na mali zinazohamishika kama dhamana anazo tujeshapiga hatua.

Kwa hivyo, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuzungumza mabenki haya na pia mpango wetu wa kuanzisha Benki ya Wakulima ili wakulima nao wapate nafuu. Kuendelea kutumia miradi

yetu hii ya *SSBP* pamoja na *PADEP* na *TASAF* pia kuwawezesha wakulima wetu. Namshukuru kwa kututanabahisha kwamba *SIDA* imetenda shilingi milioni 12 kwa ajili ya tafiti tutalifanyia kazi hilo.

Pia amezungumza taafsiri ya Mamlaka ya Umma haijakamilika na irekebishwe. Sina tatizo na hilo, lakini kama alivyosema mwenyewe alikuwa anazungumza haraka haraka kutokana na muda, tutapopitisha vifungu kimsingi sina tatizo na hilo Mwanasheria Mkuu naye atatusaidia ili tafsiri hiyo iendane na ile iliyokuwemo kwenye mswada wa Kiingereza.

Vile vile ametaka Baraza la Taifa liwe na maamuzi ya juu lakini kuhusu uhakika wa chakula na lishe nalo hilo nalikubali marekebisho hayo tutayafanya. Amezungumza idara kuwa sekretarieti, Katibu Mkuu ndio anakuwa mkuu, lakini inakuwa tofauti. Nalo hilo kimsingi sina tatizo nalo na ninakubaliana naye. Ametaka kifungu Nam. 2 Kamati Tendaji iwe inashauri Baraza tu na sio idara, nalo hilo sina tatizo nalo.

Kifungu nambari 13(b) nani anaamua idadi ya wafanyakazi. Kimsingi idara inaomba kama utaratibu wa serikali ulivyo na mamlaka zilizokuwa juu ya idara ndio zinapanga wafanyakazi wangapi wenye taaluma ipi wanapaswa kuajiriwa na kwa utaratibu upi. Hili lilizungumzwa na zaidi ya mjumbe mmoja kwa hivyo nalijibu kwa pamoja.

Kifungu cha 18(2)(c) alitaka marekebisho, lugha nalo hilo pamoja na hayo mengine nakubaliana nayo. Kifungu cha 22 kinachozungumzia habari ya Mkuu wa Kaya kushindwa kutoa chakula kwa Kaya yake. Hili nakubaliana naye, tunaweza tukafanya marekebisho ya lugha pale na hapo nitamuomba Mwanasheria Mkuu ikiwa mkuu wa Kaya kwenye kifungu cha 22 pengine atafanya hivyo kwa makusudi akazuia Kaya yake pengine kujishughulisha na kilimo kwa njia za halali, basi huyo anaweza akachukuliwa hatua.

Lakini kwa mazingira hayo aliyoyazungumza Mhe. Ismail Jussa na mazingira ya hali halisi ya uwezo wa wakulima wetu basi nakubaliana naye. Kwa hivyo, na yeye namuomba anikubaliye tuongeze maneno hapo ikiwa huyo Mkuu wa Kaya kufanya kwa makusudi, kuingilia utaratibu wa Kaya yake katika kulima na kujipatia chakula kwa njia za kihalali, lakini Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia kuliweka katika lugha muwafaka zaidi.

Pia alitaka Wizara ya Nishati kuongezwa kwenye jadweli. Hilo nalo nakubaliana naye, kwa sababu katika mpango wetu wa kuelekea kwenye kilimo cha umwagiliaji maji bila ya umeme wa uhakika fedha zote ambazo tutaziwekeza zitakuwa hazileti maana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Jussa na

kama nilivyomwambia Mhe. Hamza Hassan Juma na wengineo wasizuie vifungu kimsingi nimekubaliana nao kwa yote ambayo wameyaleta.

Mhe. Saleh Nassor Juma alitaka neno 'matumizi ya chakula' liongezwe kwenye mswada. Kama nilivyokwishasema Mhe. Saleh kwamba sio kila jambo tunaweza kuweka kwenye mswada wa sheria, ninamuomba kutokana na umbile lake la kimataifa jina hili atuachie. Katika utaratibu wa kutunga kanuni bila shaka masuala ya matumizi halisi nayo tumeyazingatia na nakubaliana naye kwamba ni jambo la msingi kabisa nitalifanyia kazi kwa misingi hiyo.

Amezungumza kwamba na baraza ni kubwa mno lakini hili hili nimelitolea ufafanuzi. Alitaka wawakilishi wawili wawemo namuomba akubaliane na mimi huu muundo tulioupendekeza kwa hili hivi unatosha, ikiwa tunazungumza kubwa tukaongeza zaidi inaweza kuleta mtafaruku mkubwa zaidi. Waliopangwa wote wamepangwa kwa sababu ya misingi ya kuwepo kwao.

Pia alizungumzia utaratibu wa kuweza kuwasaidia wakulima wetu na wafugaji kuhifadhi chakula. Mheshimiwa usarifu wa mazao ni jambo la msingi kabisa ambalo limekosekana hapa kwetu. Niseme kwamba kwa upande wa Pemba jitihada za wananchi wenyewe wakulima na wavuvi zinaonekana. Pemba wako wakulima wanakausha maembe kwa kiwango cha juu sana na wanasafirisha Afrika ya Kusini hivi sasa.

Pemba wako wavuvi wanakausha dagaa na limeanza kutumika katika ukanda huu wa Afrika na Mashariki, sina taarifa ya uhakika kama tunasafirisha nje ya nchi. Hao tutaendelea kuwasaidia na tunayo mipango ya kuwasaidia wakulima wetu kote nchini kuweza kusarifu kile ambacho wanakifuyga kwa maana ya samaki au wanakivua pamoja na upande wa kilimo na tayari kituo kinaendelea kujengwa Kizimbani kwa ajili ya shughuli hiyo. Katika mipango yetu ya muda mrefu hilo nalo tumelizingatia.

Hivi sasa tunao mradi ambao tunaendelea katika mazungumzo na umefika katika hali nzuri, unaitwa (*Marketing Initiative Value Addition* na *Rural Infrastructure)*. Mradi huu unafadhiliwa na *IFAD*, Benki ya Maendeleo ya Afrika na *NGOs* ya *Green Revolution for Africa*, neno lake kwa ufupi silijui halinijii hivi sasa, ambapo Bodi ya *IFAD* tayari imeshaukubali mradi huo tunategemea *African Develop Bank* itafanya hivyo hivyo.

Mradi umekusudia kujenga masoko ya wilaya, miundombinu ya vijijini, kwa maana ya kurahisisha mwenendo wa vyakula na mifugo, pia kujenga *cold storage* katika kuhifadhi nyama, samaki na kadhalika na pia kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji wetu ili waweze kusarifu mazao yao na kuyahifadhi nje ya msimu, kwa maana wakishakuuza kile ambacho wanataka kuuza lakini pia

waweze kukausha, kuhifadhi na kuendelea kutumia na kuuza baada ya msimu huo. Kwa hivyo hayo yote tunaendelea kuyazingatia na tutayaongezea nguvu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad alizungumzia kifungu cha 14(2) juu ya masuala ya Mamlaka ya Idara kuweza kuajiri, nimeshalijibu hilo. Alizungumzia kipengele cha 15(2) kuhusu habari ya sifa ya Mkurugenzi nalo hilo nimezungumzia, alizungumzia kifungu cha 18(3) Idadi ya Wajumbe nalo hilo nimelizungumza, alizungumza nene 'mfumo' au 'mfuko' nadhani ni mfuko, lakini kwa vile alikuwa anazungumza haraka haraka sijampata vizuri, lakini niko tayari kulizingatia hilo wakati wowote ule.

Pia amezungumzia masuala ya matumizi ya ardhi. Niwashukuru wale wajumbe ambao wamechangia kwa maandishi, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Farida Amour Mohammed na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Yale yote ambayo wamenielekeza, wamependekeza na kushauri ipasavyo wakiwa wawakilishi kinamama zaidi waliotiliwa mkazo juu ya kuwalinda na kuwawezesha kinamama na wao ambao wana mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu, ninawahakikishia kwamba tunalithamini hilo na tunalifanyia kazi kwa upeo wake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji Wajumbe wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wasioafiki, walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2011

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2	Wizara husika

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ya lugha tu kifungu kidogo cha pili, waziri anaweza kwa kutoa notisi nadhani neno la Kiswahili ni taarifa. Naomba tufanye marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu na ninakubaliana naye, Kifungu cha 3

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 3(1) naomba Baraza lako liridhie baada ya kutumika neno wakaazi wote wa Zanzibar iwe wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mjumbe na nakubaliana na yeye.

Kifungu cha 3 Matumizi ya sheria pamoja na marekebishoyake
Kifungu cha 4

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa natoa mchango wangu nilizungumzia kifungu cha 4 katika tafsiri ya Mamlaka ya Umma na Mhe. Waziri aliniomba wakati wa kupitisha vifungu nilieleze tena kwa utulivu zaidi, kwa sababu wakati ule nilikuwa nina tatizo la muda. Namuomba aangalie tafsiri ya Kiingereza katika ufafanuzi wa kifungu hicho Mamlaka ya Umma kwa maana ya *Public Authority* imeelezwa hivi:

"Public authority" means a Ministry, department, parastatal, argency, local government or public officer in which or in whom any law in force in Zanzibar, vests function of control or management of matters related to food security and nutrition".

Sasa katika tafsiri ya Kiswahili haya maneno 'vest' function of control of management of matters releted too yameachwa. Kwa hivyo, ndio maana nilikuwa naomba katika ile tafsiri ya Kiswahili kwa sababu ndio tuliyoipitisha hapa hasa katika Baraza tuichukue tafsiri kama ilivyo, Mamlaka ya Umma maana yake ni wizara, idara, shirika la umma, wakala, serikali ya mtaa au afisa wa umma ambaye au ambayo sheria yoyote inayotumika Zanzibar. Sasa pale inayohusika neno 'inayohusika' tuifute halafu tuongeze maneno 'inayotumika Zanzibar imeipa au imempa'.

Kwa sababu kule juu kuna ambae na ambaye, imeipa au imempa majukumu ya udhibiti au uendeshaji kwa maana ya ile *control or management,* udhibiti au uendeshaji wa mambo yanayohusiana halafu tutaendelea pale na uhakika wa chakula na lishe. Kwa hivyo, naomba isomeke niirejee tena kwa Kiswahili kwa ukamilifu wake.

“Mamlaka ya Umma maana yake ni wizara, idara, shirika la umma, wakala, serikali ya mtaa au ofisa wa umma ambaye au ambayo sheria yoyote inayotumika Zanzibar imeipa au imempa majukumu ya udhibiti au uendeshaji wa mambo yanayohusiana na uhakika wa chakula na lishe”. Mhe. Mwenyekiti, naomba marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kusema wakati najumuisha kwa vile tunarekebisha iendane sawa na ule Mswada wa Kiingereza, niko tayari nimeshamkubalia tangu mwanzo Mhe. Mjumbe. Kwa hivyo, mimi sina tatizo na marekebisho hayo.

Kifungu cha 4	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5	Uanzishwaji na Muundo wa Baraza
Kifungu cha 6	Uwezo na Kazi za Baraza

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba tufanye marekebisho kadhaa ya lugha katika kifungu cha 6, nianze na pale mwanzo kifungu cha 6(1) nilikuwa napendekeza mwisho kabisa kwenye neno ‘malengo’ tuongeze neno ‘yaliyotajwa’. Kwa sababu katika Kiingereza imezungumzwa *stated goals*. Kwa hivyo, nilikuwa naomba liongezwe neno hilo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, si niendelee tu kutaja haya marekebisho kwa pamoja au nitaje moja baada ya moja? Kwa sababu yote yamo katika kifungu hiki cha 6.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, labda taarifa kwanza, Mhe. Mjumbe alikuwa anazungumzia hiki kifungu cha sita marekebisho yake ayafanye yote kwa pamoja halafu ndio tuamue au aende moja baada ya moja?

Mhe. Mwenyekiti: Afanye yote halafu tuamue.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo yako. Kwa hivyo, nasema moja lilikuwa ni hilo kuongeza neno ‘yaliyotajwa’. Lakini pili katika kijifungu kidogo cha (2)(a) mwisho wa mstari pametumika neno ‘maliasili’ si neno sahihi, neno lililotumika katika Kiingereza ni *resources* (rasilimali). Kwa hivyo, nilikuwa naomba pia hilo sio kuhakikisha upatikanaji wa mgawanyo unaolingana wa mali asili tukianza kugawana malialisi itakuwa hatari Mhe. Mwenyekiti, ni wa rasilimali.

Halafu kifungu kinachofuata cha (b) ukisoma kwa Kiingereza imesemwa, *“monitor progressive realisation of right to food as specified in this Act”*. Sasa

Kiswahili imetafsiriwa kufuatilia maendeleo ya upatikanaji. Naomba ili lisomeke vizuri kwa lugha yetu sisi watu wa pwani ya kuakisi kisawa sawa ile dhamira ya Kiingereza naona hata umeme unakubaliana na mimi kwamba isomeke kama ifuatavyo:

'Kufuatilia ufikiwaji wa hatua kwa hatua kwa upatikanaji wa haki ya chakula kama ilivyoainishwa ndani ya sheria hii.

Mwisho kabisa katika kifungu hiki Mhe, Mwenyekiti kifungu cha (d) kuhakikisha uwajibikaji nadhani sio 'kwa', wa wizara, hatutaki kusema Kiingereza hapa kinachozungumzwa ni uwajibikaji wa wizara yenyewe. Ni *of* sio *to*. Kwa hivyo, nadhani hilo neno 'kwa' ukiliacha linabadilisha kabisa maana. Kwa hivyo, naomba tukisome kuhakikisha uwajibikaji wa wizara husika katika uetekelezaji wa sheria hii. Hiyo kama ni moja ya majukumu ya Baraza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimeutizama ule mswada wa lugha ya Kiingereza si mtaalamu wa lugha ya Kiswahili, lakini baada ya maelezo ya Mhe. Mjumbe yanaingia maanani. Kwa hivyo, sina sababu ya kumkatalia *unless* Mwanasheria Mkuu awe na maneno mengineyo, lakini kwangu mimi ambaye si mtaalamu wa lugha ya Kishwahili na baada ya kuupitia ule wa Kiingereza naona haya ni mambo ya msingi na ninakubaliana na Mhe. Mjumbe.

Kifungu cha 6 Uwezo na kazi ya Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 7 Mikutano ya Baraza
Kifungu cha 8 Sekreterieti ya Baraza

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Waziri alitaja kukubaliana na mapendekezo tuliyoyatoa mimi na wenzangu. Sasa naomba atusaidie ili tujue tunapitisha nini kwamba, tulikuwa na *concern* hii ya kuwa hii idara iki-*act* kama ni seketerieti inaongezwa na Katibu Mkuu lakini huku inaongozwa na Mkurugenzi. Kwa hivyo, naomba kidogo atuwekee sawa tunakubaliana nini hapa hilo alilolikubali ili tujue tumepitisha nini. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa sioni kwa nini wajumbe wawe na *concern* hiyo. Kwa maana kamati tendaji yenyewe itakuwa inashauri idara katika masuala ya uhakika wa chakula na lishe tu, haina kazi nyengineyo. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe hili lisiwe suala la kuwapa tabu kwa maana ushauri wao unajikita zaidi katika masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda nimsaidie tu kama nimemfahamu vizuri Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wengine walisema kwamba kifungu hichi kuweka idara halafu ukasema inaongozwa na Katibu Mkuu si sahihi. Mhe. Naibu Spika, mimi napendekeza kwamba labda kisomeke kiwe namba 8 "Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza itakayoongozwa na Katibu Mkuu". Labda kisomeke hivyo nadhani huo utata utaondoka.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika.

Kifungu cha 8 Sekretarieti ya Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 9

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 9 naomba tufanye marekebisho ya lugha kwa sababu naelewa kuna wenzetu huwa wanapata tabu katika kutafsiri lugha za kisheria katika Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 9 © kinasema *"make arrangements for periodical evaluation of the policy and programmes implementation in relation to the functions of the Council."*

Mhe. Mwenyekiti, hapa imeandikwa kufanya maandalizi ya tathmini ya vipindi sio sahihi kabisa. Sasa nilikuwa naomba tuweke kwa Kiswahili isomeke kwamba: Kuweka utaratibu kwa ajili ya kufanya tathmini ya vipindi ya utekelezaji wa sera na iendelee mpaka mwisho wake"

Mhe. Mwenyekiti, kifungu (d) ndio naona kimevurugwa kabisa. Kiingereza kinasema: *"on behalf of the Council, establish and maintain relationships with international, national and local institutions that have the responsibility for addressing food security and nutrition matters."*

Mhe. Mwenyekiti, ni *institution* tunazungumzia sio uhusiano wa kimataifa. Sasa hapa imeandikwa "Kuanzisha na kuendeleza kwenye Mabaraza uhusiano wa kimataifa, kitaifa na taasisi za kijamii". Hili neno kijamii halimo kabisa humu katika Kiingereza. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kisomeke "Kuanzisha na kuendeleza kwenye Mabaraza uhusiano na taasisi za kimataifa, kitaifa na za ndani ambazo zina majukumu ya kushughulikia uhakika wa chakula na lishe".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu (e) pale tumalizie "Kufanya jambo jengine lolote ambalo ni muhimu katika utekelezaji wa kazi za Baraza". Kwa hiyo, neno "wa" linakosekana pale.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo yote matatu ya Mwanasheria aliyebobea katika lugha ya Kiswahili Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Kifungu cha 9 — Kazi za Sekretarieti ya Baraza pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wa kipindi chetu cha asubuhi unakaribia kumalizika na kazi hatujamaliza. Namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais aweke utaratibu ili tumalize shughuli yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, naliomba Baraza lako tukufu liridhie kuongeza muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Kifungu cha 10 — Kuanzishwa na Muundo wa Kamati Tendaji.
Kifungu cha 11

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naona mapungufu mengine madogo madogo lakini nayaachia. Hasa nazungumzia kifungu cha 11 (f) nadhani kidogo tukirekebishe vizuri ili kiendane na ile dhamira ambayo imo katika mswada.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 (f) kwa Kiingereza kinasema *"promote efficient allocation and utilization of resources for the achievement of policy goals and targets and provide guidance on resource mobilization."*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna moja niliseme hapa ili nisirejee tena huko mbele. Kuna neno limetumika kila pahala humu kutafsiri *resources* kwamba ni nyenzo. Sasa sisi tumezoea *resources* kama ni rasilimali na ndio maana tuna *human resources* tunaita rasilimali watu. Kwa hivyo, kidogo nilikuwa naomba kama tutakubaliana neno *resources* maana yake ni rasilimali basi kote katika mswada palipotumika *resources* isomeke rasilimali.

Lakini hapa mbali ya hilo katika lugha nilikuwa naomba tukirekebishe kifungu (f) kwa Kiswahili kisomeke "Kukuza upangaji na utumiaji mzuri wa rasilimali katika kufikia malengo na shabaha za sera na kutoa muongozo juu ya uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali". Yale maneno "na walengwa" tuyaondoe. Nafikiri wametafsiri *target* kwamba ni walengwa wakati *target* ni zile shabaha za sera.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, hili suala la nyenzo popote linapokuja kwenye mswada wangu kuwa rasilimali sina tatizo nalo, lakini pale tu ambapo haitoondosha mantiki ya mswada wenyewe. Kwa hivyo, hilo ni suala la Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria wa Baraza kuliweka sawa. Hili pendekezo lake la kifungu (f) na mimi nimeupitia tena mswada wa Kiingereza na sina tatizo na maoni ya Mhe. Mjumbe.

Kifungu cha 11 Uwezo na Kazi za Kamati Tendaji pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 12

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 naomba kufanya marekebisho yafuatayo. Kwanza kifungu kidogo cha (3) "Akidi ya mkutano wowote wa Kamati Tendaji utakuwa nusu ya wajumbe wote". Mimi naomba nipendekeze isomeke "utakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote".

Lakini vile vile kifungu kidogo cha (4) neno la mwisho upendeleo ni uamuzi. Yaani "Maamuzi ya Kamati Tendaji yatafanywa na idadi kubwa ya wajumbe waliohudhuria; na ikitokea kuwa na idadi sawa ya kura, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi".

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 12 (3) "Akidi ya mkutano wowote wa Kamati Tendaji utakuwa nusu ya wajumbe wote" sioni kwa nini Mhe. Mjumbe ana tatizo na hapo. Kwani kuwa nusu ina tatizo gani, yeye anataka iwe zaidi ya nusu. Sasa kama nilivyosema mimi si mtaalam wa lugha ya Kiswahili lakini lengo la wizara hasa ni kuhakikisha kwamba ile akidi wakitimia nusu basi ndio *quorum* imetimia hapa. Hili suala la uamuzi badala ya neno upendeleo sina tatizo nalo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani mimi sina matatizo tukisema zaidi ya nusu. Kwa hiyo, tuweke zaidi ya nusu.

Kifungu cha 12	Mikutano na Akidi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13	Kuanzishwa kwa Idara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 14	Kazi za Idara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 15	Mkurugenzi.
Kifungu cha 16	Uwezo na Kazi za Mkurugenzi.
Kifungu cha 17	Kamati ya Uongozi wa Wilaya na Muundo wake.
Kifungu cha 18	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia mswada nilipendekeza hili na Mhe. Waziri alikubaliana na mimi. Kwa hivyo *just* nalirejea katika kuweka *record* kama alivyosema mwenyewe kwamba aliponiomba nisaidie katika hichi kifungu kuweka sawa yale ambayo nimeyarekebisha. Nilikuwa napendekeza kifungu cha 18 (2) © ili kutafsiri sawa sawa ile dhamira ya Kiingereza kama nilivyosema pia isomeke "Kuhakikisha uainishaji sahihi wa watu wenye sifa za kunufaika na miradi na kuhakikisha vigezo sahihi vya kuwatambua wanaofaa vinazingatiwa". Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio mapendekezo yangu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Mhe. Mjumbe kwa vile nilikuwa tayari nimeshamkubalia wakati najumuisha.

Kifungu cha 18	Kazi za Kamati ya Uongozi wa Wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 19	Utayarishaji wa Mipango ya Kazi za Uhakika wa Chakula na Lishe pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20	Majukumu ya Serikali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 21	Wajibu wa Kila Wizara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22	Wajibu wa Mkuu wa Kaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango nililigusia suala hili na nashukuru kimsingi Mhe. Waziri alikubaliana na hoja yangu lakini nilikuwa naomba kwa sababu tunaweka vizuri hapa kumbukumbu huko mbele.

Nilisihi katika maelezo yake kidogo hakunielewa vizuri lakini asingekubaliana na mimi. Yeye alizungumza kuondoa katika ile sehemu ya makosa na adhabu yale masharti ya kifungu cha 22 na akapendekeza nikubaliane nae kwa kuongeza maneno kwamba "akifanya hivyo kwa makusudi".

Sina tatizo na hilo, lakini katika maelezo yake alionekana kama vile ana-*refer* kwamba ni suala la Mkuu wa Kaya kuzuia watu labda wasilime kwa kilimo cha kujitosheleza. Lakini naomba tuweke rekodi sawa tu hapo tuelewane tunapitisha nini.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 22 kinasema "Wajibu wa Mkuu wa Kaya katika upatikanaji chakula kilicho salama, chenye virutubisho na cha kutosha itakuwa ni:

(a) kutoa chakula kwa watu wote wa kaya; na
(b) kufanya kazi yenye maslahi ili kupata chakula cha kutosha kwa watu wote wa kaya kwa kutumia juhudi ambazo zinaheshimu utu wa mtu na utawala wa sheria".

Sasa kifungu cha 23 Mhe. Mwenyekiti, kinasema "Mtu au Afisa atakayekiuka sharti lolote la vifungu vya 20, 21 na 22 vya sheria hii". Ndio kusema kwamba Mkuu wa Kaya ikiwa yeye mwenyewe atashindwa kutoa chakula kwa watu wake wote wa kaya au atashindwa kufanya kazi yenye maslahi ili kupata chakula atakuwa katenda kosa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alikubali lakini katika maelezo yake ilionekana kama vile alikuwa ana-*refer* kwamba ikiwa Mkuu wa Kaya atazuia watu wake au wanafamilia yake au wanakaya yake wasilime kwa kujitosheleza kwa chakula.

Lakini *issue* hapa ni yeye mwenyewe yule Mkuu wa Kaya kwamba akishindwa kufanya haya mawili kutoa chakula kwa watu wote na kufanya kazi yenye maslahi anakuwa ametenda kosa. Ndio nikasema tuelewane vizuri ili tuweke rekodi zetu vizuri.

Mimi nilipendekeza kwamba kifungu hichi cha 23 hii *reference* iliyosomeka 22 tuiondoe kwamba huu ubakie kuwa ni wajibu wa Mkuu wa Kaya lakini tusiweke sharti kwamba ukiwa umevunja hukutekeleza hili itakuwa ni kosa la jinai na unaweza kushtakiwa na kufungwa hata kupigwa faini. Kwa sababu kama nilivyosema mazingira yetu ya kiuchumi bado hayajaifanya serikali yenyewe kumhakikishia kila mwananchi kwamba anaweza kuleta chakula lakini pili ya kumpatia kazi yenye maslahi kila mmoja wetu. Ikiwa sisi hatuja-*create* mazingira hayo naona si sahihi kuweka kifungu cha kumtia makosani mtu ambaye atakuwa ameshindwa kuyatekeleza hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atukubalie kwamba hii *reference* ya kifungu cha 22 tuiondoe hapa kwenye kifungu cha 23 *unless* Mwanasheria Mkuu labda atusaidie kwamba tuiweke katika lugha gani ambayo itakidhi yote mawili, ile *concern* yangu na ile haja ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba meza yako ikupe muongozo katika kifungu cha 84 (10) cha Kanuni za Baraza. Kwa sababu ninavyofahamu ni kwamba haya anayozungumza Mhe. Mjumbe ni maelezo ambayo anataka tubadilishe huu mswada kwa baadhi ya mambo. Ikiwa ni hivyo Mhe. Mjumbe anaruhusiwa kufanya hivyo wakati wa kuchangia.

Wakati wa kuchangia Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu: "Mara tu baada ya Mswada wa Serikali kusomwa mara ya kwanza, Mjumbe yeyote anaweza kuinuka na kutoa taarifa yam domo kwamba anakusudia kuleta hoja ya mabadiliko kwenye mswada huo wakati wa Kamati ya Baraza Zima. Iwapo Mjumbe anatoa taarifa kama hiyo atataja kile kifungu cha mswada huo kinachokusudiwa."

Kwa hivyo, haya yanayozungumzwa hivi sasa ni nje ya yale mazungumzo ambayo yamezungumzwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi tunakwenda kinyume na kanuni na naomba twende kwa mujibu wa kanuni. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naheshimu ufafanuzi alioutoa Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Lakini katika mchango wangu wakati naujadili huu mswada nilikigusia kifungu hichi na ndio maana katika majibu ya waziri na yeye pia alikigusia. Nilichokuwa nakizungumza mimi hapa ni kwamba katika majibu ya waziri inaonekana hakunielewa ule msingi wangu wa nilichokuwa nakipinga. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Abubakar arejee katika maelezo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu ndani ya Baraza nilikigusia kifungu hichi na nilitoa hoja hii hii kwamba *reference* ya kifungu cha 22 katika kifungu hichi iondolewe.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi kabisa Mhe. Mjumbe wakati anachangia kifungu hichi alikigusia na alitumia katika vifungu *serious* kabisa anavyotaka kuvichangia. Mimi kimsingi nikubaliana nae sikuona haja Mkuu wa Kaya kumuwekea adhabu atakaposhindwa kufanya yale yaliyozungumzwa ambayo yeye sasa hivi anayakariri. Lakini nilimwambia lengo la wizara yangu ili tuondokane na uzembe kwa sababu kama Sera yetu ya Uhakika wa Chakula na Lishe inavyozungumzia mwaka 2008 na hasa tunavyozungumzia kwenye mswada kazi ya kujipatia chakula mwananchi ni

yake mwenyewe kwa njia za kihalali na Wakuu wa Kaya humu wamepewa majukumu.

Sasa huyu ikiwa atachangia lengo lilikuwa ni hilo. Kama atachangia katika kuzuia wanakaya wake kujishughulisha na kujipatia chakula kwa njia ya halali basi adhabu hii ndio imfike. Nikaomba sasa Mwanasheria Mkuu atusaidie kutuwekea lugha ambayo itaweza kukidhi mahitaji ya Mhe. Mjumbe. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali atusaidie kutuwekea lugha hili la adhabu liwepo lakini pia kukidhi matumaini na haja ya Mhe. Mjumbe mimi sina tatizo nalo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri pale katika kujibu hoja alikuwa amezungumzia kwamba kwa makusudi. Kwa hivyo, nimejaribu tu kukiandika hichi kifungu labda kisomeke hivi: "Mtu au Afisa atakayekiuka sharti lolote la vifungu vya 20, 21 na 22 vya sheria hii kwa makusudi atakuwa amefanya kosa".

Kifungu cha 23 Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 24 katika Kiswahili hakikukamilishwa naomba tuongezee maneno pale mwisho ili kiende kama kilivyokusudiwa. Kinasema "Mtu yeyote ambaye bila ya ruhusa chini ya sheria hii:

(a) kwa makusudi anatoa taarifa za uongo zisizo sahihi ambazo zinakwamisha utekelezaji wa shughuli za uhakika wa chakula na lishe.

(b) anaathiri upatikanaji wa haki ya chakula au;

(c) anakwamisha au kumzuia Afisa Uhakika wa Chakula na Lishe katika utekelezaji wa kazi zake."

Kwa hiyo, atakuwa kafanya nini haisemi. Lakini Kiingereza inasema kwamba atakuwa ametenda kosa. Sasa yako yale maelezo katika kile kifungu cha juu pale inapaswa yajirejee hapa kwamba imalizie "atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu au adhabu zote mbili faini na kifungo". Hivyo ndivyo ilivyo katika mswada wa Kiingereza Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo hayo yaongezwe vile vile.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tukitazama katika marekebisho ya kamati hilo limefanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, pale kuna kifungu 20, 21, 22 na 24 katika kile cha 23 kwa taarifa niliyokuwanayo mimi. Sasa hilo ninalolizungumza ni la msingi na kama halimo basi hapo kiongezewe hicho kifungu namba 24.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri nataka kumpa taarifa tu kwamba hayo niliyoyataja hayakuwamo niliangalia marekebisho ya kamati. Kamati ilichofanya ni marekebisho ya neno la pembeni tu badala ya kuwa Afisa lisomeke Ofisa. Haya niliyoyasema mimi yalikuwa hayamo ndio maana nikaomba kwamba yaingizwe.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali.

Kifungu cha 24	Taarifa za Uongo na Kumzuia Ofisa kufanya Kazi zake pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25	Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula.
Kifungu cha 26	Dharura ya Chakula na Utambuzi wa Makundi Hatarishi.
Kifungu cha 27	Fedha za Kugharamia Mipango Kazi ya Uhakika wa Chakula na Lishe.
Kifungu cha 28	Fedha za Kugharamia Hifadhi ya Taifa ya Chakula.
Kifungu cha 29	Mpango wa Bajeti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 30	Mgawanyo wa Hesabu na Matumizi.
Kifungu cha 31	Uwezo wa Kutunga Kanuni.
Kifungu cha 32	Kufutwa na Kubakiza.
Kifungu cha 33	Kupingana na Sheria Nyengine.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaoukubali mswada wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2011 Pamoja na Marekebisho Yake

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ya mwaka 2011 usomwe mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaounga mkono mswada kusomwa mara ya pili wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kukubaliwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kikao chetu mpaka jioni nina matangazo matatu. Tangazo la kwanza tunaarifiwa hapo nje tukitoka tu sasa hivi panafunguliwa maonesho ya wenzetu waliotupa semina jana kwa hiyo tunaambiwa sote tushiriki.

Lakini la pili kuna waheshimiwa wana matatizo ya vitambulisho vyao havijakamilika. Kwa hiyo, litakuwepo basi hapo nje sasa hivi mkitoka mtaingia na mtakwenda Ofisi ya Vitambulisho kwa marekebisho ili mpate vitambulisho vyenu.

La tatu tunaomba jioni tuje mapema ili tusome Mswada wa Watoto ambao ni muhimu sana.

Baada ya maelezo hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitisha mswada wetu huu ambao ni muhimu kwetu sote. Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao mpaka saa 11:00 za jioni.

(Saa 7:30 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Allah Subhanahu Wataala kwa kuweza kunisimamisha katika Baraza lako tukufu ili kuweza kutoa suala zima la mswada huu wa sheri uliopo mbele yetu.

Pili Mhe. Mwenyekiti, naomba nikupongeze kwa dhati kwa mara ya kwanza kukikalia kiti hicho. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuja kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Mswada wa Sheria ya Mtoto Zanzibar, utakaotoa utaratibu unaofaa wa kushughulikia masuala ya haki na ustawi wa watoto hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi pia kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mhe. Amina Iddi Mabrouk, pamoja na wajumbe wake wote. Mhe Mwenyekiti tumefanya kazi nzuri sana pamoja na kamati kuupitia mswada huu kifungu hadi kifungu, michango yao na marekebisho waliotoa yamesaidia sana kufanikisha mswada huu kufika hapa leo.

MADHUMUNI YA MSWADA

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa sheria ya watoto 2011, kunatokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto unaoendeleza hapa nchini. Aidha, sheria nyingi zinazohusiana na watoto zimesambaa katika sheria mbali mbali, hivyo inakuwa ni vigumu kuweza kushughulikia masuala ya haki za watoto kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unakusudia kuweka sheria moja ambayo inajitosheleza katika kuondoa matatizo ya kisheria yaliyopo hivi sasa na kuwawezesha wananchi kuona jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kushughulikia haki na ustawi wa watoto nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa ina viwango vya kimataifa kutokana na kuzingatiwa kwa mkataba wa umoja wa mataifa wa haki ya mtoto 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990 pamoja na Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2001.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu pia unalenga kuzifuta za mtoto zilizopo hivi sasa ambazo ni za zamani na hazitoshelezi na hazikidhi mahitaji ya ulinzi wa haki za watoto.
Sheria hizo ni:

(a) Sheria ya Watoto na Watoto Vijana, sura ya 58 ya mwaka 1952 na
(b) Sheria ya kuwasili, sura ya 55.

MUUNDO WA SHERIA

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla mswada huu wa sheria ya mtoto umegawika katika sehemu katika sehemu kuu 13 na ina jumla ya vifungu 139.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI WA SHERIA

Sehemu hii inajumuisha kifungu cha kwanza na cha pili, ambapo kifungu cha kwanza kinaeleza jina la sheria yenyewe pamoja na muda wa kuanza kutumika kwa sheria hiyo na kifungu cha pili kinatoa tafsiri na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yatakayotumika ndani ya sheria hiyo.

SEHEMU YA PILI
MASLAHI BORA

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya pili inajumla ya vifungu 14 ambavyo vinatoa haki za lazima za kupewa mtoto, kinga kwa watoto, majukumu ya wazazi kwa watoto, adhabu kwa watakaotenda kinyume na masharti yaliyowekwa, pamoja na kuweka majukumu ya jumla ya mtoto.

SEHEMU YA TATU
MAHAKAMA YA MTOTO

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya tatu ina kifungu kimoja ambacho kinaanzisha mahakama ya mtoto, kuweka mamlaka ya mahakama, uwezo wa mahakama, pamoja na utaratibu mzima wa kuendesha kesi za watoto na ukataji wa rufaa.

SEHEMU YA NNE
MATUNZO NA KINGA YA MTOTO

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya nne inazungumzia matunzo ya mtoto pamoja na kuweza kinga kwa mtoto. Sehemu hii inajumla ya vifungu 16 na kifungu cha 18 kimeweka orodha ambayo inafafanua jinsi ya kutambua mtoto ambae anahitaji matunzo na kinga, baadhi ya mambo hayo ni:

(i) Mtoto anaefanya kazi mitaani.
(ii) Mtoto aliye katika hali ya kutelekezwa kimwili na kiakili.
(iii) Mtoto yatima au aliyetupwa ambaye hana matunzo ya kutosha au msaada.
(iv) Mtoto aliyekuwa ameathirika kwa usafirishaji kwa watoto, na mambo mengi mengineyo ambayo yameorodheshwa katika kifungu hicho.

Sehemu hii ya nne pia imeweka jukumu la kutoa taarifa ya uvunjwaji wa haki za mtoto, kwenye kifungu cha 20 na kimeorodhesha wale ambao wanahitajika kutoa taarifa ya uvunjwaji wa haki za mtoto kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii, Polisi na Sheha.

SEHEMU YA TANO
WATOTO WALIO NA MATATIZO NA SHERIA

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya tano inazungumzia juu ya watoto walio na matatizo na sheria *(children in conflict with the law)* sehemu hii ina jumla ya vifungu 20 ambavyo vimegawika katika sehemu 6 kama ifuatavyo:

Sehemu ya kwanza, inazungumzia umri wa dhima jinai na uwamuzi wa umri.

Sehemu ya pili, inazungumzia utaratibu wa kuwakamata watoto na kuweka majukumu ya polisi.

Sehemu ya tatu, inaweka utaratibu wa kufanyiwa tathmini mtoto anayeshukiwa kufanya kosa na atafanyiwa tathmini hiyo na Afisa wa Ustawi wa Jamii kabla ya kumfikisha mtoto huyo mahakamani.

Sehemu ya nne, inaweka utaratibu kwa waendesha mashtaka kuangalia kosa lililotendwa na mtoto na kuweka utaratibu mwengine wa adhabu bila ya kumpeleka mtoto huyo mahakamani.

Sehemu ya tano, inaweka utaratibu wa jinsi ya kuendesha kesi za jinai zinazohusu watoto ambao watapelekwa kwenye mahakama ya watoto, na

Sehemu ya sita, inaweka masharti mengineyo ya jumla ambayo yanakataza uchapishaji wa taarifa za mtoto aliyefikishwa mahakamani, taarifa zinazokatazwa kuchapishwa ni jina la mtoto, anuani, skuli anayosoma, picha ya mtoto na kadhalika.

SEHEMU YA SITA
UZAZI, ULEZI NA MATUNZO YA MTOTO

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya sita ina jumla ya vifungu 17 ambavyo vinaweka utaratibu wa mambo yafuatayo:

(i) Ombi la kuwa Mzazi;
(ii) Uthibitisho wa mzazi;
(iii) Kipimo cha Daktari;
(iv) Matunzo ya mtoto;
(v) Ulezi wa mtoto;
(vi) Fursa ya kumuona mtoto aliye kwenye ulezi wa mtu mwengine;
(vii) Kumuondoa mtoto kinyume cha sheria; pamoja na mambo mengine mengi ambayo yameorodheshwa katika sehemu hii ya sita.

SEHEMU YA SABA
MATUNZO KUTOKA KWA WAZAZI WA KAMBO

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla sehemu hii ya saba inazungumzia malezi ya kambo *foster care* ambayo atapewa mtoto kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na vifungu vya sehemu hii. Inajumla ya vifungu 3 ambavyo vinaweka masharti kwa watu wanaoweza kulea na kuweka kanuni za matunzo kwa wazazi wa kambo yaani *foster parents*.

SEHEMU YA NANE
KUASILI

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya nane inazungumzia *adoption* ya watoto na pia inafuata sheria ya kuasili inayotumika sasa. Sehemu hii imegawika katika sehemu kuu 2.

Sehemu ya Kwanza, inazungumzia utaratibu wa ‘kafala’ utaratibu huu unaweka mazingira na masharti kwa waumini wa dini ya Kiislamu kufanya kafala.

Uwamuzi wa kuweka sehemu hii umekuja baada ya wataalamu kupokea mapendekezo kutoka kwa wadau ambao walisisitiza na kupendekeza, kuwa waumini wa dini ya Kiislamu kwa mujibu wa sheria za dini hawaruhusiwi kuasili watoto, kwani kumfanya hivyo ni kumfanya matoto huyo kutumia jina la baba na pia pale baba huyo atapofariki mtoto huyo atakuwa na haki sawa ya kurithi mali ya baba huyo kama vile ambavyo wanarithi watoto waliozaliwa na baba huyo. Hivyo, sehemu hii imeweka utaratibu kwa wale waumini wa dini ya Kiislamu ambao watakuwa na haja ya kufanya kafala kwa watoto.

Sehemu ya pili, inaweka utaratibu wa kufanya *adoption* kwa wale wote ambao sio waumini wa dini ya Kiislamu na inatoa uwezo kwa Mahakama Mkuu, kutoa amri ya kuasili, inaweka utaratibu wa kufanya maombi, ridhaa ya wazazi na masharti mengine ya jumla.

SEHEMU YA TISA
HATUA MAALUM ZA KINGA KWA MTOTO

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya tisa ina jumla ya vifungu 14 ambavyo vinaweka hatua maalum za kinga za watoto kwenye maeneo yafuatayo:

(i) Ajira ya mtoto;
(ii) Kinga kwa mtoto anapofanyishwa kazi;
(iii) Kinga kwa ajira mbaya kwa watoto;
(iv) Kinga ya ngono kwa watoto;

SEHEMU YA KUMI
RIDHAA YA UTABIBU WA KIDAKTARI NA UPIMAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya kumi inaweka masharti ya kupatikana kwa ridhaa ya mtoto endapo atahitajika kufanyiwa operesheni ya upasuaji au akihitajika kupima virusi vya ukimwi. Sehemu hii imeweka umri wa mtoto kuanzia miaka 16 au zaidi endapo atahitajika kufanya upasuaji au kupima virusi vya ukimwi, itahitajika kupatikana ridhaa yake.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
SKULI YA MAREKEBISHO (SKULI YA MANUNDA)

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya kumi na moja, inazungumzia kuanzishwa kwa skuli ya marekebisho na kufanya uteuzi wa wajumbe wa bodi wa wakaguzi wa skuli ambazo zitaanzishwa, pamoja na kuweka masharti ya kumuezesha waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa madhumuni ya kuanzishwa

kwa skuli hizo. Sehemu hii pia inakusudia kufuta sheria iliopo sasa yaani *Approved School decree Cap 59*.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
UANZISHWAJI WA MAKAAZI NA MATUNZO YA KUTWA

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya kumi na mbili inaanzisha makaazi na vituo vya matunzo ya kutwa ya mtoto, inajumla ya vifungu kumi na mbili ambavyo vinaweka masharti ya kuanzishwa kwa vituo hivyo, utaratibu wa kupokea watoto, ukaguzi wa vituo, maombi ya kuanzisha kituo, ufutaji wa leseni, pamoja na kuweka adhabu kwa makosa yatakayofanywa na mtu anayeendesha vituo au nyumba za makaazi ya watoto.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
MAMBO MENGINEYO

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya kumi na tatu na ya mwisho ya rasimu hii ya sheria ya mtoto, kama ilivyo kawaida inazungumzia mambo mengine ya jumla ambayo ni;

(i) Uwezo wa Mhe. Waziri kutengeneza kanuni.
(ii) Utaratibu wa rufaa kwa mtu ambaye atakuwa hakuridhika na uamuzi wa waziri.
(iii) Kufuta sheria na kubakia baadhi ya vifungu vya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, natumai Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watakuwa wamepata muda wa kutosha wa kupitia mswada huu wa sheria ya mtoto, ili waweze kuuchangia. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe mswada huu wauchangie kwa makini na kwa manufaa ya watoto wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAPENDEKEZO YA MSWADA WA SHERIA YA MTOTO ITAKAYOTOA HAKI NA MASLAHI BORA YA MTOTO,

ITAKAYOSHUGHULIKIAWATOTO NA MATATIZO NA SHERIA, ULEZI, UKAAJI, KUMUONA NA KUMTUNZA MTOTO, KUASILI, HATUA MAALUM ZA KINGA KUHUSIANA NA MTOTO, RIDHAA YA UTABIBU WA KIDAKTARI, ITAKAYOANZISHWA SKULI ZA

MAREKEBISHO, MAKAAZI NA MATUNZO YA KUTWA, ITAKAYOREKEBISHA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI NA KUSAHIHISHA SHERIA ZINAZOHUSIANA NA MAMBO HAYO

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma hotuba yangu, nichukuwe nafasi hii kwa dhati kabisa kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti, ukiwa mwanamke mwenzangu kwa kukalia kiti hicho, ukiwa Mwenyekiti wa Baraza. Matarajio yangu ni kwamba umeanzia na umwenyekiti, na utaishia na uspika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii nikiwa mzima wa afya ili kuweza kuwasilisha mchango wa kamati yetu kuhusu Mswada wa Sheria ya Mtoto, itakayotoa haki na maslahi bora ya mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, shukrani zangu ziwafikie wajumbe wa kamati na watendaji wote wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto kwa mashirikiano ya kutosha wakati wa kuuupitia na kuuchangia mswada huo. Napenda kusema kwa niaba ya Kamati tunawashukuru kwa dhati watendaji hao.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa pia kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na Wanasheria wetu wa Baraza kwa kutoa mchango wao kwa kutupa muungozo na ufafanuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema kukutambulisha kwa kuwataja wajumbe 10 wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambao walihusika katika kuupitia Mswada wa Sheria ya Mtoto itakayotoa haki na maslahi bora ya mtoto.Wajumbe hao ni:-

1.	Mhe.Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2.	Mhe Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe.Asha Abdu Haji	Mjumbe
4.	Mhe Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6.	Mhe Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mhe Nassor Salim Ali	Mjumbe
8.	Mhe Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9.	Nd. Shemsa Maabad Mohamed	Katibu

10. Nd. Talib Enzi Talib Katibu

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa niende katika mswada husika .

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa Sheria unaokusudia kutoa haki na maslahi bora ya mtoto, utakaoshughulikia pamoja na mambo mengine ulezi, ukaaji, kumuona na kumtunza mtoto, kuasili, hatua maalum za kinga kuhusiana na mtoto, ridhaa ya utabibu wa kidaktari, uanzishwaji wa skuli za marekebisho, makaazi na matunzo ya kutwa, kurekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Kusahihisha Sheria Zinazohusiana na mambo hayo. Kwa kweli umezingatia maeneo hayo yote muhimu ambayo yatasadia kulinda haki za mtoto nchini. Wakati umefika kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa haki na maslahi bora ya mtoto yanalindwa na kusimamiwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nyingi zinazohusiana na masuala ya haki za mtoto ambazo zimeonekana kusambaa katika sheria mbali mbali, zimekuwa zikileta ugumu katika kushughulikia masuala ya watoto, na kwamba urasimu huo pamoja na mambo mengine unapelekea kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto unaoendelea siku hadi siku.

Hivyo Kamati inasisitiza kuwa baada ya kupitishwa kwa sheria mpya, kuna haja kwa serikali na vyombo vyengine vya kisheria kuhakikisha kuwa urasimu huo unaondoka, ili kurahisisha usimamiaji wa haki na maslahi bora kwa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi kamati imekubaliana na mapendekezo ya rasimu ya Mswada, hata hivyo imefanya baadhi ya marekebisho madogo madogo ya kimaandishi, pamoja na kukirekebisha kifungu cha 68(1)(c) ambacho kinahusu kumalizika muda kwa amri ya matunzo.

Kamati imeona ni vyema amri ya matunzo itakayotolewa na Mahkama, imalizike muda wake ikiwa mtoto mwanamke atakapoolewa na ndoa yake ikadumu hadi atakapofikia umri wa miaka 18.

Mhe. Mwenyekiti, aidha katika kifungu cha 124(2) ambacho kinatoa uwezo kwa Mhe Waziri kukasimu madaraka yake kwa lengo la utekelezaji mzuri wa majukumu, Kamati imeshauri kuwa uwezo huo wa kukasimu madaraka aliopewa Mhe. Waziri utumike vizuri kupitia taasisi au vyombo mbali mbali vilivyoanzishwa ndani ya Sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Mtoto ni muhimu katika kuhakikisha maslahi na haki zao zinalindwa. Hivyo nachukua fursa hii kuwaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kuuchangia ipasavyo, ili malengo hayo yaweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo basi, naomba nichukuwe nafasi hii kuwasilisha rasmi hotuba yangu, ahsante.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na uzima na afya, kwa kuweza kufika kwenye kikao chetu kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa leo kuanza siku yako ya mwanzo kukalia kiti hicho, Inshaallah Mwenyezi Mungu atakuwezesha kufanikisha kazi hiyo kwa wepesi.*(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kutoa mchango wangu katika mswada huu muhimu, mzito na mgumu uliokuwa mbele yetu wa kuweka matunzo kwa watoto watu. Nasema kuwa ni mswada mzito na ambao umegusa pia sheria za Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, jambo lolote linaloingilia na sheria za Mwenyezi Mungu basi linakuwa zito, kwa sababu sheria ya Mwenyezi Mungu haitaki kukisiwa wala kuendewa kombo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ile sehemu ya tafsiri ya mtoto. Juzi katika semina Sheikh Soraga alitoa ufafanuzi mzuri wa tafsiri ya mtoto. Mimi nadhani nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu wanasema kwamba huu mswada waliwashirikisha na Masheikh, lakini tafsiri aliyoitoa Sheikh Soraga juzi ni tafsiri tosha ambayo ilitutosha kuelewa kuwa ile ni tafsiri ya mtoto na ndio maana tunayoifahamu.

Mtoto ni yule ambaye bado hajaandikiwa dhambi. Siku unayobaleghe tu, basi Malaika wanaanza kukukabidhi kitabu chako, utakalolifanya hata liwe na uzito wa mdudu chungu liwe ovu basi linaandikwa katika kitabu chako, basi hapo utakuwa sio mtoto tena, unajua hili jema na hili baya. Labda iwe vyenginevyo imetokezea maradhi ya taathira basi hapo utakuwa huendelei kuandikiwa dhambi, lakini ukiwa una akili timamu, siku utakayopata kubaleghe ndio siku utakayokabidhiwa kitabu chako kwa mujibu wa kuitwa hapo sasa sio mtoto tena ni mtu mzima. Kama ni mwanamke anaweza kuolewa akapata mtoto na kama ni mwanamme anaweza akaowa akapata mtoto.

Kwa hivyo, kutokana na tafsiri hii bado ninamuomba Mhe. Waziri ikaenda kufanyiwa tena utafiti tukapata tafsi ambayo inalingana kwa mujibu wa sheria ya dini yetu. Kwa sababu huyu mtoto ana kiasi chake na matu mzima akifika

kiwango chake anaitwa mtu mzima. Akifika miaka 18 mimi nadhani huyu tayari kuitwa mtu mzima, miaka 16 au 17 tayari kuwa mtu mzima wakati keshabaleghe. Kwa hivyo, bado kwa mujibu wa sheria hii na tafsiri hii, mimi naona bado haijatosheleza. Namuomba Mhe. Waziri wakakae tena tuipe haki yake tafsiri ya mtoto.

Mhe. Waziri, mimi naweza kusema kwamba ile sheria ya mtoto ukiiweka hapa bado mtoto wa miaka 16 ni mtoto huyu. Mimi nasema kuna watoto wa miaka 12 ndio huyo tunayesema keshabaleghe basi anakushinda wewe mtu mzima. Juzi Mhe. Zahra Ali Hamad Naibu Waziri, alitoa mfano akasema kwamba kuna watoto wamekwenda kwenye wizara yake ambao wanataka kuolewa, wapo mitaani watoto kama hawa Mhe. Waziri na wazee wao wameshajitahidi kuwasomesha na wameshakata tamaa.

Kwa hivyo, mimi nadhani hii sheria tuitizameni vizuri, kwa sababu tunaweza tukabeba majukumu kwa Mwenyezi Mungu. Mtoto anayetaka kusoma mzee anamjua yeye mwenyewe na anamsomesha. Mtoto asiyetaka kusoma huna la kumfanya hataki tu kusoma na atakushinda mzazi, umfanye nini ni kumpa mume tu ili upate wajukuu, lakini mwisho watoto watatufikisha mbali tutashindwa la kwenda kujibu kesho siku ya kiyama. Mhe. Mwenyekiti, tunapotunga sheria lazima tujitahidi tusichupe mipaka sana na sheria za Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwenye ukurasa wa 162 naomba nitoe wasi wasi wangu. Kwa kweli hapa nimepatwa na wasiwasi mkubwa katika kifungu cha 77 kuhusu ombi la kuasili najua sheria hii inawagusa wenzetu ambao wenye dini nyengine.

Vile vile kwenye kifungu cha 78 kuhusu ridhaa ya wazazi na walezi amri ya kuasili itatolewa tu ikiwa ridhaa ya wazazi au walezi wa mtoto anayeasiliwa. Kwa kweli nakubali kwamba hii ni sheria ya upande wa dini ya wenzetu, isipokuwa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti nanitoe wasiwasi wangu.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa mwanamke ameolewa na mwanamme ambaye dini ya upande mwengine na haya ni mambo ya kawaida siku hizi. Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria hii ilivyoandikwa basi hao watoto wetu anamtafuta anayempenda yeye mwenyewe, mzee ukikubali kumuozesha sasa akikataa basi anakwenda kujiozesha uko na anapofika huko anasema kwamba amesilimu na mke anamtaka.

Kutokana na hali hiyo, Sheria ya Mahakama ya Kadhi inafuata utaratibu na kumuozesha, baada ya kumuozesha anakuja nyumba na kukaa baadaye kupata

watoto. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu anasema "*Kullu Mauludun yuuladu alafitrati llislam*", yaani kila kinachozaliwa chochote basi kitazaliwa katika umbile la Kiislam.

Kwa hivyo, hapa nina wasiwasi, kwa sababu kila kinachozaliwa basi kimezaliwa katika umbo la Kiislamu ikiwa baba Majusi na mama awe nani, lakini pale kinachozaliwa na hii ni sheria ya mtoto, basi huyu mtoto anayezaliwa pale atakuwa Muislamu.

Je, Mhe. Waziri katika hali kama hii upande huu mwanamke Muislamu na baba upande mwengine na tayari wameshaoana na kupata watoto, lakini wamekwenda katika serikali na kuozeshwa na kukaa pamoja.

Sasa sheria hii baada ya muda yule amemkimbia na wala hakukaa naye na hayo yanatokea itakuwa vipi sheria hii hapa, wakati tukisema huyu ni mtoto. Kwa hivyo, atakapokuwa baleghe mtoto yule sheria inamtaka hapo anaweza kutoa maamuzi kwa mujibu wa sheria tu ama atakwenda kwa baba yake ikiwa Mmajusi au kwa mama yake akiwa Muislamu.

Je, kwa sheria hii kwa hapa tuko vipi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie ufafanuzi juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu ni kwamba mswada huu wa sheria lengo lake ni kumlinda mtoto kutokana na madhila mbali mbali, nasema ni mswada mzuri na umekuja wakati muafaka. Kwa kweli watoto wetu wanapata madhila makubwa hususan mtoto anapoondokewa na baba yake, wakati anapoondokewa na baba yake mtoto yule tunamwita yatima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda sana kusikiliza *cassette* na siku moja nilihudhuria kwenye Ijitimai ya Pemba nadhani ilikuwa ni mara ya kwanza, basi yalitolewa mawaidha kuhusu mtoto yatima ambaye alikuwa akilelewa na baba yake mdogo na mali yote alikula baba yule. Kwa kweli mtoto analia anamwambia baba yule kwamba nataka kusoma, alimwambia amfuate kabirini, baba naumwa nahitaji kutibiwa, anaambiwa baba yako wala mama yako hawapo wafuate kabirini, tulilia sote Mhe. Mwenyekiti.

Kutokana na hali basi yule mtoto alikwenda kaburini na kukaa chini ya makaburi ya wazee wake na kulia pamoja na kusema baba umeniacha hivi nikiwa mkiwa sijui niende wapi. Kwa mujibu wa mswada wa sheria huu utatusaidia kutokana na madhila haya. Kwa kweli mswada huu ni mzuri, lakini tunga sheria ni jambo moja na suala la utekelezaji ni suala la pili, yaani hapa ndipo ninapopata mashaka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tutunge sheria lakini naomba sheria hii iwe na utekelezaji wake, kwa sababu sheria nyingi zipo lakini utekelezaji haupo. Kwa maana hiyo, ni vyema tuone kwamba sheria ambayo tumeitunga kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu basi ifanyekazi kweli, kwani watoto wanapata idhilali wanadhalilishwa, yaani uzalilishwaji wa watoto jambo ambalo ni zito hasa kama mimi ni mwanamke.

Kwa mfano, ukienda huku mtoto amebakwa mara amefanya nini na unaulizwa je Mhe. Mwakilishi hizi sheria hazifanyikazi hali iko vipi na hata juzi Mhe. Waziri alisema tufanye nini kwa hawa watu wenye kubaka.

Kwa hivyo, nadhani tukae na wala tusione aibu ikiwa sheria zetu hazifanyikazi basi tutafute Masheikh nini Mwenyezi Mungu amesema kwa watu hawa, yaani wafanywe nini watu hawa. Kwa kweli watu wameshatoka imani na watu hawa, nadhani siku moja niliwahi kusema kwamba itafika wakati watu watachukua sheria mikononi mwao.

Kwa mfano, mwizi hivi sasa tunasikia wanavyouliwa, hivi Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa sheria amesema mwizi auliwe, kwa kweli hakusema auliwe isipokuwa akatwe mkono. Sasa watu wanapomuona mwizi anaranda nje basi na yeye akimkuta anamuua. Kwa hivyo, na hili itafika wakati jinsi watoto wetu wanavyodhalilishwa, basi watu watachukua sheria mikononi mwao Mhe. Waziri, kwa sababu watu wameshachoka na hili.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mpandae mtoto wa kike anarudi skuli amebakwa, yaani ni mtoto mdogo, tena huyo mbakaji amemuharibu kwa nyuma mtoto wa miaka 6, mtoto yule analia tu. Sasa wazee wake wamekusanyika kama wanaolala matanga, yaani wanasema bora angeondoka tukajua mtoto wetu hayupo tumelala matanga, mtoto anapotaka kufanya haja anapiga kelele na kusema mama nakufa na yule mbakaji hakupatikana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, haya ni masuala ambayo Mhe. Waziri yanatuuma kama sisi wazazi. Kwa maana hiyo, tunaomba hizi sheria tukae na tuhakikishe kwamba sheria hii ya kufungwa mtu miaka 15 si kweli, yaani akifika jela anawekwa sehemu ya jikoni na wakati anapotolewa tumbo lake kama mlariba, kwa sababu hana dhiki.

Kwa kweli mtu anakwambia nimetoka jela, basi huamini kama ametoka jela, kwa sababu alikuwa jikoni anastarehe na sahani yangu niekeeni. Mhe. Waziri suala hili tulione. Mhe. Mwenyekiti, ninayo kumbukumbu hiyo kwamba kuna mtu alifungwa miaka 15 tena namjua ambaye alimbaka mtoto na kule jela

alikuwa amewekwa jikoni, basi anapika kama kuna supu au nini na baadaye anakula na kushiba na hata nyumba yake haitaki Mhe. Waziri.

Sasa ukimwambia aende kule nyumbani kwake akilikokuwa akibakia watoto kwenye kibanda chake cha mgongo basi hakutaki, yuko radhi akae pale wakati yuko jikoni anakula na kushiba. Kwa hivyo, atahisi ni bora maisha ya jela, wakati alipotoka tumbo lake kubwa sana utafikiri hakuwa jela.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tuone hali hii jinsi watoto wetu wanavyodhalilishwa, basi tuweke sheria zenye machungu, yaani yule mhalifu aone kwamba amepata machungu na Mwenyezi Mungu anasema kuwa watapata adhabu yenye kuumiza, basi waanze kuipata hapa kwa kweli tumeshachoka Mhe. Mwenyekiti. Kwa mfano, sisi tupo hapa lakini akili yote iko nyumbani kwamba yule mtoto wangu hajatoka nje, yaani utakuwa unawaza hilo.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba lazima tuwe makini kwa suala hili. Kwa kweli ninayo imani kuwa wizara hii tumempa mama ambaye anaujua uchungu wa mzazi au wauzazi, kwa sababu mwenye kujua uchungu wa uzazi ni mwanamke kwani yeye ndiye mwenye kuumwa na uchungu.

Kwa mfano, unajua wakati unapojipiga kichwa na kufumua nywele, yaani pale mwanamke anapoumwa na uchungu. Kwa hivyo, hali hii ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri atakuwa makini, ili kuiona hali hii na labda asaa Mwenyezi Mungu anaweza kutupa afuweni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu suala la kuundwa Chuo cha Malezi na jambo hili naliunga mkono, kwa sababu jambo zuri huigwa nakumbuka tulikuwa na Chuo chetu cha Mafunzo meli 10.

Kwa kweli ni vyema tukachukua kumbukumbu zetu, ili tuone kwa jinsi gani tulinufaika na chuo kile, yaani tufanye tathmini. Kwa mfano, mimi katika familia yangu nilinufaika watoto wawili walitoka na kupelekwa pale, kwa sababu walikuwa ni manunda sana, yaani wameshinda.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa nilielezea historia yao huwezi kuamini, kwa sababu ni walimu wazuri kweli, mmoja ni mwalimu wa skuli anazo madrasa 6 anasomesha na mwengine ni Imamu wa Msikini. Kwa hivyo, faida gani tuliipata pale, nadhani ni faida kubwa sana tuliipata pale kwa sababu tulipiga kelele sana kwamba lazima kiwepo Chuo hiki cha Mafunzo.

Lakini namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kuwa uanzishwaji wa chuo hiki, vyema tuangalie sana katika suala zima la maadili, isiwe washughulikiaji au wachungaji wa chuo hiki wakawa ndio waharibifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache ambayo nimechangia katika mswada huu, basi naomba niwapishe wenzangu kwa ajili ya kutia baraka zao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sifanyi jema kama wewe umekaa hapo na mimi nisichangie. Kwanza napenda nikupongeze kwamba umeomba nafasi naona unaimudu, basi jitahidi na Mwenyezi Mungu atakusaidia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu nimeomba nisimame hapa kama daktari, mimi ni Muislamu kama walivyo wengine. Lakini nataka nizungumze jinsi gani sisi madaktari tunavyopata matatizo wakati watoto wadogo wapoolewa na kujifungua.

Nadhani tumefahamu alivyotueleza Sheikh juzi kwamba mtoto akesha balegh iwe miaka 9 au 16 ina maana huyo tayari ameshakuwa mtu mzima, nakubaliana na hilo. Mhe. Mwenyekiti, watoto wote wanapokwisha kuvunja ungo wakike ina maana ni watu wazima.

Vile vile nakubaliana na wale wote wanaosema tusiache maelekezo ya Mwenyezi Mungu katika tafsiri ya mtoto, kwa sababu hayo ndiyo tunayotakiwa tuyafuate, ili tuweze kuwa na maadili mema.

Lakini kama daktari au mwanamke kuna mambo ambayo tunakutana nayo au tulikutana nayo wakati mimi nilipofanyakazi katika Wodi ya Wazazi, ambapo kwa kweli mtoto mwenye umri chini ya 18 kwenye wodi ile inakuwa sio mambo mepesi kwetu wala kwa yule mzazi.

Kwa kweli tunaangalia sisi tunaozungumza, yaani tunaziita *extremes* kwamba watoto wawili au watatu ambao wamekuwa watu wazima, lakini vitendo vya vikakithiri vya watu wazima. Mhe. Mwenyekiti, sio watoto wote tulionao kwenye ulimwengu huu wanafanya hivyo ni asilimia ndogo ya watoto wanaokuwa hivyo.

Mambo kama hayo yanasababishwa na sababu mbali mbali kama vile mtoto akili yake sio nzuri tokea amezaliwa, kwa sababu wale ambao ni taahiri ukiwatizama sisi madaktari, yaani mtoto kama yule anakuwa na nguvu hizo za kutaka hayo wakati akiwa na umri mdogo na hayo ni sehemu ya maradhi ya akili.

Watoto wengine inategemea na malezi na jumuiya aliyokuwa nayo. Kwa mfano, watoto wanaokua katika jumuiya isiyokuwa na usimamizi mzuri, basi wanaanza hayo mapema kabla ya kuvunja ungo. Kwa hivyo, hiyo inakuwa ni tabia.

Vile vile kuna wengine ambao wamekuwa watu wazima, lakini Mwenyezi Mungu anawajaalia wanakuwa na maumbile ambayo tuseme ni *hormones* zinazidi kiwango. Kwa hivyo, huyo atakuwa na matamanio ya mwili mapema kulinganisha na wengine. Kwa maana hiyo, hizo ni *extremes* sio kwamba kila mtoto yuko hivyo.

Watoto wanaovunja ungo wakati huo tulipovunja ungo sisi basi sote tulikuwa tukielekezwa kwamba hili usilifanye, sasa wako waliokuwa wakisikia na wasiosikia juu ya kwamba tunaambiwa. Kwa kweli tunajua kuwa kufanya hili ni kosa na tunafanya makosa, ndio maana utakuta kwamba wako wanaozaa nje ya ndoa pamoja na kuambiwa na wazee wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumze kama daktari. Tunapozungumza watoto na watu wazima kidaktari kuna makundi matatu, yaani kuna mtoto mdogo ambaye tunamwita *child*, halafu kuna mtoto ambaye tunamwita *adolescent* na kundi jengine mtu mzima. Kwa hivyo, mtoto akiwa chini ya umri wa miaka 15 au 16 yule bado anakuwa ni mtoto ambaye ni *child* lakini hasa mpaka 14, anapoingia 15 mpaka 18 tunamwita *adolescent* na baada ya hapo ndipo anapoanza kuwa mtu mzima.

Sasa tabia za mtoto ambaye mpaka umri wa miaka 14 bado zinakuwa za kitoto hata kama ameshavunja ungo. Kwa hivyo, anapofika umri wa miaka 15 anaanza kuwa mtu mzima kimaumbile na anakuwa na matamanio yote kama mtu mzima. Kwa maana hiyo, umri huo kumzuia mtoto inakuwa si rahisi sana hata kama anakuwa na walezi wazuri kiasi gani sana, kwa sababu ni maumbile ndiyo yanayomfikisha pale.

Lakini tunapofikisha umri wa miaka 18 yule mtoto hata kama alikuwa mtukutu kiasi gani kwa kipindi kile anaanza kutulia, kwa sababu mambo mwilini mwake yameshatulia na viungo vyake vyote vinakuwa tayari vimeshakua. Kwa hivyo, mtoto wa umri wa miaka 18 anaweza kuolewa au anakuwa tayari ameshakuwa mtu mzima na hata akiolewa inakuwa hakuna madhara, kwa sababu kila kitu kiko tayari.

Sasa katika ulimwengu wetu wa leo tunazungumzia masuala ya usawa wanaume na wanawake, kielimu, kimaisha na kiuchumi. Mhe. Mwenyekiti, hayo katika taratibu zetu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sijui labda

wabadilike sasa, wakati tuliposoma sisi watoto walikuwa wakiolewa na huku wakisoma na baadaye ikabadilika, ukisoma hutakiwi kuolewa. Kwa hivyo, sijui kama watayarudisha tena masuala ya kuolewa au kama wanaolewa sina uhakika.

Lakini tunataka mtoto wa kike sisi kama wanawake tunataka maendeleo ya leo, yaani asome na amalize. Kwa kweli asome aweze kuwa ni mwanamke bora, mwenye uelewa, maisha mazuri, kiuchumi, kiutamaduni pamoja na mengine yote ambayo tunayapenda yawe.

Kwa maana hiyo, tupate ule nafasi ya kumsomesha mtoto wetu wa kike, mtoto wa miaka 9 ukishamuoza ina maana kwamba amebahatika amepata miaka 10 amezaa mtoto, basi huyo hana masomaji tena na wala usimtegemee kwamba atakuwa na maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunazungumza hapa kwamba ukitaka familia iendelee basi msomeshe mwanamke mmoja atasomesha familia nzima. Sasa mtoto wa miaka 9 ataisomesha familia ipi wakati yeye mwenyewe ni mtoto mdogo. *(Makofi)*

Nadhani angalau mtoto anayefika darasa la 12 ina maana siku zote ana-*approach* miaka 18. Kwa hiyo, huyo hata kama hakufaulu na kupewa mume, basi kwa kiasi fulani inakuwa imemsaidia kwa sababu umri wa kuolewa umefika akiwa na mwili ambao tayari umeshakuwa kiasi cha kuweza kuwa na mume, akili imetulia na wakati wa kujifungua mtoto hapati matatizo.

Sasa mtoto mdogo wa miaka 9 mpaka 15 anapokuja Wodini sisi madaktari roho zetu zinakuwa juu, kwa sababu hatujui itapita salama vipi. Kwa kweli siku zote kuzaa kwao ni kwa kusaidiwa na wanapozalia nyumbani wanapoteza maisha, kwa sababu ya kupoteza damu nyingi pamoja na michaniko, kwani mwili wake bado haujawa tayari na wala sisemi wasiolewe, lakini nataka tujue kinachoendelea. Mhe. Mwenyekiti, kama kweli tunawapenda watoto wetu sidhani tungetaka watoto wetu wafikwe na haya.

Mhe. Mwenyekiti, tafsiri zibaki kama zilivyotafsiri, yaani ya dini ibaki kama ya dini na tukubali, lakini tuangalie na maisha yetu ya leo ulimwengu tulionao leo, ambao tunataka wanawake na wanaume tuwe sawa kielimu, kifamilia, kipato na maisha tunayokwenda nayo ulimwenguni. Kwa vyovyote vile itakavyokuwa jua kuwa ni Waislamu hatwendi nje ya ulimwengu huu tunaokwenda nao, kwa sababu ulimwengu ni mmoja na mambo yake yanakwenda kwa pamoja.

Kwa hivyo, jambo la msingi tuseme na watoto wetu, tuwachunge na tuwalee vizuri, wafikie umri unaotakiwa na wala wasipate madhara, wasome na halafu

waolewe, kwani tunachokikimbilia kitu gani mtoto akiolewa miaka 18 anayo nafasi ya kuzaa mpaka akiwa na miaka 40 na kinachokimbiliwa ni kipi.

Sasa yule mwenye bahati mbaya atakayetokea kwa sababu yoyote ile ambayo imemfika na wala hawezi kusubiri basi hayo ni mengi na sisemi asiolewe, kwa sababu hata ukimuweka atatoka na kwenda kufanya anayoyataka.

Lakini tujitahidini tuwatunze watoto wetu wawe wakubwa, wasome wamalize, wawe wanawake bora wanaoweza kutunza familia zao. Kwa kweli mwanamke aliyesoma anaweza kutunza familia pamoja na ndoa yake vizuri ukitafautisha na yule ambaye hakwenda skuli, kwa kweli aliyesoma hawi sawa na asiyesoma. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu kwa maneno mawili matatu.

Kwa kweli mchango wangu utakuwa ni kijumla jumla. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak ingawa nitayagusia kidogo yale mambo aliyoyazungumza.

Nadhani ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba ile tafsiri ya mtoto atupatie tena ili kuweka sawa, kwa sababu mswada ukesha kupitishwa ndio unakuwa sheria na leo tutaupitisha Mwenyezi Mungu akipenda tutaupitisha. Kwa hivyo, mswada ukesha kupitishwa ndio inakuwa ni sheria. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bado ninazungumza kama kuna mtoto atafikia miaka 30 anaitwa mtoto kutokana na umbile lake alilonalo, kwa sababu kuna watu miaka 30 bado ni mdogo hata akipata waume 10 ni mtoto tu ukimuona. Lakini kuna watu kama nilivyozungumza miaka 9 atakuwa ni mwanamke tena ni mwanamke wa kweli, yaani ni mwanamke na huyo tukisema mpaka afike miaka 18 basi atazeeka bure na ukimuona utadhani ni mzee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna watoto tusiwakoseshe masomo yao, lakini kuna watu ambao hawasomi, yaani hawaendi skuli na wapo nyumbani tu. Sasa mtoto ameshafika miaka 9 au 16 ni mtu wa kuowa na baba yake ameshapata mume wa kumuozesha amuweke tu nyumbani. Kwa hivyo, bado namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili utupe tafsiri vizuri kwani leo mswada huu tunataka kuupitisha, ili uwe sheria. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine kuhusu suala la malezi ya mtoto. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kupitia wizara yake aiombe serikali watoto wagonjwa wa akili, basi waekewe sehemu ya kuhifadhiwa kama wale watoto mayatima, kwa sababu kama anavyozungumza kwamba hawa watoto wanapata tabu sana kama vile kubakwa pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, serikali kama itawaweka sehemu na kuwa na matunzo ya serikali, basi si rahisi mtu kuingia na kumbaka.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aiombe serikali kama hawa watoto waekewe sehemu kama skuli kwa ajili ya kuhifadhiwa, kwa sababu ni watoto wetu kama tunayo nia ya kuwatunza watoto wetu kweli, basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, afanye hivyo kwamba wajengewe kama skuli wale watoto wagonjwa wa akili ambao ni watoto na wala sio wale waliobakwa na tayari wameshazalishwa, ili tuwatunza watoto wetu.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tuwaombe wazee wa watoto. Kwa mfano, sisi Waheshimiwa Wajumbe ambao tumo humu ni jumla ya wazee wa watoto, kweli kumeingia vitendo vya watu kubaka watoto. Lakini na sisi wazee jamani tujitahidini kwa sababu tumeacha mila pamoja na silka zetu, kwa kweli watoto tumewapa uhuru ambao ni mkubwa. Kwa kweli mtoto anatoka nyumbani na wewe baba yake ukimtiza unamuona hawezi kufika hata hapo njiani atabakwa, basi unamtiza tu na wala huthubutu kumkemea na wala kufanya kitu chochote, jamani tunaelekea wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, narudia kusema kwamba sisi ni wachunga na tutakwenda kuulizwa jinsi ya uchunga wetu tuliochunga. Kwa kweli Zanzibar tumeacha mila na silka zetu pamoja na kuwepo kwa Haki za Binadamu, kwa sababu hizi Haki za Binadamu ndizo zinazotupa mambo yote.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tutoe msisitizo kwa wazee na wala tusiweke msisitizo mtoto kwamba mtoto amelelewa vibaya na baba yangu apate adhabu hii na ile. Lakini watoto wetu malezi tunayowapa sio, kwa sababu tumewapa malezi mpaka tumeacha kuangalia hata zile dini zetu jamani, watoto tunawalea vibaya, yaani mtoto anatoka nyumbani na mzazi unamuona.

Kwa mfano, mtoto anatoka nyumbani kuanzia saa 1:00 za asubuhi mpaka siku ya pili, hivi kweli asibakwe vipi huyo na lazima atabakwa na sisi tunawatizama tu. Kwa hiyo, kubakwa ni kubakwa tu hata ukimwambia wewe kwa sheria za wenzetu tayari umeshamkaba kama hakukwambia yeye mwenyewe. Sasa kama anatoka kuanzia asubuhi mpaka siku ya pili ndio anarejea na nguo anazovaa ni mtihani.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tunakwenda mwenendo ambao sio, unamuona mwanao anatoka na wakati anaporudi anakuja na simu ya shilingi 400,000/- na wewe baba hujamuuliza simu hii umeipata wapi. Vile vile simu ile inahitaji fedha ili iweze kutoa huduma, yaani mtoto mchana mzima anapiga simu na kuzungumza na watu, kwa kweli anatiliwa fedha na watu na wala humuulizi. Kwa hivyo sisi tunakuja kusema watoto wanabakwa na wakati mwengine hawabakwi isipokuwa wanajibakisha wenyewe.

Nawaomba tunatunga sheria lakini na hili tuliangalie tutizame watoto wetu na tuwakemee tusiwape uhuru mpaka ukazidi kipimo, watu wanasema demokrasia ikizidi kipimo inakuwa ni mbaya na watoto wetu uhuru tumewapa mkubwa mno, jamani tuwaleeni watoto wetu tusiwape uhuru mpaka ukakisiri waheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti suala jengine ambalo kuwa kwenye mswada sijui kama sikuliona au ni macho yangu ni suala jengine nakuomba na hili nalo tuliangalie kwa upana wetu, watoto wetu wadogo wadogo ni watumiaji wa madawa ya kulevya, unamkuta mtoto mdogo kabisa miaka sita anavuta bangi hata huyo mtu wa miaka mia moja havuti kama anavyovuta yeye.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na hili nalo kama kalisahau kuliweka kwenye mikakati basi nalo tulione kwamba jamani na hili ni moja katika maadili yetu ya watoto wetu ambao wanavuta bangi na madawa ya kulevya, tena watoto wadogo wadogo na wakishafana hivyo ndio wanaotumbukia kufanya vitendo viovu wanakuwa wabakaji wanawabaka mpaka wazee wao, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti sasa hivi wewe ukenda Mboriborini watoto unaosikia ni wahuni wanapora watu simu, wanaonyang'anya watu pesa na kuwapiga mapanga ni watoto wadogo wadogo huwezi kuamini. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba na hili ulione kwamba watoto wetu wanatumia madawa ya kulevya na wakishatumia madawa wanatoka kwenye maadili yetu.

Mhe. Mwenyekiti kwa hayo machache naomba nikae ili niwape fursa na wenzangu nao waendelee. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mswada huu haki ya mtoto, hapo mwanzo haki ya mtoto tulikuwa tunaelewa kwamba kuanzia miaka kumi na nane kuelekea chini huyo ni mtoto, lakini tunakwenda kwa wakati huu huu mtoto wa miaka kumi na nane tunaona ni tayari kijana, kwa hivyo wakati wa kuitwa mtoto ni afadhali awe na miaka kumi au miaka kumi na mbili. Kwa sababu sasa mtoto wa miaka kumi na tano tayari anataka mke je utamwita mtoto bado huyo, mtoto wa miaka kumi na mbili wa kike tayari anadai mume na anamleta mwenyewe nyumbani kwamba

mimi baba tayari nimepata mchumba ana miaka kumi na mbili na lazima umkubalie kumpa mchumba huyo, kama hukumpa anakwambia nitajinyonga au nitahama nyumbani.

Kwa hivyo haki ya mtoto isianzie miaka kumi na nane iwe kuanzia miaka kumi mpaka kumi na mbili ibaki hapo, kwa sababu kuanzia miaka kumi na tano na kumi na nane huyo ni kijana sio mtoto tena na hata akibakwa kwa miaka kumi na nane huyo sio mtoto ni kijana, kwa sababu vijana wote wanaotembea hasa mjini kwa umri wao ni maka kumi na mbili au miaka kumi na nane unawakuta watu wazima na ndio wanaotembea mjini kwa hivi sasa.

Kwa hivyo nachangia kwamba miaka kumi na nane tuondoke katika suala la mtoto na tumuite kijana asilimia kubwa ya watoto wa miaka kumi na mbili na miaka kumi na tano ndio watendaji wa taifa hili na sio kungojea mpaka miaka kumi na nane, suala la miaka kumi na nane namuomba Mhe. Waziri akaliondoa na kuita watoto kuanzia miaka kumi na kumi na mbili, hapo ndio tungelikuwa na jukumu la kusema tunawatunza watoto sio miaka kumi na nane kusema kuwatunza watoto.

Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa na mengi ila ninachangia hayo tu kwamba tuelewe suala la watoto lisizidi miaka kumi na mbili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu nikiwa miongoni mwa wajumbe wa kamati ya maendeleo ya wanawake na ustawi wa jamii na nikiwa ni makamo mwenyekiti wa kamati hii, kabla sijachangia kwa sababu mswada huu ni muhimu sana nichukue nafasi hii kwa niaba ya kamati yangu kuwaomba wajumbe wachangie mswada huu kwa sababu utamsaidia Mhe. Waziri kuweza kuwaka sheria hii katika hali ya uwazi na utasaidia nchi yetu kuwa na sheria ambayo itawalinda watoto kwa siku za karibuni na siku za baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati hii na tumeupitia mswada huu kwa upeo wetu kwa muda wa siku tatu, kimsingi Mhe. Mwenyekiti mswada huu kama kamati tumeuona ni mswada muhimu ambao kimsingi hauna matatizo na una nia safi ya kuwalinda watoto wetu, lakini kwa sababu mswada huu ni mkubwa na unagusa maeneo mengi muhimu ya kisheria kuna haja ya kuomba wajumbe wawe makini sana kuchangia mswada huu, kwa sababu pale ambapo tutaamua kupitisha itakuwa tumewaamulia Wazanzibari maamuzi ya milele.

Mhe. Mwenyekiti, mimi natoa wito tu kwa wajumbe wanzangu kuchangia mswada huu kwa lengo la kuwawekea maisha mazuri watoto wetu ambao watapata haki fursa na maslahi mengine katika sheria hii, sasa mimi kiujumla

sina matatizo na huu mswada nia yake na malengo yake ni mazuri na umekusudia kuwaokoa watoto wetu wa Kizanzibari, lakini kwa sababu ya ukweli kwamba mswada huu umegusa maeneo ya kidini na baada ya taaluma ya juzi ya Katibu wa Mufti Sheikh Soraga naomba niseme kwamba tafsiri ya mtoto Mhe. Waziri ningemuomba akaiangalia vizuri na tena, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwenye sheria ya dini mswada huu unasema kwamba unangalia utamaduni, silka na mwenendo wetu wa kidini.

Katika mswada huu kuna kifungu kinachozungumzia Kafala na kuwasili kwa maana ya kwamba umezingatia maslahi ya kidini. Kwa maana hiyo katika tafsiri ya mtoto katika mafundisho ambayo Mtume ametufundisha alitwambia kwamba mambo matatu yakifika muda wake hayapaswi kuwekwa. Kwanza sala ikifika wakati wake isaliwe hilo ni agizo la Mtume, pili akatuagiza kwamba mtu akifariki basi haraka sana azikwe na tatu akatuagiza kwamba mwanamke anapofikia baleghe basi haraka aolewe. *(Makofi)* Mhe. Mwenyekiti hayo ni maagizo ya Mtume na wala hayataki mjadala wala hayana sheria itakayopinga mtume hasemi ila kwa agizo la Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo Mtume anasema kwamba mwanamke akifikia baleghe haekeki aolewe kama hakuna sababu za msingi ambazo sheria inakubali huyu aolewe kama hasomi kama hana matatizo mengine ya ungojwa kama alivyosema Dk. Sira basi haraka hiyo biashara isiwekwe iolewe, na juzi kwenye semina Shehe alitwambia zaidi kwamba Mtume huyo huyo akasema tena kwamba mtu aliyelala kalamu haiandiki madhambi, halafu tena akasema mtu mgonjwa wa wazimu kalamu haiandiki madhambi na mtoto ambae hajabaleghe vile vile kalamu haiandiki madhambi. Kwa hivyo ni kwamba mtu akibaleghe huyo sio mtoto ndio tafsiri ya maneno haya ya Mtume.

Mhe. Mwenyekiti mimi naheshimu sana mswada wakamati nikiwa ni mmoja miongoni mwao lakini nikiri kwamba siku ile tulikuwa hatuna taluma nzuri ya kidini, mawazo ya Shehe Soraka kwa mujibu hadithi alizotoa na Quran ni sababu tosha za kujenga hoja kwamba mtoto huondoka mtoto pale baada ya kubaleghe, kwa hivyo ili Wazanzibari wasiingie kwenye makosa ningeomba kwamba wanasheria na Mhe. Waziri wazingatie hoja hii kwambatuweke tafsiri ya mtoto vizuri, nadhani hii tafsiri ya kwamba mtoto aliyekuwa hajafikia umri wa miaka kumi na nane tuongeze tu kwamba na ambae hajabaleghe. Kwa sababu wengine miaka kumi na nane hawajabaleghe kuna wanaweke miaka kumi na nane wengine hawajavunja ungo kwa hivyo sawa ni mtoto, lakini akibahatika miaka kumi na mbili akavunja ungo baso kwa mujibu wa sheria ya dini huyo sio mtoto.

Mhe. Mwenyekiti tukubali kwamba kuna maumbile tumezidiana kuna watoto hapa wadogo sana kiumri lakini wakubwa sana, ukiambiwa huyu ni miaka

kumi na mbili unakataa ni chuma cha nguvu, kwa hivyo mantiki ya sheria hii kulingana na Mtume hakukosea aliangalia mazingira hayo, miongoni mwetu humu tumeoa watoto miaka kumi na sita lakini ni watoto wa kweli kweli. Nikikwambia kwamba huyu ni mke wa fulani ana miaka kumi na sita huamini mtoto wa nguvu, kwa hivyo ningeomba sheria kingezingatia yote hayo kwamba watoto wadogo wengine ni umri wao lakini maumbile yao ni makubwa, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwamba kuna watu wengine ni watu wazima lakini akili zao sio barabara, viungo vyao sio makini kwa hivyo wale wasiolewe.

Lakini madam mtoto hasomi na hana mazingira mengine ya kiasari za afya na yuko tayari kuolewa na tayari sheria ya dini na sheria nyengine zimemkubali nadhani huyu aolewe na tumpe mazingira salama ya kumuokoa katika maisha yake, hatuwezi kuzuia matamanio ya nafsi, nafsi ni sehemu nyengine ya haki Mhe. Mwenyekiti, na mswada huu umesema kwamba mtoto asiasiriwe kiakili na hata kiroho. Mhe. Mwenyekiti nadhani kwenye maslahi ya kidini tuangalie sana kwenye suala hili, mimi kwa sababu najua kila mmoja ni mchunga na kila mmoja ataulizwa hapa sitokuwa rahisi mpaka wale Mufti akina Abdalla Juma watusaidie nahofia kamba kuja kuamua maamuzi ambayo yataingilia mamlaka ya kidini, lazima tuwe makini na kwa tafsiri hii naomba tulinde na tuongeze na tulinde azimio la umoja wa mataifa lakini maazimio haya yasikiuke maazimio ya Mungu na Mtume wake.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hilo nimeeleweka lakini jengine ambalo ningerpenda kucnangia ni kutoa pongezi kwa wizara nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa kuamua kuweka watu kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu, zamani ilikuwa kesi za kubaka zinapotoea mtu anabakwa kwenye mashamba lakini kesi ikifika polisi inamalizika.

Hivi leo wameamua kuita *one stop sentre* ndani ya hospitali ya Mnazi mmoja kwamba pale panakuwa na mtu wa ustawi, panakuwa na watu wa wakurugenzi wa mashitaka, panakuwa na polisi na madaktari kwa hivyo tukio likitokezea pale pale suala la mara moja linamalizika bila ya utata. Kwa hivyo hili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwakuamua kwa makusudi kuweka kituo kile ndani ya Zanzibar kwa ajili ya kuokoa watoto wetu. Mhe. Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Mhe. Waziri aharakishe sana Pemba kifunguliwe kituo kile ili watoto wa Pemba waweze kupata haki yao haraka iwezekanavyo.

Suala jengine ambalo niwapongeze kwa dhati kabisa ni maamuzi ya serikali ya kuwatoa watoto wale wa Forodhani na kuwapeleka nyumba ya watoto Mazizini, kwa kweli bila ya kuzingatia sababu nyengine mimi sizungumzii kwamba nyumba ilikuwa ya nani na kapewa nani, nazungumzia mazingira ya

kuhifadhi mtoto maamuzi ya serikali kumtoa mtoto Forodhani na kumpeleka Mazizini ni sahihi na kwakweli wanaishi katika maisha mazuri hata kama wale wawakilishi hatuwamudu, anapolala mtoto hapo Mazizini sisi wawakilishi wengine hatulali kama hapo, wanalala katika mazingira mazuri sana vitanda vya maana. Wanapata huduma nzuri kwa hivyo hili nataka nichukue nafasi hii kumpongeza *ZAYADESA na* mama Shadia kwa maamuzi yao ya kuwasaidia watoto katika nyumba ile.

Mhe. Mwenyekiti ili nyumba ile ibakie na maendeleo mazuri ya kisasa naomba Mhe. Waziri maslahi ya wale walinzi yaongezwe walezi wale wanapambana na watoto tofauti, wengine hawana akili wengine midomo haisemi na wengine wagonjwa kwa hivyo mazingira wanayolala wazee ni magumu kwa hivyo maslahi yale basi yaongezwe.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo nizungumzie haraka haraka ni suala zima la uzalilishaji wa kingono, sheria hii inazungumza kwamba wale watakawazalilisha kingono watoto wetu wapate adhabu na mimi naunga mkono kwamba lazima wanaowadhalilisha watoto kingono waadhibiwe, sijui wanasheria watanambiaje lakini haiwezekani mtu mwenye wake wawili au watatu akenda kutafuta watoto wadogo nadhani huyo mtu raha zitakuwa zimemzidi, sasa kama zimemzidi basi tumuhasi kwa kumpunguza matumainio kwa sababu mtu ana wake wawili au watatu au wanne bado watoto wadogo anawavamia. Ni tatizo kwa hivyo tumpunguze nguvu apumzike sijui wanasheria watasemaje lakini mimi nadhani kulea kubaya tumuhasi ili asituhasi katika maisha yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti mmesahau wanasheria kwamba mnamuangalia mwanamme tu ndio anayaharibu kingono, wapo wanawake wanaochakachua wanawake wengine, kuna wanawake wanawaharibu wanawake wengine sawa sawa na mwanamme anaiharibika kingono wanawachakachua. Kwa hivyo sheria haikusema kwamba mwanamke atakayekamatwa akimuharibu mwanamke mwengine kwa mkono au kwa mguu lakini afanywe nini, nadhani hii Wizara ni ya Wanawake na Watoto lakini Ustawi wa jamii na mwanamme alindwe na mwanamke apate adhabu, kama kuna mwanamke Zanzibar au nje ya Zanzibar akija hapa akimchukua mtoto wa kike akimharibu kwa njia yoyote ile huyu ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria sio mwanamme tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti kuna wanawake wengine wanafanya hatari sana na wanawakosesha wanawake wengine haki zao hata za kuolewa anakuwa hatamani kuolewa, hatamani kusoma kwa sababu ya mkono au mguu. Kwa hivyo Mwenyekiti mimi nasema sheria lazima iseme wanawake wale watapata adhabu gani sio mwanamne tu anaangaliwa kwa nini kabaka ndio anabaka tuwaadhibu wafungwe, kwa sababu sioni tukielekea kwa wanaume hawa

wanawake ambao kuwa wamepevuka haraka wataelekea kwa wanawake wengine. Kwa hivyo ili kuweka msingi wa kuwazuia basi tuweke adhabu na sheria iseme kwamba mwanamke huyu atapewa adhabu gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti mimi ni mjumbe wa Kamati na Waziri akiniweka sawa hapo penye wanawake ambao wanachakachua na tafsiri ya mtoto mimi sina wasi wasi sheria ni nzuri na nawaomba waheshimiwa wajumbe wachangie tuwasaidie wenzetu hawa wapitishe sheria hii na hii tafsiri ningemuomba Mhe. Waziri akae na wanasheria wake na Mashehe wengine akina Abdalla Juma mutupe tafsiri ili tusije tukavuka mipaka kidini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru na naunga mkono hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Hija Hassan Hija kanimaliza yote niliyokuwa nataka kuzungumza ni bosi wangu huyu katika kamati, wala hayataki tochu kuyamurika hayo aliyosema, kwa hivyo nataka nimpongeze sana kwa ufasaha Makamo wa Mwenyekiti.

Lakini vile vile nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sikuchangia hata kidogo kwenye mswada huu, kifungu 76 Mhe. Mwenyekiti masharti ya sehemu hii yanawahusu mashehe wa dini ya kiislam kwa nini tutunge sheria inayokwenda kinyume na maadili yetu sisi waislam tuwatungie wakiristo sheria hii, kifungu hiki cha 76 mpaka cha 85 kifutwe.

Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitimize wajibu wangu, kwanza kabisa mimi naipongeza serikali kwa kuleta mswada huu ambao ukiuangalia lengo na madhumuni yake ni kuwatunza watoto wetu. Kwa sababu watoto ndio taifa la kesho ndio nguvu kazi, sasa naipongeza sana serikali kwa kuzingatia hilo.

Mhe. Mwenyejkiti, mimi nina maoni mengi ambayo ni haki za watoto lakini katika mswada huu sikuyaona na naomba niyaseme wenzangu wayajue, pengine na Mhe. Waziri anaweza kushawishika akaona nayo yawe ni sehemu ya huu mswada.

Mhe. Mwenyekiti watoto wana haki nyingi na haki hizo tunazo sisi wazee wao nitatoa mfano tu sisi wazee tukiachana kwa namna moja au nyengine tukipenda au tusipende lakini tumevunja haki za watoto kwa sababu mtoto analelewa na babaake na mamaake haiwezekani hata siku moja mtoto kulelewa na baba wa kambo akapata mafunzo kama yale ya babaake hilo haliwezekani, ubinaadamu utapita tu kwamba huyu mimi sio mwanangu kwa hivyo malezi yake

hayatakuwamazuri. Lakini na mama wa kambo nae ni hivyo hivyo akiolewa na baba ambae ana watoto wake basi mama yule malezi ya wale watoto wa mume wake hatafanya kama ambavyo kawazaa yeye mwenyewe, kwa hivyo tendo la kuachana mke na mume ni kuvunja haki za mtoto.

Mhe. Mwenyekiti tumeelezwa na Mashehe kwamba talaka mungu kaifanya halali kwa kunyongea pale patakapokuwa hapana budi wakiendelea kukaa hawa watasababisha madhara makubwa, lakini ni halali pekee katika mambo aliyohalalisha Mwenyezi Mungu ambayo anaichukia talaka sasa msingi wa kuichukia ni kwamba watoto watapata tabu. Kwa hivyo tuzingatie kwamba wazee wasiwe wepesi kuachana kirahisi kwa sababu tutakuwa tunawadhalilisha watoto na kuna familia nyingi na mifano mingi ambayo tunawaona watoto wanavyoteseka na wanavyopoteza muelekeo baada ya wazee wao kuachana, sasa nilikuwa si rahisi kusema watu wasiachane, lakini sheria ingezingatia kwamba sasa watu wakiachana basi kuwe na jopo maalimu linalifanya kwa nini waachane ikiwezekana warejeane wakalee watoto wao hilo mo.

Lakini la pili miongoni mwa haki kubwa sana ya mtoto ambayo tunaivunja sisi wazee ni kuwaachia watoto *free* tukawa hatukuwaleya kwa mujibu wa maadili, tumeambiwa pia siku ya kiama ikifika mzee kama kaswali mpaka kavijuka uso lakini kama hakumwambia mwanawe aswali au hakumfundisha mwanawe tabia njema basi mbele ya mungu atakuwa kavunja haki kubwa sana ya mtoto na inawezekana ikawa sababu ya yeye kwenda motoni. Sasa tukiangalia malezi ya watoto tusiangalie tu katika mtazamo wa kidunia lakini tuangalie hata katika mtazamo wa maslahi ya huko mbele tunakokwenda.

Sasa mimi nafikiri lazima tunasihiyane kwamba watoto wetu miongoni mwa haki zao kubwa sana ni kuwalea kimaadili sio kuhakikisha kwamba wanavaa vizuri, kwenda shule, wanakula vizuri tukasema tumemaliza haki za mtoto lakini pia kumlea katika maadili mema hiyo ni haki moja kubwa sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema hapa kwamba kifungu cha 76 alikuwa anapendekeza kile kifungu kifutwe, mimi nilikuwa na mawazo kwamba sisi waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hapa tunapitisha sheria, tukisharidhia sheria kupitishwa basi yatakayotendeka kwa mujibu wa sheria ile na sisi tunahusika kwa njia moja au nyengine. Sasa Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 76 kinazungumzia mambo ya kuwasili na tukiangalia maana ya kuwasili ni kumtoa mtu kwenye familia yake ya kwanza ya kibailojia na ukamhamisha ukampeleka katika familia nyengine, katika hiyo familia anayokwenda anakuwa na haki zote kama vile kazaliwa ndani ya familia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naogopa sana kuliridhia hili na naogopa kwa sababu dini yetu sisi haituruhusu kufanya hivyo, kwa sababu mtoto kumtoa katika

familia moja ukampeleka katika familia ya pili na kule akawa anapata haki zote maana yake kule atarithi, kama ni mwanamme atamuodhesha ndugu yake mke na mimi ni mume mambo ambayo hayakubaliani na dini yetu.

Mimi nilikuwa nafikiria hii kafala ingetosha. Mimi binafsi siko radhi hata siku moja kukubali kifungu hiki kiwemo, achukuliwe mtoto akapewe mirathi isiyokuwa haki yake, kesho akhera Mwenyezi Mungu akanikamate kwa hii ukaipitisha. Hilo Mhe. Mwenyekiti siliridhii na naomba sana waheshimiwa wenzangu tusilikubali hili.

Mimi nilikuwa nadhani *concept* ya kusaidia ulezi. Hichi kifungu cha 74 kilichokuwa kinazungumzia mambo ya kafala kilikuwa kinatosha. Kina mahitaji yote ya kusaidia ulezi kwa familia nyengine. Kuweka hii ambayo itasababisha madhara. Mimi hii sikubali na nasema hapa nitapiga buti kesho tukijaaliwa mpaka iwe balaa.

Mhe. Mwenyekiti, nikirudi kwenye kifungu Nam. 2, kwenye ufafanuzi. Pale kuna neno udhalilishaji wa mtoto. Limetolewa tafsiri yake vizuri sana. Mbele huku kuna udhalilisha watoto. Hichi kwa kwanza udhalilisha mtoto, kule kuna wadhalilisha watoto. Nilikuwa sioni kama kuna haja au vyenginevyo watoto iwe na tafsiri nyengine, ukiachilia mbali ule umoja na wingi kuwa huyu ni mtoto wale ni watoto. Labda iwe na maana nyengine. Lakini ikiwa maana ni ile ile basi hii ya kwanza ilikuwa inatosha. Na hii ya pili nilikuwa naomba ifutwe.

Kifungu cha 4. kunamaelezo pale naomba nisome kidogo.

Kifungu cha 4 “Katika kuamua maslahi bora ya mtoto vigezo vifuatavyo vitazingatiwa:-

(a) “Hali ya uhusiano binafsi baina ya (i) mtoto na wazazi au mzazi maalum”

Hoja yangu hapa iko kwenye huyu mzazi maalum ni mzazi gani. Maana ukishasema wazazi ni baba na mama na ndio wazazi wa mtoto. Kama kuna mzazi mwengine maalum mimi naomba nisaidiwe tafsiri. Imejirudia hilo kwenye kifungu (a), (b) na (c). Sasa nilikuwa naomba waziri akija anifafanulie kidogo kuhusu huyu mzazi maalum ni mzazi gani.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba nitoe tahadhari kidogo kwa sababu Mswada huu utakuwa umeingiliana sana na mambo ya kidini. Tumezozona sana hapa kuhusu tafsiri ya mtoto ni nani. Mpaka juzi nakumbuka shehe Soroga akatoa tafsiri ya mtoto kwamba ni yule aliyefikiwa umri wa

kuweza kuzaa ikiwa ataowa au ikiwa ataolewa ndiyo tafsiri aliyotoa yeye kwa mujibu wa kiislamu.

Watu wengine wanasema mara awe na miaka 12 mara 15 mara 18. Sasa *Wallahi* mimi jawabu sina. Nafikiri tukubaliane na ile tafsiri ya Shekh Soroga. Mtoto ni yule aliyekuwa hajafika umri wa kubaleghe. Tusiisabu miaka, mara hii Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa kwenye zoezi la kuandikisha kupiga kura, tunapeleka watoto wana miaka 20, 25, lakini ukifika kwa Afsa Uandikishaji anakwambia huyu hajafikia umri, huyu ni mtoto, kwa cheti ana miaka 20 lakini bado anaitwa mtoto, kutokana na lile umbile laki la mwili ni mdogo. Kuna mwengine anakuja pala ana umri wa miaka 12 tu, akifika pale haulizwi kutokana na umbile lake la mwili ni kubwa. Namkumbuka mtu kaolewa akiwa na umri wa miaka 9 na akapata mtoto akiwa na umri wa miaka 11 hajafika hata miaka 12.

Sasa ikiwa sheria inasema bado yole ni mtoto kwa kuwa ana miaka 12, mtoto hazai. Nafikiri tutafute lugha ya kutumia ili tuweze kukubaliana kwamba mtoto ni yule aliyekuwa hana uwezo wa kuzaa. Ikiwa mtu ana uwezo wa kuzaa basi huyo si mtoto tena hata kama atakuwa na umri wa miaka 9. Sheria hii itakuwa ina utata sana na tutazozana hapa mpaka keso asubuhi hapa hatupati jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote naunga mkono Mswada wote isipokuwa kifungu cha 76, sikiungi mkono Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Mswada huu muhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umekuja kwa kuzingatia yale yote yanayowasibu watoto wetu. Watoto wetu tulionao katika nchi yetu ya Zanzibar. Kuna watoto ambao wazee wao wana uwezo Alhamdulilahi. Kuna watoto ambao masikini na hawana uwezo. Kuna watoto mayatima aidha hawana baba au mama na kuna wengine hawana baba wala mama. Kuna watoto ambao wamezaliwa nje ya ndoa. Kuna watoto wametupwa na wengine wametelekezwa. Makundi haya yote ndio makundi tunayoyazungumza hapa.

Tukitaka tusitake watoto wana haki zao za kimsingi na ni lazima tuzitilie maanani na tuzitekeleze. Kubaleghe kwa mtoto ni siri ya mtoto na wazee wake. Ndio maana sheria ikaweka kwamba miaka 18 kwa sababu itakuwa haiwezekani mtoto kufika miaka 18 akawa hajabaleghe, hapa atakuwa keshabaleghe tu. Wengine wanabaleghe miaka 9 wengine 15 wengine 17 wengine 18 wengine 14.

Kimantiki tumuangalie mtoto wako mwanamke wewe amebaleghe ana miaka 9, halafu umkabidhi mume, mume anashughuli anataka kushughulikiwa asubuhi mpaka usiku. Je, mtoto wako wa miaka 9 atahimili mikiki na kazi hizo atakazokwenda kupewa katika nyumba. Hii nyumba ataimudu, ataiweza. Kweli wewe mzee una huruma. Kweli hatuwezi sisi tukaiga makarama ya bwana Mtume Muhammad (SAW), kaowa mwanamke wa miaka 9 lakini pia kaingia nyumbani miaka 11 na sio miaka 9.

Kwa hivyo nasema kwamba tuangalieni ukweli ulivyo na hali halisi ilivyo. Tumuangalieni mtoto wa miaka 9 ambaye tumeshampa mume akifika miaka 10 anakwenda kujifungua hospitali. Mwanao huyo huyo, usimwangalie mwana wa mwenzio, wewe utakuwa hali gani, huyo mume atakuwa hali gani na yeye atakuwa hali gani. Naamini kwamba ukizingatia kwa upeo wake utaona hatari zake zinazomkabili mtoto huyo. Naomba tuiangalie sheria hii kwa upeo wake na hali halisi ilivyo.

Matatizo yanayowakumba watoto wetu tunayajua wazi wazi, kuanzia katika masuala ya kimsingi. Mtoto ana haki za kupata chakula tena ni chakula bora, kupata makaazi, matibabu, elimu, uhuru wa kucheza, kupumzika na angalau kusema akasikilizwa. Hizo ni haki za msingi za mtoto ambazo anastahili apate. Sheria yetu imeangalia hayo kwa upeo wake.

Vile vile hawa watoto wetu wanapofanya makosa wanakwenda kuhukumiwa katika mahakama za kawaida. Tumeona matatizo yanayowakabili katika mahakama hizo. Ndio maana tukaanzisha mahakama maalumu ya watoto. Tusichanganye mahakama ya watu wazima na mahakama ya watoto. Nafikiri mnakumbuka mwaka jana Mhe. Zahara alivyokuwa analia katika ukumbi wa Baraza hili, jinsi watoto wanavyodhalilika na kunyanyasika kwa kukaa katika mahabusu moja ambayo imetengwa tu mbali na watu wazima. Sheria hii imeyazingatia hayo pamoja na malezi ya mtoto kwa ujumla. Sheria imezingatia mambo yote, la msingi hapa ni kuangalia kitu gani kimekwenda kinyume na matarajio yetu.

Wiki mbili nyuma natoka Msikitini kwenye Sala ya Ijumaa, Mlandege pale *Quality Super Market*. Natoka nikakutana na kijana baro baro hivi, kakaa na baskeli kati kati ya barabara. Ile baskeli haiyendi mbele wala nyuma, kaganda kama sarakasi. Nyuma kuna magari yanakuja. Nikamwambia baba we, ondoka hapo utapondwa na gari. Kijana hasikii kaganda anaangalia. Anaangalia wapi? Kumbe anamwangalia msichana labda ana miaka 12 au 13. Yule mtoto mwanamke kavaa nguo inang'ara kama biharusi, lakini nguo haina kifungo wala haina hata nyuzi, mgongo wote wazi, kifua nusu wazi. Nikamwambia tena baba utapondwa na gari ondoka hapo. Nikamwambia yule msichana ondoka hapo utaulisha watu hapo hebu tafuta safari uende. Hali kama ile pale utaona

mtoto yule ile nguo aliyovaa ni *very expensive* sio nguo ya bei rahisi. Nguo ile kaipata wapi yule? Bila shaka mzee wake kamnunulia.

Sisi wazee katika malezi yetu tumeanza kubadilika. Unajua kwamba nguo hii namnunulia mwanangu hamstiri atakwenda kifua wazi, atakwenda nguo fupi sana, atakwenda na nguo tumbo wazi, atakwenda mikono wazi, kwapa nje. Yule anapita njiani anafanya *invitation* na watu wakishakuwa *invited* wanakaribia. Malezi yetu yameanza kuharibika hapo.

Kwanza tuangalie malezi ya wazee, halafu tuangalie mila zetu. Zamani ilikuwa mtoto halelewi na mzee mmoja, jamii nzima inasaidiana katika malezi. Maisha ya mtoto kwa mzee wake anajificha asimuone kwa mwengine hajifichi. Sasa wewe unaweza ukawa hujui kama anafanya mambo yasiyostahiki, wazee wengine wanaona lakini hawakusaidii. Zamani tulikuwa tukisaidiana, mtoto analelewa na jamii. Sasa hivi jamii hailei tena mtoto.

Mhe. Spika, kuna watoto wanatoka makwao na hijabu na mabuibui wakifika pahala wanayavua wanayatia ndani ya mikoba wakavaa vitopu na visuruwali akenda kutembea, akirudi kwao na hijabu zao na mabuibui yao kama wao sio waliovaa nguo zile. Jamii inaona kama mtoto huyu akitoka kwao anatoka na hijabu na nguo za kujistiri na akirejea yupo hivyo lakini huku nje sivyo alivyo. Hawasaidiani na kumwambia kwamba mwanao keshaanza kuharibika anapotoka na anafanya hivi na hivi. Zile mila na desturi za zamani ambazo ziliifanya jamii kuwajika katika malezi sasa hivi zimetoweka. Zamani ilikuwa jamii yote iko pamoja, inasaidiana katika malezi.

Sheria hii imeweka wazi wazi wajibu wa ulezi, kwamba wazazi ni walezi wanaojikubalisha kisheria kwamba watakuwa walezi. Jamii nayo itawajibika, Asasi za Kiraia zitawajibika na serikali itawajibika katika ulezi. Naamini kwamba zote sekta hizi zikishirikiana kwa mujibu wa sheria hii ilivyoandikwa mambo yetu yatabadilika. Utu wa mtoto utapatikana, haki za watoto zitapatikana. Sasa hivi kuna matatizo makubwa sana, mtoto anazaa mtoto, hawezi kulea mtoto huyu.

Mimi nimekwenda katika maonyesho hapo nje tangu saa 7:30 sikuondoka mpaka saa 11, nilikuwepo hapo napita sehemu moja moja. Namuuliza NGO yenu nyinyi ya Micheweni mnashuhulikia watoto. Akaeleza watoto ni wengi sana kule, malezi shida, masikini. Lakini kwa nini ikawa *child labor* kubwa ikawa ipo Micheweni. Akanambia kule watoto wameolewa mapema na wakaachwa mapema. Hakuna mtoto wa kulea watoto, kwa hivyo watoto wanalelewa na bibi na babu basi tena utakuta watoto wanahangaika.

Mhe. Subeti hapa anapiga kelele na kule NGO inapiga kelele. Watoto wadogo wameolewa, wakaachwa, mtoto mwenye ana miaka 13, 14 ana watoto wawili, hawawezi, anawatupa akatafuta maisha yake akaendeleza mengine. Hali hilisi ilivyo ndiyo hivyo. Lakini mtu hataki kusema ukweli anaanza kuficha ficha. Tuseme ukweli tuangalie, haya matatizo tunayo na ni lazima tuyatafutie dawa. Dawa yake ni kuweka sheria madhubuti kama hizi za kuweza kusaidia watoto wetu ili waweze kulelewa na waweze kupata haki zao za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, katika Sheria Nam. 76 ambayo inaliliwa hali naomba niisome:

> "Uwezo wa kutoa amri ya kuwasilia masharti ya sehemu hii hayatawahusu watu wanaofuata dini ya Kiislamu"

Sheria hii ya nchi na nchi hii ina wakaazi mbali mbali. Ina waislamu na wasiokuwa waislamu. Kipengele kimesema wazi, sasa sielewi mtu anakipinga kwa nini wakati kipengele kimesema wazi, sielewi mtu anakipengele kama hichi. Huyo Jaji huko Mahakamani ukifika huko akahukumu vipi. Kwamba wewe si Muislamu lakini ni lazima ufuate dini ya Kiislamu. Mashaka makubwa sana. Ule ni uhuru wa binaadamu haki za binaadamu hapo unaanza kuziharibu.

Vile vile tuangalie sasa kipengele cha 75. Katika sheria hii kuna kafala na kuna kuwasili. Wenye dini ya Kiislamu watafata kafala kama alivyotueleza kwenye semina Shekhe Soraga, kama kafala haikuanza leo, tangu enzi za Mitume, na hilo suala linakubalika na halina matatizo yoyote. Imesema hapa kwa kuzingatia vifungu vya sheria hii maombi ya kafala yatapelekwa Mahakama ya Kadhi. Mahakama ya Kadhi ndiyo inayohusu masuala ya Kiislamu.

Athari za kafala na wazazi imeeleza mpaka mwisho. Kafala Waislamu wote wanaotaka kwenda kulea watoto watakwenda kwa kadhi, watapewa watoto wale na watafuata dini ya Kiislamu. Wale waliokuwa sio waislamu hawatokwenda kwa kadhi, watakwenda Mahakamani kuwasili. Sasa tukisema sheria hii tutunge ya Kislamu wale wenzetu watakwenda wapi? *Adoption* kwa dini nyengine inakubalika na wala hakuna matatizo yoyote. Mtu kuanza kuibana sheria kwa misingi hiyo atakuwa hakuitendea haki sheria hii, wala hakulitendea haki Baraza hili tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, watoto wanabakwa na mpaka sasa hivi hakujakuwa na hata zile juhudi za makusudi za kukomesha masuala haya. Tunaamini sheria hii inayokuja itaweza kudhibiti kwa kiasi kikubwa masuala haya. Kubakwa Mhe. Mwenyekiti sio kwa wanaume tu kubaka hata wanawake. Kuna kubaka na kuna *abuse*, vile vile kuna *child abuse*. Kuna wanawake wanaitwa shugamani wana *abuse* watoto wanaume. Ukimwambia mbona mtoto huyu mdogo unamuharibu.

Anakwambia mtoto kwa baba ake na mama ake, kwangu miye mtu mzima huyo. Wakati mtoto wa kiume ana mia 14, mwanamke ana miaka 30, 40, mtoto wa watu kumuhamisha kwao anaye kwake kama keshaolewa.

Nasema kwamba sheria hizi na kanuni hizi ni muhimu sana kuzingatia yale mazingira halisi tuliyonayo katika masuala ya watoto. Watoto wanatelekezwa, wanahangaika, wamo katika shida, hawana walezi, hawapati chakula, hawapati malezi bora, hawapati elimu ni matatizo. Watoto wengi ambao wamepata misukosuko hiyo wengine wanakula madawa ya kulevya. Unapomuuliza anakwembia wazee wamenitelekeza sina la kufanya nimeamua kuingia kwenye madawa ya kulevya.

Nawaomba na nawanasihi ndugu zangu Wawakilishi wa Baraza hili tukufu kuangalia kwa kina suala la sheria hii. Sheria hii haijaweka vikwazo vya kuwa mtu asiolewe. Sheria hii haijakiuka maadili ya Kiislamu. Muislamu tekeleza dini yako kama ipasavyo, haijakuzuia fanya dini yako kama unavyotaka. Naomba tusiipeleke sheria hii katika dini wakati haijazuia muislamu kutekeleza dini yake ya Kiislamu.

Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitachukua muda wako mdogo tu. Kwanza nakupongeza kwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza. Leo ni mara ya pili naona fahari kwamba wanafunzi wangu wanakuwa viongozi wangu mbele ya macho yangu. Maana Baraza lililopita Mhe. Thuwaibah nae alikuwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina makubwa nilitaka kuongeza nguvu tu. Nalazimika kuchangia Mswada huu kwa sababu sisi Wizara ya Afya vile vile unatugusa. Matatizo mengi yanayotokana na watoto mwishowe huishia Wizara ya Afya hospitali. Bahati nzuri Mswada huu umezingatia sijui kama ni *one shop center au one stop center* tumekuwa mara nyingi Wizara tukilaumiwa kwamba unakosekana ushahidi wa kutosha, katika kutetea kesi ya watoto kuonewa. Kwa sheria hii sasa Wizara tumepata nguvu kwamba tumepata wenzetu tutashirikiana nao katika kulinda haki za mtoto.

Jambo la pili nililotaka kutia mkazo, nimesikiliza wajumbe wakijadili na jana kwenye semina tumejadili sana kwa urefu masuala ya watoto yanayohusiana na kubaka, kubakwa, ndoa. Lakini vile vile tunasahau kwamba kuna matatizo mengi ambayo zamani yakikaa kimya. Mimi huwa naji *refer* tukuvyokuwa sisi wadogo. Sidhani kama tulilelewa kwa sheria ya watoto, mimi sikumbuki. Labda kwa sababu nilikuwa mtoto, lakini sidhani kama kumekuwa na sheria ya watoto mpaka tumekuwa hivi.

Sisi tumekuwa hivi kwamba jamii yetu yenyewe ilikuwa ni sheria kutulea. Ninapokuwa nazungumza na wenzangu huwa nawambia kwamba si vibaya kusema kwamba tulikuwa watundu sana, hasa katika kutafuta embe za watu na matunda ya watu. Lakini unapofanya kitendo hicho mzee yule jioni yupo kwa mzee wako. Ni ukweli uliokuwa haupingiki, mama mzazi akiletewa ripoti na mzee wa mtaa, mtoto wako kaiba machungwa yangu au kaiba madafu. Mama anaificha ile siri kukulinda kwa baba maana utakiona cha mtema kuni baba mzazi akiambiwa kwamba umekwenda kuiba machungwa ya watu. Ile jamii yenyewe na wazazi walikuwa wanachukua hima ya kutaka tuwe watoto wazuri.

Mtoto akikosea kwenye mtaa, mzee yeyote anaweza akamrudi. Atamchukulia hatua na si ajabu atakwenda kumwambia na mzee wake kwamba mtoto wako nimemkuta anafanya kitendo hiki nimemrudi. Mzee na yeye anaweza akasema alah! Hukumpiga huyu. Wale wazee walikuwa wanaogopwa na watoto. Si kwa nia mbaya. Walikuwa wanaogopwa kwamba hawataki wazee tuingie katika mambo maovu.

Tujuulize kumetokea nini leo? Labda kwa kuwa walimu vijana. Mwalimu ampige mtoto kumrudi, si ajabu kesho baba mzazi akaja skuli akamwambia utamtambua. Kwa hivyo, hata yule mwalimu ile kazi aliyopewa ya kulea anaiogopa kufanya kwa sababu ya hali ya jamii ilivyobadilika, jamii imebadilika sana na kiasi hicho ndio kinatufanya sasa tutunge sheria ya kuwalinda watoto na kuwachukulia hatua mpaka hata hao wazee wanaowahusudu watoto.

Vile vile tumesahau hatusemi kuna wazee makatili kupindukia si mara moja wala mbili ndugu zangu nasikia mtoto anachomwa vikucha mpaka vinaungua anakuwa kilema kwa kuiba senti kumi, shilingi mia moja, shilingi mia mbili basi anachomwa moto. Haya nayo kama hatukuwalinda watoto basi itakuwa mtu sasa anafanya atakalo. Sheria hii inatupa nafasi ya kuweza kuwalinda watoto katika misingi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tunasemwa kina baba lakini sijui kuna kina mama nao sijui huchanganyikiwa anamzaa mtoto na tumesema hapa kwamba wazazi tunaumwa lakini huwaje yule mzazi aliyemtoa mtoto wake tumboni akenda akamtupa, yeye huwa haumwi. Lazima litizamwe pande zote mbili, lisitizamwe katika suala la kuona kwamba wanaume tu makatili lakini kuna na wanawake makatili kushinda hata wanaume mara nyengine. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ni msumeno iwalinde wote katika kuwalinda watoto hao.

Mhe. Mwenyekiti, tuna matatizo ya mabadiliko ya jamii lazima tukubali, sisi tulikuwa televisheni hatuijui, redio ilikuwa tukasikilize kwa mmanga kwenye

duka familia chache sana kama hazikwenda kwenye kituo basi nyumbani kuna televisheni ya watoto mbali, kuna televisheni ya wageni mbali na kuna televisheni ya baba mbali. Yaani jamii imekuwa kwa maneno ya Mkapa imekuwa *modernize* sio *development* maana *development* ni tofauti na *modernization* ni kwamba sasa hata watoto wadogo wana simu. Sisi tulipokuwa Makatibu Wakuu ilikuwa ukirudi nyumbani unaambiwa kuna simu yako imepigwa, lakini leo hapa hapa wakati upo hapa ukijificha tu hapa unaambiwa nitaonana na wewe saa moja.

Kwa hivyo, hali hii nayo inalazimisha serikali kufanya mambo ya kulinda jamii sio kwa sababu tu ya kutaka lakini ile *modernization* inatulazimisha. Sheria hii itakuwa na mambo machache, lakini angalau sasa unaweza kusema kwa sababu mtoto huyu nimemfanya hivi basi na wewe utafanywa hivi, huko nyuma kulikuwa hakuna hayo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo Mhe. Waziri jana kwenye semina mmelisahau kulizungumza kwa sababu yaliyozungumzwa tulitaka tuyapatie nafasi. Ni kwamba watu wamekuwa wakizungumza dini na sheria hii, lakini kuna suala moja la kuachwa radhi sijawahi kusikia mtu hata mmoja kulizungumza. Mhe. Mwenyekiti, tunaachwa radhi sio katika jamii yetu ipo hiyo.

Mimi nilimuuliza Shekhe Soraga pale katika mazungumzo nikamwambie Shekhe mazungumzo yako yote uliyosema mbona hukusema kwamba wewe mtoto huna adabu na wala huna radhi zangu na zinapata. Nikamuuliza hili unaliangaliaje katika ulezi wa watoto. Basi akanitolea hadithi akasema hadithi ya Mtume imesema adabu nyengine zote zinaweza kusubiriwa huko chini ya Mkunazi, lakini adabu ya mtoto kumkosea mzee mpaka akafika kuachwa radhi nasikia inapata hapa hapa. Kwa hivyo, kuna tabia vile vile ya wazee wengi kuitumia silaha ya radhi kama ndio fimbo ya kuwaumiza watoto, sina hakika hili mashekhe hapa kina maulamaa sijui tunaliangalia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niliseme hili kwamba limenyamaza kimya katika mazungumzo na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono mswada huu mia mbili juu ya mia kwa sababu mimi na Mhe. Zainab tuna kazi ya aina moja, nawashukuru sana.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji katika mada hii. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kukupongeza kwa mara ya kwanza kuweza kukaa kwenye kiti kikubwa hicho na kuweza kutuongoza vizuri katika majukumu haya ambayo tunaendelea nayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nimejaribu kutulia sana kusikiliza wajumbe wenzangu wanavyochangia michango mbali mbali kuhusiana na mswada huu wa mtoto. Kwa kweli mengi yamekwishakuzungumzwa na mengi yamekwishakufafanuliwa lakini mimi nina moja tu ambalo humu nimejaribu kulitafuta lakini sikuliona. Mimi nililokuwa nalo ni katika suala zima la mswada huu ni uhuru wa kuabudu kwa watoto. Mhe. Mwenyekiti, ziko baadhi ya ndoa ambazo zinafungwa na watoto hawa wanazaliwa na wazee ambao wana dini mbili tofauti.

Sheria mama inamlinda mtoto pale ambapo atakuwa na umri wa miaka 18, lakini kwa utaratibu wa mswada wetu huu kwa wale watoto ambao watakuwa wako chini ya umri huo na ambao watakuwa wanataka kwenda kuabudu lakini ukatokezea mvutano wa kidini baina ya baba na mama. Sijui Mhe. Waziri katika hilo ndani ya mswada huu analipa nafasi gani. Kwa sababu ni mambo ambayo yamo ndani ya jamii yetu na yanaendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni mimi sina la ziada isipokuwa naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Machano Othman Said): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kutoa maoni yangu katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikupongeze sana kwa mara ya kwanza kukalia kiti cha enzi nina hakika sote tumefurahi, tumeridhika na uendeshaji wa Baraza letu tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeanza kujadili mswada huu ambao unazungumzia haki, fursa na mambo mengine ambayo yanahusiana na hayo. Mswada huu mimi naweza kusema umekuja kwa wakati, mswada muhimu katika maendeleo ya watoto, pia utaimarisha haki za watoto katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu yao kwa hakika nchi yetu imebadilika sana hali ya matunzo ya uendeshaji na mazingira ya watoto yamebadilika sana. Maisha yao yamekuwa katika hatari kubwa kuanzia wao wenyewe watoto kwa watoto, lakini pia watoto na walezi na watoto na watu wenye umri wa utu uzima. Tumekuwa tukishuhudia vitendo ambavyo havistahiki kufanyiwa watoto, binafsi sisi Waheshimiwa Wawakilishi mmoja mmoja na kwa ujumla wetu tumepiga kelele sana, tumekuwa tukitetea sana lakini bado hali haijabadilika.

Tukiwa wakweli tutasema wazi wazi kwamba kila siku zikienda mambo yanazidi kuwa magumu hakuna unafuu katika maisha ya watoto kwa pande nyingi. Lakini jambo kubwa ambalo hivi sasa linawaumiza watoto kwanza ni kunyanyaswa kijinsia ikiwemo kubaka na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, suala hili linaenea kwa kasi sana na hapa tunapozungumza tusizungumze kwa kuwalenga watoto wa kike, lakini tuangalie na upande wa pili wa shilingi hata watoto wa kiume nao sasa hivi wanatendewa vitendo vibaya wakiwa katika umri mdogo na wanaumizwa sana. Kwa hivyo, sheria hii inaweza ikawa ukombozi kama itasimamiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, upande wa pili watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 18 na zaidi wale ambao wanaishi katika mazingira magumu wamekuwa wakipambana na tatizo la ajira katika umri mdogo. Suala hili la ajira katika umri mdogo linawadumaza na linawasababisha wakose elimu. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tafiti nyingi zimefanywa na zinajulikana Wilaya ambazo zinaongoza katika kuwatumikisha watoto katika umri mdogo.

Kwa bahati mbaya baada ya kuanza kupata pesa na wao wengine wanazifuata wenyewe ajira hizo lakini wengine wanatumwa na wazee wao kufanya ajira hizo, na wengine kwa bahati mbaya wanaingia wanaingia katika ajira hizo. Kwa kuwa na sheria ambayo itaweka kinga kwa watoto hili ni jambo zuri na serikali inastahiki pongezi. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba ni jambo jema sana kwa serikali kuleta mswada huu ambao utakuwa ni kinga kwa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, sisi sote humu ndani ni wazazi ni kweli ni wazazi lakini sisi ni walezi, wakati mwengine unaweza kuwa mzazi usiwe mlezi na unaweza kuwa mlezi usiwe mzazi. Lakini nafasi ya ulezi ni jambo muhimu sana kwa sababu unaangalia mwenendo na taratibu zote za mtoto. Watoto wana haki ya kupata malezi bora ikiwemo malazi, mavazi na elimu. Kwa bahati mbaya haki hizi zinadhibitiwa na walezi ama uwe mzazi wa mtoto ama mlezi wa mtoto, si aghlabu kwa mtoto kudai zaidi hapa petu Tanzania na Zanzibar kwa watoto wa Kizungu wanadai lakini kwa huku kwetu mtoto hawezi kudai kwamba leo lazima nipate hiki au nifanye hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hawadai maamuzi ya nini wapate watoto tunayo sisi wazazi na walezi, lakini wakati mwengine hata wale wazazi ambao wana uwezo wa kuwahudumia watoto vizuri hawafanyi hivyo, hivyo wasipofanya hivyo ndio watatoa mlango wazi kwa vijana wao kuharibika zaidi. Kwa hivyo, mimi niwaombe wazazi wenzangu na walezi wenzangu kwamba tujitahidi sana kutoa fursa na vijana wetu kupata elimu, kupata malazi bora na kupata mavazi mazuri. Mhe. Subeit Khamis Faki pale alisema kuna watoto wengine miaka 9 sio watoto wanakuwa ni watu wazima. Mimi kwa hili nataka nipingane nae

kidogo miaka 9 kwa hali yoyote bado ni mtoto hata kama ana umbile la aina gani bado ni mtoto na hastahiki kuolewa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi kusoma ni muhimu zaidi kuliko kuolewa nafasi ya kuolewa itakuja na nafikiri hata dini na huko kusoma pia imetia msisitizo. Nilimsikia Mhe. Mazrui kwamba alikwenda Micheweni na mimi pia nilikwenda Disemba 1 mwaka jana nilialikwa basi nilipata mashuhuda pale katika uwanja wa Shaamemata watoto wadogo wamebeba watoto wengine mgongoni. Nikawauliza vipi hawa wanasema sio ndugu zetu hawa hawa ni watoto wetu, lakini mtu kaolewa ana miaka 14 miaka 15 au 16 ameshachwa tena ana mtoto. Mhe. Mwenyekiti, ili amlishe mtoto wake lazima azunguke Micheweni tena akifika miaka 17 ana mtoto wa pili, akifika miaka 20 ana watoto 4 ndio hajiwezi kabisa na hao watoto wanakuwa wanne lakini wana miaka kati ya mmoja na miaka minne au mitatu na miezi tisa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tatizo la umasikini unalizidisha zaidi maisha yanakuwa magumu na jamii inaanza kumuona kwamba hajali watoto wake, lakini ukweli ni kuwa hawawezi. Hili pia linasababisha sasa tatizo jengine kwa mzazi nae kupata maambukizo ya maradhi ya ukimwi ama kuzoofika kwa lishe duni. Juzi tuliambiwa wakati tunapewa semina ya chakula na lishe kwamba maeneo ambayo yanaongoza kwa kuwa na wanawake wenye wepesi mdogo zaidi ni Micheweni. Kwa nini? Kwa sababu watoto wanazaa watoto wenzao. Mimi naomba suala hili lisitufanye tukaingia hofu kwa wapiga kura wetu hata huko Micheweni nina hakika kwamba na wao wanataka malezi bora, wanataka maisha bora, wanataka kusoma na watoto wanataka kukua katika makuzi mazuri.

Kwa hivyo, mimi niwashawishi Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwamba mswada huu tuukubali kama ulivyo na tumuunge mkono Mhe. Waziri na timu yake waende wakamalizie shughuli zilizobakia kwa kupelekewa Mhe. Rais kuweka saini na kuanza kutumika kama sheria ili na watoto na wao waone kwamba tunawajali. Watoto lazima tuwajali kwa sababu kama watoto wa nchi hii wataharibika tutakaoathirika ni sisi, sisi hatuwezi kuwa viongozi maisha yetu yote, tunaongoza kwa muda tu leo tuko sisi lakini kuna rika linakuja kuongoza. Sasa kama rika lijalo kutuongoza haliwezi kuongoza kutakuwa na nchi, kama rika lijalo halina sheria za kuwalinda hivyo kutakuwa na nchi ya kuendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine kwenye ushindani tunasema huyu asije ili mimi nibakie lakini katika mambo haya ya kuendesha nchi huwezi kuweka vigenge vya kusema kwamba hawa wasije au waje katika udhaifu ili mimi niendelee kuongeza kwa muda mrefu, lazima utafika wakati utang'oka watakuja wenzako lakini ni bora aje mtu ambaye aliyekuzidi wewe aongoze

vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, niombe kwamba malezi lazima tuyaekee msingi na ikiwezekana kwa watu ambao wana uwezo basi asilimia angalau 50 ya mapato yao wayatumie katika kuwaekea mazingira mazuri watoto wao ili na wao waje wawasaidie baadae. Kwa sababu sasa hivi kutokana na hali ya kimaisha inavyokwenda leo tunazungumzia mswada wa watoto, lakini baada ya muda tutakuja hapa kuzungumzia mswada wa kuwalinda wazee. Kwa hivyo, hatuwezi kuja kuzungumzia wazee kama hatujazungumzia leo watoto na tukizungumzia watoto tukiona mambo yanakwenda vizuri tutakuja kuzungumzia wazee na miongoni mwetu tutakuwemo kwamba hawa ni wazee ambao wanataka kulindwa na sheria. Kwa hivyo, mimi naomba tuendelee na hili jambo lisiturudishe nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo linatusumbua sana tunalo tatizo wakati wazazi wanapotengana watoto wadogo wanatanga tanga sana, wanasumbuka sana hawajui waende wapi. Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine kunakuwa na kinyanganyiro cha mtoto kati ya familia ya baba na familia ya mama. Kwa hivyo, shida inakuwa kubwa na wenye kupata madhara ni watoto wenyewe. Kwa hivyo, naomba basi hili nalo waheshimiwa tulione kwamba ni tatizo na tuliunge mkono kwamba sheria isonge mbele katika kutekeleza suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza bahati nzuri Mhe. Waziri wa Afya kalizungumza na Mhe. Hija pia alilizungumza la kuwa na mnyororo wa taasisi za kiserikali na za kijamii katika kushughulikia matatizo ya watoto. Shida ambayo ipo baadhi ya taasisi za serikali na za kijamii hazitowi mashirikiano mazuri wakati watoto wetu wanapatikana na shida zaidi za kubakwa. Mimi mwenyewe nilikuwa nikizungumza siku zote kwamba Wizara ya Afya kuna siku maalum za Alhamis ndio mtoto anapelekwa kupimwa lakini bahati nzuri juzi nimesikia kwenye redio wanasema kwamba hakuna jambo hilo sasa hivi. Siku yoyote mtoto anaweza kupelekwa hospitali akachunguzwa kama amefanyiwa kitendo kibaya anajuulikana kama hakufanyiwa anajulikana yanakwisha. Kama ndivyo ilivyo basi mimi naunga mkono suala hili kwamba iwe ni siku zote na ikiwezekana kuwe na daktari maalum anayeshughulikia matatizo haya ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti, pia polisi, masheha, jamii mitaani na Idara yenyewe ya Ustawi wa Jamii hizi ni taasisi muhimu sana katika kuhakikisha kwamba madhila kwa watoto hayaendelei Zanzibar, watoto ambao wanapata mazila wanasaidiwa na sheria inachukua mkondo wake. Tuna tatizo la kijamii kwenye familia wakati mwengine yakitokezea matizo haya zinakutana familia wanataka kulimaliza nje ya taratibu za kisheria kwamba huyu mtoto wa mjomba, huyu mtoto wa shangazi mimi nafikiria mambo yale sio mazuri hivyo sheria ichukue mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi kwamba katika sheria hii tunazungumzia kuwepo kwa Mahakama ya Watoto na nizungumzie kwa mambo mawili ambayo baadhi ya wajumbe hapa wameleta mjadala mzito kwamba hayastahiki kwa nchi likiwemo hili la kuathiri mtoto. Kama walivyozungumza wenzangu tukisoma sheria kifungu Nam. 76 (1-3) ya sheria hii nina hakika sote tutajiridhisha kwamba jambo hili halituumizi na naomba lisituumize vichwa. Limezungumzwa wazi wasi na sheria kwamba hii litakuwa kwa wale watu ambao sio waislamu tena tumepata bahati sana kwamba sheria mpaka imetubainishia hasa kwamba kwa wale waliokuwa sio waislamu, pengine sheria ingelikuwa kimya tungeliweza kusema jamani hili jambo lina matatizo waislamu litatuumiza, lakini limebainisha kwa wale ambao sio waislamu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu 94 kinazungumzia hata waliokuwa waasili wenyewe sio kwa mgeni inatakiwa ifanywe kwa wenyewe mgeni haruhusiwi. Mwaka juzi nchini Malawi alikwenda Madona akaomba mtoto pale kukawa na mvutano wa kinchi lakini baadae alimchukua nafikiri sasa hivi anae huko Ulaya, lakini bahati nzuri kule Malawi wao serikali yao sio kama yetu wao wana dini zao na sisi tuna dini yetu. Mhe. Mwenyekiti, ingawa hatutamki moja kwa moja na sisi nchi yetu haiongozwi na sheria ya Kiislamu lakini kutokana na silka zetu, utamaduni wetu ndio tunajielekeza huko. Lakini sheria yetu hii imetamka na imetoa fursa na kwa waislamu wamepewa fursa yao ya kufanya kwamba wewe kama muislamu basi zungumzia katika kafara, huko huna tatizo utafanya kutokana na sheria ya dini ya kiislamu hakuna mtu ambaye atakuzonga wala hubughudhiwi na mtu.

Kwa hivyo, nafikiri Waheshimiwa Wajumbe nawashawishi sana kwamba tukubaliane na mapendekezo ya Mhe. Waziri kwani ni mapendekezo mazuri unajua jambo likishafafanuliwa na likawekwa wazi basi wewe mwenye dini nyengine linakuwa halikuathiri wala halileti maneno. Kwa sababu tukizungumzia hili tunaweza tukazungumza mambo mengi ambayo yako Zanzibar ambayo sheria inayaruhusu na sio ya dini yetu yanafanywa na hatuna matatizo nayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nizungumzie kuhusu umuhimu wa kuwepo vituo vya kuwalea watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu. Bahati nzuri tunavyo vituo hapa tulikuwa na kituo cha Forodhani, lakini bahati njema kabisa tumshukuru sana Mhe. Mama Shadya Karume baada ya kuona udhaifu wa kile kituo na udogo wake akaamua kujenga kituo kizuri cha kileo ambacho kipo hapo njia ya Mombasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bahati nzuri nimeshawahi kukitembelea nimeridhika sana na hali ya mle ndani, mle ndani kuna vyumba vikubwa vya kutosha, kuna

vitanda, kuna sehemu za kuchezea na kuna sehemu za kufanyia ibada. Kwa hivyo, mle wanajitosheleza kwa mambo mengi sana na huduma za maji na mambo mengine yapo pale ya kutosha. Kwa hivyo, nafikiria kwamba kila serikali ikipata uwezo tuwe na vituo kama hivi na vyengine vya kurekebisha tabia za watoto maana yake pale nafikiri hapana watoto watukutu kuna watoto wema ambao maisha yao ni magumu. Lakini ni vyema kuwa na vituo vya kuwalelea watoto watukutu ambao maisha yao yameharibika. Kuna vijana wengine wadogo sana wanavuta bangi, wanatumia madawa ya kulevya, hawasomi chuoni wala hawaendi skuli. Kwa hivyo, hawa lazima wapatiwe nafasi ya kulelewa katika vituo ambavyo vitawabadilisha maisha yao na wapate fursa za kusoma.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wapo wenye uwezo wao walikuwa wakichukuwa watoto wao wengine wanaipeleka Kenya kwenda kuwabadilisha maisha yao katika vituo vya huko nje na mazingira waliyoyazoea wenyewe, lakini hawana budi wanatumia fedha nyingi wanakwenda huko. Nafikiri na hapa tutafute maeneo yaliyokuwa tulivu ili tuanzishe vituo hivi hata kama kwa ada ndogo kwa wale ambao wana wazee walipe lakini ni muhimu kwamba wawekwe ili wabadilishwe tabia zao ziwe njema na waweze kusoma ili baadae waweze kuja kulitumikia taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimalizie kwa kuwaomba wenzangu kwamba tuuchangie mswada huo kwani ni mzuri wala tusione kwamba Mhe. Waziri na timu yake wamekurupuka huu ni mswada ambao ni mzuri, utatusaidia na bahati nzuri kama alivyosema Mhe. Waziri umepata fursa ya kujadiliwa na viongozi wa dini, wametoa maoni yao, wameukubali na kuafiki kwa hivyo na sisi Waheshimiwa Wawakilishi hatuna hoja ya kuukataa mswada huu. Baada ya maelezo yangu hayo machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chumbuni mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia.

Mhe. Ismai Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote kabisa nikupongeze kwa dhati kabisa kutokana leo kwa mara ya kwanza kukalia kiti hicho ukitekeleza kazi zako kama mwenyekiti. Hii inaonesha kwamba wanawake hata bila ya kuwezeshwa wanaweza wao wenyewe. Kwa hivyo, nakupongeza sana kwa hilo mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nitumie fursa hii kuchangia machache kuhusiana na mswada huu unaohusu Mswada wa Sheria ya Mtoto itakayotoa haki na maslahi bora ya mtoto, itakayoshughulikia watoto na matatizo ya sheria, ulezi, ukaaji, kumuona na kumlinda mtoto na mambo mengine mengi yaliyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwanza nampongeza waziri na serikali kwa ujumla kwa hatua hii iliyofikia ya kuleta mswada huu muhimu kuhusu kuweka haki za mtoto na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Lakini pamoja na kumpongeza waziri na serikali kwa hatua hii, niseme kwamba nadhani kuna baadhi ya maeneo tunahitaji kuyaangalia vizuri.

Mimi nimebahatika nilisomea fani ya sheria ingawa si mwanasheria *by professional* kwa sababu sifanyi kazi za sheria. Tulipokuwa tukisona huko kuna somo linalohusu *human right* (haki za binadamu) na katika hili kuna nadharia mbili zimejikita, kuna ile dhana ya *universality of human right*, kwamba haki za binadamu popote zilizpo kwa watu wote ni sawa sawa na kule ile dhana ya *volatility of human right* kwa maana ya kwamba kuna mahitaji maalum na jamii maalum kutokana na tamaduni zao na mambo yao wanatafsiri kidogo inatofautiana katika baadhi ya mambo, haigusi haki za msingi. Kwa mfano, haki ya kuishi, haki ya mtu kutafuta, lakini kuna mambo ambayo yanazingatiwa kwa misingi tofauti.

Niseme katika hili achilia mbali kwa nchi zetu Mhe. Mwenyekiti, hata katika ulimwengu wa Magharibi bado kuna mvutano mkubwa juu ya dhana ipi itumike na wao wenyewe hawakubaliani moja kwa moja juu ya huo msingi wa *universality of human right*. Nalisema hili Mhe. Mwenyekiti, kama utangulizi ili tusionekane kama watu wa ajabu tunapohoji baadhi ya vitu au kutaka pafanywe marekebisho kulingana na mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, imezoeleka kwamba Marekani ni katika nchi inayosifiwa sana katika misingi yake ya haki za binadamu, angalau ilivyo katika sheria. Na watetezi wakubwa wa msingi huu wa haki za binadamu kuwa sawa kwa wote, lakini mpaka leo katika ulimwengu wa Magharibi kuna mvutano juu ya Marekani kuwa na sheria inayoruhusu mtu kuhukumiwa kifo. Sio Waisilamu tu wanaohojiwa katika hili, hata Marekani ina sheria ya kuruhusu kifo, ikiwa kunyongwa, ikiwa kwa kutumia sindano, wao wanatumia kudunga singano mara nyingi kwa utaratibu wao. Lakini hili linahojiwa na miongoni mwa nchi za Magharibi kwamba je, kwa kufanya hivyo Marekani inaheshimu haki za binadamu?

Kwa hivyo, nasema tusionekane kama vile watu wa ajabu tukihoji baadhi ya vitu, haya ni mambo ambayo hakuna nadharia moja, duniano kwenyewe huko kwenye ulimwengu wa Magharibi kuna tofauti za mtazamo katika masuala haya.

Sasa kwa nini nalisema hilo Mhe. Mwenyekiti? Hoja iliyojengeka katika jamii za nchi za Mashariki na nikisema Mashariki hapa sikusudii zile ziliyoko chini ya *Sovieti*, ulimwengu mara nyingi unatizamwa baina ya *West* na sisi tuliobakia

sote tukaingizwa katika *group* moja la nchi za *East.* Kwamba kwetu sisi tofauti na wao na hivi sasa kuna haki na wajibu na wenzetu huko walikotoka walikuwanayo hayo, lakini wakayaachia mpaka leo wengine wanafika kuandika makala na tafiti za kisomi wakijutia kuacha misingi iliyokuwa ikijenga jamii zao kama *community* kama jamii. Kwa sababu suala la wajibu linakuja katika jamii.

Nakumbuka wakati nasoma pale Uingereza mimi palikuwa na mjadala mkali sana kuhusu utovu wa nidhamu uliojengeka katika skuli zao, utomvu wa nidhamu wa watoto kwa wazazi wao kwa sababu ya kuendekeza mno haki na kusahau wajibu. Nakumbuka wakati wa awamu ya tatu niko mwanafunzi hapa moja katika usemi maarufu uliokuwepo wakati ule alikuwa Rais wa Awamu ya Tatu Mhe. Ali Hassan Mwinyi alisema, ‘ haki na wajibu ni watoto pacha’. Sasa nimetumia muda mrefu kulieleza hilo kidogo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu naona sheria hii imejikita mno katika kuzungumzia haki, lakini katika wajibu iko kimya.

Kuna kifungu kimoja nadhani kama sikosei cha 17 kinazungumzia majuku ya jumla ya mtoto. Lakini hata hiki hakikuandikwa katika hali ya kutilia nguvu kama vile vifungu vinavyozungumzia haki vilivyoandikwa haki za mtoto. Sasa hapa mimi napata mashaka kidogo, kwamba mara nyengine kwa sababu ya hoja hizi za kwamba tumeridhia mikataba ya kimataifa kama tunafungika, labda hapa tujifunze kitu. Kwa sababu unapokwenda wanaokwenda kuridhia mikataba ya kimataifa si Zanzibar ni Jamhuri ya Muungano, hapa Mhe. Mwenyekiti, pana matatizo katika hili.

Siku moja niliwahi kuhoji nilipokuwa Mbunge kwamba nafasi ya Baraza la Wawakilishi katika kuridhia mikataba ya kimataifa kwa mambo yasiokuwa ya Muungano kwa Jamhuri ya Muungano iko wapi? Hapa ndipo linapokuja tatizo hili Mhe. Mwenyekiti. kwa sababu kwa wenzetu kwa mila zao inawezekana wao wakaona ni sawa tu, lakini katika sheria za kimataifa kuna suala la ku-*opt out* katika mikataba, kwamba kuna vifungu fulani hiyo mikataba ya kimataifa inayozungumzia haki wewe una haki ya kusema hiki mimi sikiridhi, naridhia mkataba wote lakini moja, mbili na tatu sikiridhii na ndio zilivyofanya baadhi ya nchi za wenzetu ambao tunalingana katika tamaduni zetu.

Sasa sisi kwa sababu ya kukosa haki ya kuridhia mikataba ambayo inahusu mambo yasiokuwa ya Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano tunapata matatizo kama hayo Mhe. Mwenyekiti. Tunaletewa vitu kwa jumla jumla tunaambiwa tu-*adopt* kwa sababu vimetoka katika mikataba ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa nasema suala la wajibu halikupewa uzito wake, nimesema kifungu cha 17 kinasema hivyo, lakini tizama kilivyoandikwa.

Kifungu cha 17 kinasema:

> "Katika matumizi ya sheria hii, na katika mwenendo wowote, vitendo na maamuzi ya chombo chochote cha umma kuhusu mtoto vitaangalia dhamana na majukumu ya mtoto ya:

Sasa haisemi tu kwamba huu ni wajibu wa mtoto, kwanza wametumia lugha ya majukumu tofauti na kule kwenye haki. Halafu imeweka katika hali ambayo kwamba majukumu yenyewe haya yanawekwa kwa dhamira tu ya kuwezesha hicho chombo ambacho kitakuwa kinaamua, pengine mahkama au chombo chengine chochote katika sheria hii kizingatie zile haki na haya, lakini haiweki wazi wazi kwamba na mtoto naye ana wajibu huu kwa wazazi wake, familia yake, kwa jamii anayoishi.

Mhe. Mwenyekiti, hili si jambo geni, hata katiba yetu hii imetaja haki za binadamu tena ni katiba nzuri katika *bill of right*, lakini katika kifungu cha 22, 23, 24 inataja pia wajibu wa raia. Kwa sababu kama nilivyosema katika jamii zetu sisi tumejengeka hivyo kutambua haki na wajibu. Kwa hivyo, hiyo naomba Mhe. Mwenyekiti, lizingatiwe na waziri atapokuja kufanya majumuisho atwambie hapa vipi tutazingatia kikamilifu masuala ya wajibu wa mtoto kulingana na malezi yetu, kulingana na *customary law* zetu ambazo zina nafasi katika sheria yoyote katika dunia.

Customary law zinatambulika, tusione aibu kuzi-*adopt*, *customary law* kwetu sisi zinajumuisha na maadili ya Kiisilamu na hilo Mhe. Mwenyekiti, si aibu. Hata katika hizo jamii zinazotaka kutusukumizia hizi katika nchi zao wanaheshimu hilo. Ukienda Uingereza kwa mfano, ule msingi wa kutambua *Anglican Church* kwamba ndio msingi wa jami pale uko, katika *house of law* za Uingereza Mashekhe hawamo mule, lakini Maaskofu wa *Anglican* wanatambulika kwa nafasi zao kuwemo katika *house of law.* Sasa kila nchi ina misingi na tamaduni zake, kwa nini katika nchi hizi hayatambuliwi iwe ni kiroja kwamba sisi tukidai masuala kama hayo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo Mhe. Mwenyekiti, ulitazame vizuri.

La pili Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya tafsiri za maneno. Kwa mfano, katika kifungu cha 12(2)(c) kinachozungumzia kumkinga mtoto na utelekezaji, ubaguzi, utumiaji nguvu, udhalilishaji, kumuepusha na madhara ya mwili na maadili na ukandamizaji. Sasa hizi ni zana nyingi zimetajwa hapa, lakini ukienda katika tafsiri hazikupewa tafsiri zilizopewa tafsiri zile za udhalilishaji wa mtoto, sasa haya mengine maana yake nini katika maana ya kisheria itapokuja kuwa *on forced* sasa katika mahkama mtoto anadai kwamba

kadhalilishwa, kateswa, katumiliwa nguvu, inawezekana kesho kumrudi mtoto katika nyumba akasema katumiliwa nguvu na mzee wake, katika tafsiri huku hatukuweka tukafafanua nini kinachokusudiwa.

Kwa hivyo, nasema kuna zana nyingi unazikuta katika hivi vifungu. Kwa mfano, kudhalilisha hata ukija katika tafsiri ya kudhalilisha kuna udhalilishaji watoto na udhalilishaji mtoto zina tafsiri tofauti, sijui kwa nini kama ikiwa *plural* ina maana tofauti na ikiwa *singular* sielewi hilo na katika vifungu vya utangulizi unalikuta. Kwa hivyo, naomba waziri atufafanulie hizi zana zilizotajwa kwa wingi humu tutazielewa vipi katika mukhtadha wa sheria hii itakayopelekwa wakati mtoto keshadai kwamba anadhalilishwa aweze kulindiwa haki zake.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, nije katika hili eneo ambalo limepigiwa kelele sana suala la kuwasili, kifungu cha 76 – 96. Mhe. Mwenyekiti, hapa na mimi pamoja na maelezo mazuri ya mawazidi kujitahidi sana kuupigia debe mswada huu bado sijashawishika. Kifungu cha 76 kinaanzia kwa kusema, masharti ya sehemu hii hayatawahusu watu wanaofuata Dini ya Kiisilamu, tunaambiwa kwa hoja hii hatuna haja ya kuwa na wasi wasi, Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi upo. Kwa sababu kwanza tunasema masharti ya sehemu hii hayatahusu watu wanaofuata Dini ya Kiisilamu, watu hapa ni wepi? Hawa wanaotaka kuwasili, wenye mtoto wanaotaka kuwasiliwa au huyo mtoto mwenyewe anayetaka kuwasiliwa?

Tatizo la vifungu hivi vya 76 – 96 vyote vinahusu mambo ya kuwasili hapa, ni kwamba tunachukulia kama vile kuna mpaka ulio wazi baina ya pengine familia za Kiisilamu na zisizokuwa za Kiisilamu. Lakini imeelezwa hapa kwamba katika jamii yetu ni jambo la kawaida kwamba tuna familia za mchanganyiko, sasa ukipata familia hiyo na pengine ndoa yenyewe haikudumu mtoto, baba Muisilamu mama tuseme Mkiristo, huyu anaingia katika mkumbo gani? Atakuwa vifungu hivi vya kuwasili vina-*apply* kwake au havi-*apply*? Kwa hivyo, vifungu hivi bado vina matatizo na mimi naomba hili Mhe. Waziri aje atupe maelezo ya kutosha hapa kwa sababu kama nilivyosema hatuwezi kupitisha mambo ambayo kesho yatakuja kutufanya tujekuwa mas-uuli katika mambo ambayo ya kuridhia kwa sababu tu ya kulazimishwa na mikataba ya kimataifa.

Lakini hata kama katika maelezo vitabakia Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na hoja moja vile vile kwamba, ikiwa kila tukikaa tunazungumzia ‘kafala’ mimi napendekeza kwamba tuseme hata kwa hii ‘kafala’ basi isemwe kwamba atakaeruhusika kulea huyu mtoto tunaemruhusu kwenye sheria awe ni Mzanzibari tu, sio raia wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu katiba yetu imeweka tafsiri ya Mzanzibari. Kwanza masuala haya si masuala ya Muungano

hivyo sioni kwa nini sheria hii iwape haki raia wasiokuwa Wazanzibari kuja kumlea mtoto kwa 'kafala' ambapo utakuwa huna dhamana naye tena. Kwa sababu kesho na keshokutwa likitokea tatizo hapo utakuja kuwa hujui mahkama ipi inasimamia, Mahkama Kuu ya Jamhuri ya Muungano ambayo kwa hakika si Mahkama Kuu ya Tanzania Bara au ni Mahkama Kuu ya Zanzibar, hasa ikizingatiwa kwamba Zanzibar tuna Mahkama za Kadhi na kuna mambo ya Kiisilamu yanayosimamiwa na Mahkama za Kadhi na Bara hakuna Mahkama ya Kadhi.

Kwa hivyo, tutaposema tu kwa maana ya Jamhuri ya Muungano kuna uwezekano mkjubwa wa kuja kuleta mgogoro wa kisheria katika kuja kusimamia vifungu hivi litapokuja kutokea tatizo lolote. Kwa hivyo, naomba pia katika hilo liingizwe pamoja na kwenye 'kafala', kwamba watakaohusika kuruhusiwa kulea mtoto huyu wawe ni Wazanzibari tu Mhe. Mwenyekiti.

Katika kifungu cha 108 Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba nizungumzie kwa pamoja katika kifungu hiki kidogo inahusika na kifungu cha 109. Mhe. Mwenyekiti, hapa panazungumziwa hapana mtu ambae ni mmiliki au mkaazi au anafanya, au ni msimamizi wa ukumbi wa muziki, pahala pa kuuza ulevi au klabu za usiku atakaemruhusu mtoto kuingia katika ukumbi wa muziki, pahala kuuza ulevi au klabu za usiku. Halafu katika kifungu cha 109 ukisoma pia kifungu kidogo cha (4) kilichoko ukurasa wa 173 pale kinachosema hapana pombe au bidhaa za tumbaku zitakazouzwa kuhudumiwa au kuwepo kwa ajili ya watoto walio chini ya umri wa miaka 18 katika sehemu za michezo na mapumziko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu katika vifungu hivi ni kwamba, sheria hii isiishie hapa tu, katika kusema kwamba mtoto asiruhusiwe kuingia katima maeneo hayo, nadhani twende hatua moja. karibuni tumeona mambo hapa ambayo yameleta mjadala mkubwa sana katika nchi yetu, ni suala zima la kuruhusu shughuli za aina hii katika maeneo ya wakaazi ya watu.

Kwa hivyo, kama kweli tuna dhamira ya kumlinda mtoto mimi nasema tusiishie tu kusema mtoto asiruhusiwe kuingia katika mambo hayo, lakini sheria twende hatua moja, kwamba katika kuwalinda hao watoto masuala haya ya kuwa na baa au sehemu za kuuzia pombe, kuwa na klabu za usiku na vitu vyengine vya usiku visiruhusiwe kisheria katika maeneo ya wakaazi. Tukifanya hivyo Mhe. Mwenyekiti, hata ile mizozo iliyokuwa haishi kila siku ya kwamba mambo haya mpaka watu watoke jamii nzima watu watoke wende katika Mahkama ya Vileo kwenda kubishana yataondoka.

Kwa hivyo kama tunataka kumlinda mtoto tuanze kumlinda hapa, sio tu kwamba akingwe asiingie lakini tupige marufuku kuwepo kwa vitu vya aina hii katika maeneo ya makaazi ya watu.

Falafu la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anifafanulie, hapa katika mjadala tangu katika semina mpaka hapa palizungumzwa sana juu ya tafsiri ya mtoto. Hili mimi nililiacha kwa makusudi kwa sababu sijui kama napata tafsiri sahihi katika kukidhi haja za pande zote mbili zilizokutana, baina ya wale wanaosema kwamba tufuate sheria zile zinazosema kwamba mtoto akibaleghe si mtoto tena au kwamba tafsiti ya mtoto ni mtu yoyote aliyekuwa chini ya umri wa miaka 18.

Mimi naona hapa na bahati mbaya nataka nikiri mbele yako sikupata nafasi ya kuzitizama hizi, lakini nikienda katika madhumuni na sababu moja katika maelezo yaliyokuwepo pale yanasema sheria hii pia itafuta sheria ya watoto ya watoto vijana sura ya 58 ya mwaka 1952. sasa nataka nikiri kwamba mimi sikuwahi kuzipitia hizi, lakini nilikuwa naona kitu cha kutusaidia hapa, kwamba ikiwa katika mwaka 1952 tuliweza kutofautisha baina ya watoto na watoto vijana, kwa nini tusichukue tafsiri hizi tukaziingiza katika sheria hii kwa vifungu tofauti vile ambavyo vitakuwa vinawahusu watoto na watoto vijana.

Mimi naamini kwamba hapa imewekwa hivi kwa sababu bila shaka ilizingatia jamii yetu ilivyo. Kwa hivyo, nasema tumekuwa tukivutana sana hapa kwa tafsiri ya mtoto hebu waziri akija atusaidie ile sheria ya mwaka 1952 iliwatenda vipi na kuwabagua baina ya watoto na watoto vijana ili baadae tuone kama inaweza kusaidia katika sheria hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kama nilivyosema mwanzo sina matatizo na sheria naunga mkono kwa kuletwa mswada wa sheria hii ili tuupitishe, lakini hayo maeneo ambayo mimi na wenzangu tumeyataja tunaomba kwa dhati kabisa watazamwe ili tupate sheria itakayokuwa nzuri, itakayotufanya tutimize matakwa yetu kwa upande mmoja katika kutekeleza mikataba ya kimataifa lakini pia isitupeleke katika kuachana na maadili yetu maadili ambayo kitu kikubwa yametokana na misingi ya Dini ya Kiisilamu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: nakushukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe najua kuna wengi ambao bado walikuwa na hamu ya kuchangia, lakini tukumbuke kwamba muda tunao kesho na keshokutwa. Kwa hivyo, kwa wale ambao wameleta majina yao lakini hawajapata fursa ya kuchangia *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho tutaendelea. Kwa leo kwanza nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu wenu na hekima kwa keli nawashukuru na *Inshaallah*

Mwenyezi Mungu atatujalia zaidi ya haya kesho tutachangia ili kuhakikisha kwamba mswada huu wa watoto wetu unapita na kuweza kuanza kufanya kazi haraka iwezekanavyo kwa sababu tunauhitaji. Nawashukuru wajumbe wote.

(Saa 1:45 usiku Baaraza liliahirishwa mpaka kesho tarehe 29/03/2011 saa 3:00 asubuhi)